# Nipashe

Jumatatu Novemba 11, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580069

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US







## Spika azitaka PAC, PIC, LAAC kumpa ushirikiano CAG Kichere

UKURASA 3

UKURASA 13



UCHAGUZI S/MITAA:

# Serikali yaagiza waliotenguliwa sasa kushiriki

• **Upinzani** watoa masharti, NCCR yajitoa... *Ukurasa.2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 24

**WAGANGA WAFAWIDHI KUSAKWA TUHUMA ZA WIZI MALI YA UMMA**

BARAZA la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Kakambo mkoani Rukwa, limemwagiza mkurugenzi wa halmashauri hiyo na Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwakamata waganga...

## Hoja nne zilizotikisa bungeni

UKURASA 7



Rais mstaafu Jakaya Kikwete, akiangalia wataalamu wa afya wanavyofanya utafiti wa maambukizi ya malaria katika Taasisi ya Afya ya Ifakara (IHI) eneo la Rufiji mkoani Pwani, wakati wa ziara ya ujumbe wa Taasisi ya Ushirikiano wa Viongozi wa Afrika dhidi ya Malaria (ALMA) walipotembelea taasisi hiyo mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu


## Ofisi ya Mtendaji yachomwa

• **Wachomaji** waacha msokoto wa bangi, kibiriti... *Endelea uk.2*


**MICHEZO** **VITA UBINGWA BARA MAPEMA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Waliotenguliwa sasa kushiriki uchaguzi mitaa

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amewaagiza wasimamizi wa uchaguzi kuhakikisha wagombea wote walioteuliwa na kudhaminiwa na kufanikiwa kurejesha fomu zao za uteuzi kwa wasimamizi wasaidizi wanaoshiriki katika uchaguzi huo.

Aidha, amesema wagombea ambao hawatashiriki katika uchaguzi huo ni wale ambao walibainika kuwa na makosa kama kutokuwa raia wa Tanzania, wamejidhamini wenyewe, wamejiandikisha mara mbili, hajadhaminiwa na vyamaa vyao vya siasa, wamerejesha fomu watu zaidi ya mmoja kutoka chama kimoja.

Jafo aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tathmini ya uchukuaji na urejeshaji fomu, uteuzi, pingamizi na rufani lililoanza Oktoba 29 hadi Novemba 9, mwaka huu.

"Kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi za serikali za mitaa, Tangazo la Serikali namba 371 na kanuni ya 49, wagombea wote ambao walioteuliwa na kudhaminiwa na vyama vyao na kufanikiwa kurejesha fomu zao za uteuzi kwa msimamizi msaidizi wa uchaguzi katika kipindi kilichokuwa kimepangwa cha kuchukua na kurejesha fomu, wanapewa sifa ya kupigiwa kura na wananchi katika uchaguzi wa serikali za mitaa," alisema Jafo.

Aidha, alifafanua kuwa

INAENDELEA UK. 8



Meneja Mazingira wa Kiwanda cha TBL cha Mwanza, John Lugongo (katikati), akiwaeleza wajumbe wa Bodi ya Maji ya Taifa, jitihada za kampuni za kulinda mazingira na matumizi mazuri ya maji walipofanya ziara kiwandani hapo mwishoni mwa wiki, wa kwanza kushoto ni Meneja wa kiwanda hicho, Patel Kiyovele. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 609,502 kufanya mtihani kidato 2 leo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MTIHANI wa upimaji wa kitaifa wa wanafunzi wa kidato cha pili unaanza kufanyika nchini kote leo mpaka Novemba 22, mwaka huu, ambapo wanafunzi 609,502 kutoka katika shule za sekondari 4,796 wanatarajiwa kushiriki.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mbeya jana, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani (Necta), DK. Charles Msonde, alisema kati ya watahiniwa hao wavulana wapo 288,925 sawa na asilimia 47.4 na wasichana 320,577 sawa na asilimia 52.6.

Vilevile, alisema watahiniwa wenye mahitaji maalumu ni 1,044 ambao 396 ni wenye uoni hafifu, 70 ni wasioona kabisa na 347 ni wenye ulemavu wa kusikia na 231 ni wenye ulemavu wa viungo mbalimbali vya mwili.

"Mwaka huu kumekuwa na ongezeko la watahiniwa 64,636 sawa na asilimia 11.86 ikilinganishwa na mwaka jana, ambapo tulikuwa na watahiniwa 544,866, tunatarajia mtihani huo kufanyika kwa kufuata kanuni na taratibu zote," alisema Dk. Msonde.

Alizitaka kamati za mitihani za mikoa na wilaya zote nchini kuhakikisha mitihani hiyo inafanyika kwa kuzingatia taratibu ili kuepuka udanganyifu ambao unaweza ukawagharimu wanafunzi kwa kufutiwa matokeo.

Darasa la nne

Aidha Dk. Msonde alisema wanafunzi 1,783,638 wanatarajiwa kufanya mtihani wa upimaji wa darasa la nne kuanzia Novemba 20 mpaka Novemba 22, mwaka huu na kwamba idadi hiyo ya wanafunzi ni kubwa kuliko miaka yote.

Alisema kati ya wanafunzi hao wavulana wako 901,786 sawa na asilimia 50.56 na wasichana ni 881,852 sawa na asilimia 49.44 na kwamba ongezeko la wanafunzi hao linatokana na ongezeko la hamasa ya wazazi kuwapeleka watoto wao shule baada ya serikali kuanza utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo.

Alisema watahiniwa wenye mahitaji

INAENDELEA UK. 8

## Ofisi ya Mtendaji yachomwa moto

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HALI ya taharuki imetanda katika Manispaa ya Moshi, baada ya watu wasiojulikana kuiteketeza kwa mafuta ya petroli, Ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Soweto pamoja na nyaraka zote za serikali zilizokuwa ndani ya ofisi hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alithibitisha jana kupokea taarifa za uhalifu huo, muda mfupi baada ya kuzuru eneo la Wailes, lilipo jengo hilo.

Katika taarifa yake, Mghwira ameagiza kufanyika uchunguzi wa kina ili kubaini wahusika wa tukio hilo, huku akisema ni mapema mno kulihusisha na masuala ya siasa. Watu hao wanadaiwa kuichoma moto ofisi hiyo, Novemba 9, mwaka huu, kati ya majira ya saa 1:30 na saa 2:30 usiku.

"Ni kweli mimi na kamati yangu ya ulinzi na usalama mkoa, nilipokea taarifa hizo jana usiku kwamba kuna watu wasiojulikana wamechoma Ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Soweto iliyoko eneo la Wailes, Manispaa ya Moshi na kuunguza nyaraka za serikali.

"Nimesha vielekeza vyombo vya ulinzi na usalama kuanza uchunguzi mara moja ili kubaini kiini cha uhalifu huo. Mpaka sasa kuna watu kadhaa wameshakamatwa na wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa ajili ya mahojiano."

Kwa mujibu wa Dk. Mghwira, tukio la kuteketezwa kwa ofisi hiyo liligunduliwa na mtu mmoja aishie jirani na ofisi hiyo, ambaye anadai kusikia harufu ya petroli na ya vitu vinavyochomwa moto.

"Jirani huyo alihisi kuna taka zinachomwa ndipo akaamua kuchungulia kupitia dirishani na kuona ofisi ya mtendaji ikiwa imeshika moto, hapo hapo, ndipo alipotoka nje na kupiga kelele, kitendo ambacho kilisababisha wananchi wenzake kutoka nje na kuuzima moto huo na kisha kufanikiwa kupunguza athari zilizoanza kujitokeza," alisema Mkuu huyo wa Mkoa.

Pia Dk. Mghwira alisema wahalifu hao baada ya kutekeleza nia hiyo ovu, waliacha katika eneo la tukio kibiriti na kipande cha msokoto wa bangi.

Alipoulizwa kama nyaraka zilizounguzwa ni zinazohusiana na masuala ya uchaguzi, Mkuu huyo wa Mkoa alisema nyaraka nyingi zilizoteketea ni za masuala ya afya.

Alizitaja baadhi ya nyaraka zilizokuwa karibu na dirisha ambalo lilianza kuteketea kwa moto kuwa zinazohusiana na zoezi la chanjo ya rubella, surua na polio, iliyofanyika hivi karibuni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Said Hamdan, akizungumzia tukio hilo, alisema jeshi hilo limepokea maelekezo ya Mkuu wa Mkoa na limeanza uchunguzi wa tukio hilo.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
06 – 11 - 2019

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **alhamisi tarehe 14 – 11 – 2019** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam kuelekea Mafinga,** gari hizo zenye namba za usajili:

| | |
|---|---|
| T 660 BZU / ZD 8121 | T 316 CZS / T 249 AGZ |
| T 628 DFA / ZD 8113 | T 210 BYM / T 146 CHN |
| T 641 DFA / T 137 CHN | T 324 CZS / T 777 AQR |
| T 245 BXH / T 380 DHQ | T 553 BKC / T 385 DHQ |
| T 645 DFA / T 377 DHQ | |

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | - | mita 33 |
| Upana | - | mita 4.70 |
| Kimo | - | mita 5.4 |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port hadi Mafinga Kupitia Iringa,** gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

215511102

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

HABARI KITAIFA

# 'Wahini vituo vya afya mnapoona dalili homa'

**Na Mwandishi Wetu,**
KIBAHA

WATANZANIA wametakiwa kuwahi vituo vya afya wanapoona dalili za homa ili wafanyiwe vipimo na kutibiwa mapema ugonjwa wa malaria.

Imeelezwa kuwa hatua hiyo itasaidia Tanzania kuepuka vifo vya maelfu ya watu vinavyotokea kila mwaka kwa maradhi yanayotibika, ikiwamo malaria inayoongoza kwa kuua nchini.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki mjini Kibaha, Mkoa wa Pwani na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, wakati Tanzania ilipoungana na nchi nyingine barani Afrika katika kuzindua kampeni ya 'Zero Malaria Inaanza na Mimi' ikiwa ni nchi ya 11 kujiunga na mpango huo maalumu wa kutokomeza malaria barani Afrika.

Waziri Ummy alisema kampeni hiyo inajikita katika juhudi za serikali kuzuia malaria na kuhakikisha huduma za matibabu zinafika pote nchini.

Naye Mtendaji Mkuu wa Mpango Maalum wa kutokomeza malaria, Roll Back Malaria (RBM) Partnership, Dk. Abdourahmane Diallo, alisema kwa kujiunga na kampeni hiyo, Tanzania itapiga hatua kubwa ili kutokomeza kabisa ugonjwa huo.

"Kupitia mpango huu jamii itafuatilia kwa karibu na kuwafanya viongozi wao wawajibike zaidi kutokomeza ugonjwa huu," alisema. Kampeni hiyo imezinduliwa katika kuadhimisha kumbukumbu ya Siku ya Malaria ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na mkutano wa mawaziri wa afya kutoka jumuiya hiyo unaofanyika jijini Dar es Salaam.

Kitaifa kampeni hiyo inalenga kupata msukumo wa kisiasa, kuongeza rasilimali kutoka vyanzo vya ndani pamoja na jamii ili kukabiliana kikamilifu na vita dhidi ya malaria.

"Mafanikio makubwa yamefikiwa barani Afrika, vifo vitokavyo na malaria vimepungua kwa asilimia 40 na matukio ya kuugua ugonjwa huu pia kushuka kwa asilimia 20 katika muongo mmoja," alisema.

Hata hivyo, Shirika la Afya Duniani (WHO), limesema katika ripoti yake ya hivi karibuni ilisema kuwa kumekuwa na ongezeko la ugonjwa wa malaria duniani.

Kampeni ya Zero Malaria Inaanza na Mimi, ina lengo la kuongeza kasi mchakato na juhudi za kutokomeza malaria barani Afrika na duniani kwa ujumla.

Tanzania inaungana na nchi za Ethiopia, Sierra Leone, Ghana, Eswatini, Niger, Uganda, Zambia, Senegal, Mauritania na Msumbiji kutokomeza malaria.

Pamoja na uzinduzi wa kampeni hii pia Tanzania imezindua mpango maalum (malaria scorecard) wenye lengo la kuongeza uwajibikaji katika kutokomeza malaria nchini. Pamoja na mkutano huu wa SADC pia washiriki walipata fursa ya kutembelea Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ambayo zaidi ya kuwa na mamlaka na wajibu wa kusambaza dawa nchini, pia imepata fursa ya kuhudumia nchi za jumuiya ya SADC.

## Spika azitaka PAC, PIC, LAAC kumpa ushirikiano CAG Kichere

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewaasa wajumbe wa kamati za usimamizi za Bunge, ikiwamo PIC, PAC na LAAC kuumpa ushirikiano wa kutosha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) aliyeteuliwa hivi karibuni, Charles Kichere.

Ndugai alisema hayo wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya Uwajibikaji na Uwazi katika Mikataba ya Manunuzi ya Umma kwa Kamati za Usimamizi za Bunge iliyoandaliwa na Taasisi ya Uwajibikaji wa Umma – WAJIBU, iliyofanyika Jumamosi.

Spika alitoa taarifa kwamba Kichere, anatarajia kujitambulisha rasmi katika Ofisi ya Bunge mjini Dodoma leo.

"Uteuzi huu umekuja kama ukurasa mpya wa uhusiano kwetu sisi na ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kichere ni mtu ninayemfahamu vizuri. Naamini ana nia njema na tutafanya naye kazi kwa weledi. Naombeni tumpokee na tumpe ushirikiano wa kutosha," Ndugai aliwaambia wajumbe hao.

Wakati huo huo, Spika Ndugai aliishukuru Taasisi ya Wajibu inayoongozwa na Mkurugenzi Mtendaji na CAG mstaafu, Ludovick Utouh, kwa kuandaa mafunzo hayo kwa wajumbe wa kamati za usimamizi za Bunge.

"Katika masuala kama mipango na uzalishaji, mchakato wa manunuzi hayakwepeki. Naamini kupitia mafunzo haya ya uwajibikaji na uwazi katika mikataba ya manunuzi ya umma, uelewa wa utaratibu wa manunuzi kwa wana kamati utaongezeka maradufu na kuwawezesha kusimamia vizuri sekta hii," alisema Ndugai.

Pia alipendekeza pia maboresho katika udhibiti

INAENDELEA UK. 8




# Maguful ateua wenyeviti wa bodi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amefanya uteuzi wa wenyeviti wa bodi nne za taasisi za serikali na mkuu wa chuo mmoja.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, walioteuliwa ni Mhandisi Emmanuel Korosso, kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), Dk. Alexander Kyaruzi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), Joseph Haule kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Barabara (Road Fund Board) na Dk. Felician Kilahama kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (Tafori).

Wenyeviti hao wa bodi wameteuliwa kushika nyadhifa hizo kwa kipindi cha pili baada ya kipindi cha kwanza kumalizika, na uteuzi wao umeanza Novemba 9, 2019.

Kadhalika Rais Magufuli amemteua Prof. Shadrack Mwakalila kuwa Mkuu wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (Mwalimu Nyerere Memorial Academy).

Prof. Mwakalila anashika wadhifa huo kwa kipindi cha pili na uteuzi wake umeanza Novemba 8, 2019.



Baadhi ya wasichana wanaolelewa katika kituo cha House of Hope cha Shirika la Hope for Girls and Women Tanzania mjini Mugumu Serengeti mkoani Mara, baada ya kukimbia vitendo vya ukeketaji nyumbani kwao, wakijifunza kusuka vikapu juzi ikiwa ni mojawapo ya mafunzo wanayopata kwa ajili ya kujiajiri hapo baadaye. **NA MPIGA PICHA WETU**

# Bunge kurekebisha sheria 11

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAKATI Bunge leo likihitimisha kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/21, pamoja na mambo mengineyo linatarajia kufanya marekebisho ya sheria 11.

Kwa mujibu wa ratiba ya Bunge, kesho wabunge wataanza kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali namba saba ya mwaka 2019, ambao unapendekeza kufanyika kwa marekebisho katika sheria hizo. Sheria hizo ni Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Sura ya 156, Sheria ya Ustawi wa Wanyama Sura ya 154, Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania Sura ya 197, Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura ya 134, Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa VVU na Ukimwi Sura ya 431.

Nyingine ni Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikeli za Viwandani na Majumbani Sura ya 182, Sheria ya Madini Sura ya 123, Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa Sura ya 419, Sheria ya Bandari Sura ya 166, Sheria ya Kuzuia Ugaidi Sura ya 19 na Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu Sura ya 36.

Mbali na kufanya marekebisho katika muswada huo, Bunge pia linatarajia kupitisha maazimio kadhaa likiwamo Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya Montreal kuhusu kupunguza uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya Hydrofluocarbons (HFCS) zinazomong'onyoa tabaka la 'ozone'.

Vilevile, Bunge linatarajia kujadili na pitisha azimio la kuridhia itifaki ya Jumuiya ya Nchi Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu usimamizi wa mazingira na maendeleo endelevu, pamoja na azimio la kuridhia itifaki ya marekebisho ya mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia.

Mhimili huo wa kutunga sheria pia utajadili na kupitisha azimio la kuridhia mkataba wa kimataifa wa Shirika la Chakula Duniani (FAO) wa kuzuia uvuvi haramu kupitia bandari za nchi wanachama, pamoja na azimio la kuridhia kuanzishwa kwa ushirikiano wa kimataifa wa nishati ya jua.

Azimio lingine linalotarajiwa kujadiliwa na kupitishwa ni azimio la kuridhia itifaki ya kinga na maslahi ya kidiplomasia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Pamoja na azimio la kuridhia Itifaki ya Afrika Mashariki ya mitandao ya teknolojia ya habari na mawasiliano.




# Serikali yasitisha uokoaji wachimbaji waliofukiwa Okt. 1

**Na Issa Mtuwa,** GEITA

MAJONZI na huzuni vimetawala kwenye mgodi wa wachimbaji wadogo wa Imalanguza, wilayani Geita baada ya usitishwaji wa shughuli za uokoaji wachimbaji wadogo waliofukiwa na kifusi mgodini tangu Oktoba mosi, mwaka huu.

Vilio hivyo vilitawala baada ya kuwasili Naibu Waziri wa Madini, Stanslausi Nyongo, mgodini hapo akiwa na viongozi wengine waandamizi wa wizara hiyo, mkoa na viongozi wa dini.

Wachimbaji waliofukiwa na kifusi wametambuliwa kuwa ni Calos Paulo mwenyeji wa Chato na Kulwa, Mahungija mwenyeji wa Busolwa Nyang'wale, ambao walifukiwa tangu Oktoba mosi, mwaka huu.

Usitishaji wa zoezi hilo ulitangazwa Novemba 9, ikiwa ni siku 39 tangu wachimbaji hao wafukiwe na kifusi kutokana na changamoto zilizojitokeza katika kipindi chote cha uokoaji.

Ripoti maalum ya timu ya wataalamu wa

INAENDELEA UK. 8

# MAFANIKIO YA NSSF NA MIAKA MINNE YA KISHINDO CHA RAIS DK. JOHN MAGUFULI

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) linampongeza Rais Dk. John Magufuli katika uongozi wake kwa kipindi cha miaka minne tangu aingie madarakani, Novemba 2015.

Mambo mengi makubwa ya maendeleo aliyoyafanya kwa Taifa la Tanzania ambayo ni pamoja na ununuzi wa ndege kumi na moja (11) na kulifufua Shirika la Ndege la Tanzania, ujenzi wa reli ya kisasa (Standard gauge), ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme katika Bonde la Mto Rufiji (Stigglers Gorge), ujenzi wa barabara nyingi nchini zinazounganisha maeneo yote ya nchi, ujenzi wa hospitali, vituo vya afya, shule za msingi na sekondari, uboreshaji wa huduma za afya kwa kuongeza bajeti ya dawa na vifaa tiba, pia ameboresha sekta ya hifadhi ya jamii nchini.

Uboreshaji wa sekta ya hifadhi ya jamii nchini umeenda sambamba na marekebisho ya Sheria ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwenye sura ya 50 ya mwaka 2018 ambapo sasa NSSF inatoa huduma ya hifadhi ya jamii kwa wafanyakazi walio katika sekta binafsi na sekta isiyo rasmi. Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), William Erio, amesema kwa mujibu wa Sheria ya NSSF, Shirika linatekeleza majukumu makuu manne ambayo ni kuandikisha wanachama, kukusanya michango, kuwekeza na kulipa mafao.

Katika kutekeleza majukumu ya Shirika, Erio amesema kuwa serikali ya awamu ya tano imedhamiria kuboresha maisha ya Watanzania hivyo kupitia mabadiliko ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii sura ya 50 ya mwaka 2018, NSSF imewafikia na kuwaandikisha wanachama kutoka sekta binafsi. Kwa mujibu wa sheria waajiri wote nchini kutoka sekta binafsi wanatakiwa kuandikisha wafanyakazi wao kwenye Shirika la NSSF.

Katika kipindi cha miaka minne, Rais Dk. John Magufuli amewasaidia wananchi waliojiajiri wenyewe ambao wengi wao ni wakulima na wajasiriamali; Kwanza kwa kuwapunguzia mzigo wa kodi na ushuru; Pili amewawezesha wajasiriamali kufanya biashara zao bila kubugudhiwa na kuwakabidhi vitambulisho ikiwa ni utambulisho wa kufanya biashara sehemu yoyote na mkakati huo unawajengea uwezo wakupata faida kwenye biashara zao na kuwawezesha kujiandikisha na NSSF ili kujiwekea akiba kwa ajili ya uzee, ulemavu, vifo, maradhi na majanga mengine ambayo yatasababisha kundi hilo la Watanzania kushindwa kufanya shughuli zao na hatimaye kukosa kipato cha kuendesha maisha yao na familia zao.

Jukumu la pili la NSSF ni kukusanya michango. NSSF imeboresha njia ya ukusanyaji michango kutoka kwenye utaratibu wa kupokea hundi na pesa taslimu hadi kujiunga na mfumo wa malipo wa serikali kielektroniki (GePG).

Anasema mfumo huo umeleta tija kwenye ukusanyaji michango ya wanachama. Katika kipindi cha mwaka mmoja 2018/19 kiasi cha Sh. bilioni 828.1 kilikusanywa.

Kwa mujibu wa Erio, mfumo wa GePG umeendelea kuwa na matokeo chanya kwa NSSF. Awali makusanyo yalikuwa Sh. bilioni 60 kwa mwezi, kwa sasa yameongezeka na kufikia kiasi cha Sh. bilioni 96.1 kwa mwezi.

Mkurugenzi Erio, anasema NSSF inaendelea kuboresha uwekezaji na sasa shirika linawekeza zaidi kwenye dhamana za serikali.

"Tumeongeza kiasi cha kuwekeza kwenye dhamana za serikali kutoka asilimia nane iliyokuwapo mwezi Agosti 2018 hadi kufikia asilimia 20, tarehe 30 Juni, 2019. Hivyo basi hadi kufikia Agosti 2019, NSSF iliwekeza jumla Sh. bilioni 733.8 kutoka Sh. bilioni 340.5 zilizokuwa zimewekezwa mwezi Juni 2018". Katika kipindi cha mwaka mmoja ulioishia mwezi Juni 2019, Shirika liliendelea kuhakikisha kuwa linaboresha mapato yatokanayo na uwekezaji. Mfano mmoja ni eneo moja la mradi wa Daraja la Mwalimu Nyerere, Kigamboni ambako makusanyo yake yameongezeka toka wastani wa Sh. milioni 697.4 kwa mwezi Agosti 2018 hadi kufikia Sh. bilioni 1.08 kwa mwezi mmoja wa Julai 2019 hili ni ongezeko la zaidi ya asilimia 54 katika kipindi cha mwaka mmoja.

Kwa kuwa serikali ya awamu ya tano imedhamiria kufikia uchumi wa kati kupitia viwanda, NSSF imeendelea kuwekeza katika viwanda mbalimbali kama vile kukiwezesha kiwanda cha viua wadudu, Kibaha kwa kuwakopesha mtaji, pia Shirika limetoa mkopo kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ili waweze kufufua kiwanda cha unga wa mahindi na kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti kilichopo jijini Dodoma. Shirika limeendelea na ulimaji wa mashamba ya miwa na hatua za awali za ujenzi wa kiwanda cha sukari katika eneo la Mbigiri, mkoani Morogoro zinaendelea. Hii yote ni katika kuunga mkono juhudi za Serikali ya awamu ya tano katika kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025 kupitia ujenzi wa viwanda.

Katika kuunga mkono juhudi za Rais za kuwaletea maendeleo Watanzania na kutatua kero zao nyingi kwa kuboresha mifumo yao ya malipo na hasa kuwawezesha wastaafu kupokea mafao yao moja kwa moja kupitia akaunti zao za benki badala ya kwenda kupanga misululu katika ofisi za NSSF. Anasema uboreshaji wa mifumo umesaidia kupunguza malalamiko kwa wanachama wao kwenye ucheleweshaji wa malipo yao baada ya kuanza matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ulipaji wa mafao ambayo kwa ujumla wake imerahisisha malipo ya wanachama.





Bodi ya Wadhamini, Menejimenti na Watumishi wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) tunatoa Pongezi za dhati kwa
**Mh.Dkt John Pombe Magufuli,**
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
kwa uthubutu na uongozi wake uliotukuka.

Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii
Benjamin Mkapa Pension Tower
Mtaa wa Azikiwe
S.L.P 1322, Dar es Salaam,
Tanzania

Simu : 0800 756 773
Faksi : +255 22 2163400 - 19
Tovuti: www.nssf.or.tz

Tunajenga Maisha yako ya sasa na baadae
**NSSF KWANZA**
Jiunge Nasi.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mungu ibariki Stars kuelekea Afcon 2021

**KWA** mara nyingine tena, Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kushuka dimbani Ijumaa kuwakabili wapinzani wao kutoka Equatorial Guinea.

Stars itawakaribisha wageni hao Ijumaa, kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam, ikiwa ni mechi ya kwanza ya kuanza safari ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2021).

Kikosi hicho kinachonolewa na Kocha Mrundi Etienne Ndayiragije anayeshirikiana na Juma Mgunda kutoka Coastal Union na Selemani Matola wa Polisi Tanzania, kinaanza kampeni hiyo mpya kikiwa tayari kimepata tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Stars inaingia kuanza kampeni hiyo pia ikiwa na kumbukumbu ya kucheza fainali zilizopita na Afcon, zilizofanyika Juni mwaka huu nchini Misri, ikiwa ni baada ya kuikosa michuano hiyo kwa miaka 39.

Katika kuhakikisha kuwa Stars inaendelea kufanya vema katika mashindano mbalimbali inayoshiriki, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limejaribu kuipa maandalizi ya kiwango cha juu, yanayofanana na hadhi ya timu hiyo ambayo inapeperusha bendera ya nchi. Tunawakumbusha kuwa, kilichotokea hadi Stars itapata tiketi ya kushiriki fainali zilizopita na kufuzu CHAN kwa mara ya pili, kinatakiwa kifanyike mara mbili au tatu, ili timu hiyo iweze kupata matokeo mazuri katika mechi zake.

Wachezaji wote walioitwa katika kikosi hicho, wanatakiwa kuweka uzalendo mbele, kwa kujituma na kupambana ili wapate matokeo chanya ambayo yataipeleka timu hiyo Cameroon na kuwa moja ya timu zitakazowania ubingwa wa Afrika.

Hakuna kisichowezekana, nguvu na juhudi zilizowapeleka Afcon Misri, zinatakiwa ziongezeke ili isionekane Tanzania ilibahatisha kushiriki mashindano hayo ya juu hapa barani Afrika.

Wachezaji wasifikiri kutangaza jina la Tanzania, wanatakiwa wafikirie mashindano hayo, ni daraja lao la kuelekea kwenye mafanikio, kwa sababu mawakala kutoka nchi mbalimbali hufika kutazama vipaji, na kwa maana hiyo, nyota watakaofanya vema watakuwa wamejitengenea soko.

Kila mchezaji ana ndoto zake, na ndoto kubwa ni kwenda kucheza Ulaya au kupata klabu ya kuitumikia iliyoko nje ya Tanzania ambayo tunaamini, itamlipa mchezaji huyo mshahara na posho bora zaidi ya kile alichokuwa analipwa hapa nyumbani.

Lakini njia za kufika huko ni tofauti, wengine wanapata fursa kupitia klabu zao zinaposhiriki mashindano ya kimataifa, au kupitia kufanya vema wakiwa na timu za Taifa, daraja ambalo huwa na thamani zaidi.

Nipashe inaamini kuwa, kama wachezaji kutoka Afrika Magharibi au Afrika ya Kati, wamepata nafasi ya kusajiliwa na timu za Ulaya, huu ni wakati mwingine wa wachezaji wa Stars kujituma kuisaidia timu yao, lakini vile vile ni njia ya kujitengenezea ulaji binafsi.

Tunaamini kufanya vema kwa Stars katika mashindano haya, kutasaidia nchi kuwa wachezaji wengi zaidi wanaocheza soka la kulipwa na baadaye kuungana na nahodha Mbwana Samatta kuibeba Tanzania.


Na katika kuhakikisha malengo haya yanafanikiwa, wadau wanatakiwa kuwa bega kwa bega na TFF, kwa kusaidia maandalizi kwa sababu kwa kutegemea fedha kutoka kwa mdhamini mkuu wa timu hiyo pekee, hazitoshi.

Pia tunawakumbusha washangiliaji kujitokeza kwa wingi Ijumaa kuishangilia timu hiyo ili iweze kuanza vema kampeni hiyo hapa nyumbani na baadaye kuelekea Libya ikiwa na ari na morali nzuri ya kupambana.

Kila la kheri Taifa Stars, kila la kheri Watanzania kuelekea Cameroon Afcon 2021.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

## Iliyoifunga Ndanda ni Yanga ya Zahera

**WATANZANIA** wengi wanapenda mchezo wa soka. Halafu wanapenda sana klabu za Simba na Yanga. Kupenda kwao klabu hizo, wakati mwingine kunawafanya hadi baadhi yao wanashindwa kupambanua mambo.

Kuna mwanamuziki mmoja aliwahi kuimba kuwa kupenda ni upofu. Na kweli, kwa sababu nimeona baada ya Yanga kushinda bao 1-0 Ijumaa iliyopita dhidi ya Ndanda, wanachama na mashabiki wa timu hiyo wameonekana kufurahi na kuzidi kumponda kocha wao aliyepita, Mwinyi Zahera kuwa si kocha mzuri.

Zahera huyu huyu ambaye baadhi ya wanachama walimpa uchifu, akaongoza zoezi la kuchangisha fedha, akapewa ili asajili, watu wakavaa "vipensi" kutoka majumbani kwao kwenda navyo uwanjani kwa sababu tu ya kumuunga mkono baada ya kufungiwa na Bodi ya Ligi kwa kukiuka kanuni za aina za uvaaji wa makocha.

Leo ameonekana hafai kwa sababu tu Yanga imetolewa kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho kwa kufungwa na Pyramids ya Misri.

Ukiuliza jinsi Yanga ilivyo, kama kweli wengi walitarajia kuwa ingeweza kuifunga Pyramids, mashabiki wanajibu kuwa hata kwenye Ligi Kuu timu yao imekuwa ikipata ushindi wa kusuasua.

Ukiuliza ushindi wa kusuasua upi, unajibiwa wa goli moja tu, tena yanapatikana kwa faulo, penalti au kona.

Baada ya mechi dhidi ya Ndanda FC, wanachama na mashabiki wameonekana kufurahi na kusema eti ile ndiyo Yanga waliokuwa wanaitaka.

Wanaanza kumsifia kocha, Boniface Mkwasa, kuwa ameibadilisha kidogo timu. Cha kujiuliza Mkwasa hana hata wiki kwenye kikosi, ni nini ambacho amekibadilisha?

Nilipoiangalia Yanga kwenye mechi dhidi ya Ndanda FC ni kwamba hakuna kilichobadilika.

> **Katika mechi nne za ligi ambazo Zahera ameiongoza Yanga ni kwamba imefungwa mechi moja, sare moja na kushinda mechi mbili tena kwa bao 1-0 dhidi ya Mbao FC na Coastal Union.**

Wachezaji ni wale wale waliokuwa wakicheza chini ya Zahera na hata aina ya matokeo ni yale yale.

Katika mechi nne za ligi ambazo Zahera ameiongoza Yanga ni kwamba imefungwa mechi moja, sare moja na kushinda mechi mbili tena kwa bao 1-0 dhidi ya Mbao FC na Coastal Union.

Kwenye mechi dhidi ya Ndanda, Yanga imeshinda tena bao 1-0, ambalo nalo pia limepatikana kwa nje ya faulo kama ilivyokuwa chini ya Zahera.

Ninachowataka wanachama na mashabiki wa Yanga ni kwamba wawe wavumilivu na wasiwe wepesi wa "kujaji" kocha aliyekuwapo na aliyeondoka kwa kipindi kifupi, tena mechi moja tu.

Wanachotakiwa ni kumpa nafasi Mkwasa na pia kocha mpya atayekuja ili atengeneze mfumo wake mpya na si kuanza kuwapa presha au kufananisha ubora wa kocha aliyepita na aliyekuwapo.

Kuanza kusifia sana au kuponda, wakati timu haijakaa sawa, itakapokuja kupata matokeo tofauti, wengine wataanza kumkumbuka kocha aliyepita na hapo tatizo litakuwa halijatatuliwa zaidi ya kuanza upya.

Bado inaonekana Mkwasa anatafuta pa kuanzia, hivyo kwenye mechi ijayo ikitokea bahati mbaya ikikosa ushindi wasiaze tena maneno, kwani inaonekana inaendelea kucheza vile vile kama ilivyokuwa chini ya Zahera na kama si goli la faulo, mechi ingeenda sare na kwa Wabongo navyowajua wangeanza minong'ono.

Yanga wamuache kwanza kocha afanye kazi yake kwenye kipindi hiki cha mpito, hadi atakapomkabidhi mwenzake kijiti.

Kutaka kuwafananisha au kuwashindanisha kwa kipindi hiki kifupi ni kutaka kuendeleza tatizo lile lile lililopo.

# Jinsi hoja nne zilivyotikisa Bunge

ZIKIWA zimepita siku saba tu kati ya 11 za mkutano wa 17 wa Bunge la 11, takribani mambo manne yametikisa ikiwa ni pamoja na suala la uchaguzi wa serikali za mitaa kuwa moto, hali iliyosababisha wabunge wa upinzani kukwaruzana na mawaziri.

Hoja hiyo iliwalazimu Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara kutoa kauli kali ndani ya mhimili huo wa kutunga sheria.

Mkutano huo ulioanza Novemba 5 kwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango kuwasilisha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/21 pia ulitawaliwa na hoja ya wahudumu wa ndege katika Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) kutokuwa na mvuto.

Pia, hoja ya watoto wasiowahudumia wazazi wao kushtakiwa, pamoja na kuongezeka kwa deni la taifa ilijadiliwa kwa mapana zaidi. Uchaguzi Serikali za Mitaa katika siku tano za mkutano huo, hoja iliyochangiwa na wabunge wengi zaidi ni ile ya serikali za mitaa, wakihoji namna wasimamizi wa uchaguzi huo walivyowaengua wagombea pasipo kufuata utaratibu.

Mbunge wa Singida Kaskazini, Justine Monko (CCM), ndiye aliyeanzisha mjadala huo siku moja baada ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kutangaza kujitoa katika uchaguzi huo.

Kwenye swali alilouliza, Monko alihoji: Chadema wametangaza kujitoa katika uchaguzi na kuwakosesha wananchi haki yao ya mshingi, je, serikali ina kauli gani kutokana na kadhia hii?" Naye Mbunge wa Tarime Vijijini (Chadema), John Heche, aliwatuhumu wakurugenzi wa halmashauri na wakuu wa wilaya kuwa walikuwa wakikutana na wasimamizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa na kuwafundisha namna ya kughushi matokeo ya uchaguzi huo, akitolea mfano wa Wilaya ya Tarime mkoani Mara, Mkurugenzi wa Halmashauri alikutana na wasimamizi wa uchaguzi katika Chuo cha Ualimu baada ya kazi ya kupokea fomu kumalizika, kuanza kuwafundisha namna ya kughushi matokeo.

Makamu Mwenyekiti wa Cuf, Bara, Maftah Nachuma alieleza kuwa endapo mapungufu yaliyojitokeza katika uchaguzi huo yasiporekebishwa wataenda mahakamani kumfungulia kesi Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo pamoja na wasimamizi wa uchaguzi huo.

Hoja za wabunge hao ilimlazimu Naibu Waziri wa Tamisemi, Waitara kutolea ufafanuzi na kueleza kuwa uchaguzi huo upo pale pale na utafanyika siku iliyopangwa.

Alisema vyombo vya ulinzi na usalama vimejipanga katika kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika katika hali ya amani na utulivu, huku ikiwaonya watu waliojipanga kufanya vurugu siku ya uchaguzi.

Hoja hiyo ilimlazimu Waziri Lugola kusimama na kutolea ufafanuzi zaidi na kueleza kuwa Jeshi la Polisi limejipanga wakati wote wa kampeni hadi uchaguzi kuimarisha ulinzi na asalama katika maeneo yote nchini.

Alisema Jeshi la Polisi halitatoa mwanya kwa mtu yoyote atakayejaribu kuvunja amani ama kufanya vitendo vinavyoweza kuashiria kuvunjika kwa amani na kwamba alishamwagiza Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP),

Simon Sirro, aanze kuchukua hatua kwa wahusika waliofyeka shamba la msimamizi wa uchaguzi wilayani Mbozi.

**WAHUDUMU ATCL**

Mbunge wa Kigoma Kusini (CCM), Husna Mwilima, alizua tafrani ndani ya bunge baada ya kulitaka shirika hilo kuajiri wahudumu wenye mvuto.

Wakati akichangia, Mwilima alisema wahuduma wa shirika hilo hawana mvuto, wafupi, hali inayosababisha ndege kutokuwa na mvuto zaidi.

"Wahudumu wetu kwenye shirika letu la ndege utakuta 'Air hostess' mfupi, hana mvuto, mhudumu nyuma yupo kawaida, hata mimi na miaka yangu ni 50 nimeshazeeka nilivyo ninavutia, tunapoajiri ma-Air hostess akiwa ndani ya ndege ukimuita akigeuka abiria anaona kweli," alisema Mwilima.

Hoja hiyo, ilimlazimu Naibu Waziri wa Ujenzi, anayeshughulikia sekta ya Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye kuitisha mkutano na waandishi wa habari na kueleza kuwa serikali haitumii kigezo cha mvuto katika kuajiri watumishi wa ATCL.

**WATOTO WASIOWAHUDUMIA WAZAZI**


MBUNGE wa Kahama Mjini (CCM), Jumanne Kishimba, alizua mjadala baada ya kutoa hoja ya kuitaka serikali kuleta muswada wa sheria bungeni utakaowabana watoto wanaokaidi kuwatumia fedha za matumizi wazazi wao.

Mbunge huyo alisema sheria hiyo itamsaidia mzazi aliyemsomesha mtoto wake hadi akapata mafanikio kuweza kusaidiwa gharama za matumizi, kwani hivi sasa watoto wengi wamewatelekeleza wazazi wao.

"Leo hii mzazi usipompeleka mtoto shule unashtakiwa, lakini mtoto asipomtumia pesa mzazi hawezi kushtakiwa. Tunaomba Wizara ya Elimu, Ustawi wa Jamii watuletee sheria ili mtoto asipomtimizia mahitaji mzazi wake ashtakiwe," alisema Kishimba.

Suala la kuongezeka kwa deni la taifa kutoka Sh. trilioni 49 Agosti mwaka jana hadi Sh. trilioni 52 pia liliibuka ambapo baadhi ya wabunge waliitaka serikali kuhakikisha thamani ya shilingi haiporomoki ili kuthibiti kuongezeka kwa deni hilo.

Mbunge wa Maswa Magharibi (CCM), Mashimba Ndaki, aliitaka serikali kuhakikisha thamani ya shilingi inaendelea kuwa imara kwani ikitikisika deni hilo litazidi kuongezeka. Alisema kwenye mpango serikali ihakikishe thamani ya shilingi inaimarikia, inakuwa imara dhidi ya dola na kwamba fedha ya mataifa ya kigeni ikiimarika, shilingi yetu ikitikisika deni hilo litaongezeka.




Habari na Gwamaka Alipipi, DODOMA

**MWALIMU JULIUS K. NYERERE UNIVERSITY OF AGRICULTURE AND TECHNOLOGY (MJNUAT)**

**Invitation for tender**

**Tender no: PA/132/2019-2020/G/06(1&2)**

**Supply of Office Furniture and Office Equipment**

1. This Invitation for Tenders follows the General Procurement Notice for this Project, which appeared in www.taneps.go.tz. Dated 24 October 2019.

2. The Government of Tanzania has set aside funds for the operation of the MJNUAT during the financial year 2019/2020. It is intended that part of the proceeds of the funds will be used to cover eligible payment under the contract for the Supply of Office Furniture and Office Equipment.

3. The Mwalimu Julius K. Nyerere University of Agriculture and Technology now invites sealed tenders from eligible national Suppliers for Supply of Office Furniture and Office Equipment.

4. Bidding will be conducted through National Competitive Tendering procedures specified in the Public Procurement (Goods, Works, Non-Consultant Service and Disposal of Public Assets by Tender) Regulations, 2013 –Government Notice No. 446 as amended in 2016.

5. Interested eligible Tenders may obtain further information from the Secretary of Tender Board, Mwalimu Julius K. Nyerere University of Agriculture and Technology (MJNUAT), Oswald Mang'ombe Campus, P.O. Box 976, Musoma, Mara (Headquarter-Butiama), Tanzania. Mobile No. +255 767 957 772/ 620 863 762 from 07:30 to 15:00 on Monday to Friday inclusive except on public holidays.

6. A complete set of Tendering Document(s) in English Language and additional sets may be purchased by interested Tenderers upon payment of a non-refundable fee of TZS 150,000/=. Payment should be by either Cash, Banker's Draft, or Banker's Cheque, payable to the Vice Chancellor (MJNUAT). (Please contact us via above mobile number to obtain Control Number)

7. Bids must be collected from the above-mentioned office address from 11th November 2019 and returning the books will be on 02nd December 2019 from 07:30 to 15:00.

8. Bids will be opened in the presence of Bidders' Representatives, who choose to attend at the address indicated above on 03rd December 2019 at 10:00 am.

9. Cost of Bid; The Bidder shall bear all costs associated with the preparation and submission of the bid and the procuring entity will in no case be responsible or liable for those costs, regardless of the conduct or outcome of the solicitation.

Other information related to this bid shall be available and obtained in the tender documents.

**Vice Chancellor**
**MJNUAT**

215508902



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh, na baadhi ya wajumbe wa kamati za usimamizi za Bunge, PIC, PAC na LAAC wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya uwajibikaji na uwazi katika mikataba ya manunuzi ya umma yaliyofanyika Jumamosi mkoani Dodoma. **MPIGAPICHA WETU**

# Waliotenguliwa sasa kushiriki uchaguzi mitaa

**INATOKA UK. 2**

vyama vya siasa ndiyo vilivyojitoa katika uchaguzi huo na siyo wagombea.

Hata hivyo, hakutoa ufafanuzi kutokana na sheria ya sasa nchini kitoruhusu wagombea binafsi.

Sheria ya sasa ya uchaguzi inaelekeza wagombea wote wa nafasi za uongozi wa kisiasa kupitia vyama vya siasa.

"Hapa hakuna mtu kukimbia kwenye 'cage' (ulingo), hakuna mtu kuweka mpira kwapani, wote waliochukua fomu na kurejesha fomu wataenda kushiriki uchaguzi Novemba 24, mwaka huu, kama wamezoea kukimbia safari hii hakuna kukimbia," alisema Jafo.

Kwa mujibu wa Jafo, katika uchaguzi wa serikali za mitaa wagombea waliojitokeza na kuchukua fomu walikuwa 550,036 na waliorejesha fomu walikuwa ni 539,953 sawa na asilimia 97.29.

Waziri huyo alisema hadi mchakato wa maamuzi ya rufani mbalimbali lilipohitimishwa Novemba 9, jumla ya rufani 4,921 sawa na asilimia 32 zilipitishwa na zilizobaki zilikosa sifa kwa sababu mbalimbali.

Alisema katika mchakato wa kuchukua na kurejesha fomu, CCM imefanikiwa kupita bila kupingwa katika maeneo mbalimbali kwa kuwa hapakuwa na mgombea yeyote kutoka chama cha upinzani.

Alisema kwenye nafasi za wenyeviti wa vijiji CCM imepita bila kupingwa katika vijiji 6,248 kati ya vijiji 12,319 sawa na asilimia 51, na katika mitaa CCM pia imepita bila kupingwa katika mitaa 1,169 kati ya mitaa 4,263 sawa na asilimia 27.

Kwa mujibu wa Jafo, vitongoji, CCM kimepita bila kupingwa kwenye vitongoji 37,505 kati ya vitongoji 64,384 sawa na asilimia 58, na kwa upande wa wajumbe wa kundi la wanawake jumla ya wajumbe 64,085 wamepita bila kupingwa, wajumbe kundi mchanganyiko jumla ya wajumbe 75, 560 wamepita bila kupingwa.

Kuhusu vyama kujitoa, Waziri Jafo alisema ni demokrasia ya vyama vya siasa kujitoa kwenye uchaguzi, pia ni uhuru wao wala hawalazimishwi kufanya jambo ambalo hawako tayari kulifanya.

**INAENDELEA UK. 26**

# 609,502 kufanya mtihani kidato 2 leo

**INATOKA UK. 2**

maalumu wapo 3,978 ambao kati yao 735 ni wenye uoni hafifu, 102 ni wasioona, 887 ni wenye ulemavu wa kusikia na 2,254 ni wenye ulemavu wa viungo mblimbali vya mwili.

Dk. Msonde alisema mwaka huu kuna ongezeko la wanafunzi 625,139 sawa na asilimia 53.96 ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi waliofanya mtihani huo mwaka 2018 ambao walikuwa 1,158,499.

"Kwa jinsi takwimu zilivyo ni kwamba idadi ya wavulana watakaofanya mtihani wa upimaji wa darasa la nne ni sawa na idadi ya wanafunzi wote waliofanya mtihani wa taifa wa darasa la saba, hii yote ni kutokana mafanikio ya elimu bila malipo kwa ngazi ya elimu msingi," alisema Dk. Msonde.

Alisema mtihani huo ni muhimu kwa kuwa unasaidia kujua kiwango cha wanafunzi wanaomudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu na kwamba matokeo ya upimaji huo yanabainisha maeneo muhimu yanayohitaji kufanyiwa maboresho katika vitendo vya ujifunzaji wa wanafunzi.

**KIDATO CHA NNE**

Kuhusu mitihani ya kidato cha nne inayoendelea, Dk. Msonde alisema wanafunzi wamefanya mitihani ya masomo 17 yakiwamo masomo saba ya lazima, na kwamba yote yaliyobaki ni ya hiari.

Alisema tangu mitihani hiyo ilipoanza mpaka sasa hakuna udanganyifu uliobainika nchini kote, na kwamba hali hiyo imekuwa tofauti na miaka mingine ambayo udanganyifu huo ulikuwa unafanyika.

Alisema kamati za uendeshaji wa mitihani katika ngazi za mikoa na wilaya zimefanya kazi kubwa ya kuwaelimisha wasimamizi pamoja na wanafunzi ili wajuwe madhara ya kufanya udanganyifu hali ambayo imeleta mafanikio.

Dk. Msonde alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo kamati zake za uendeshaji wa mitihani zinafanya kazi nzuri katika kuwaelimisha wasimamizi na wanafunzi, hivyo kuleta matokeo chanya.

# Serikali yasitisha uokoaji wachimbaji waliofukiwa Okt. 1

**INATOKA UK. 4**

uokoaji imeeleza kuwa kumekuwa na changamoto nyingi wakati wa uokoaji zilizosababisha kuwa na ugumu wa kuwaokoa wachimbaji hao.

Akiwasilisha taarifa ya wataalamu wa uokoaji iliyoishauri serikali kusitisha kwa zoezi hilo, Mkuu wa Wilaya ya Geita, Josephat Maganga, amemwambia Naibu Waziri wa Madini kuwa miongoni mwa changamoto zilizojitokeza wakati wa uokoaji ni pamoja na uwapo wa maji chini ya mgodi, mwingiliano wa magogo chini ya shimo la mgodi, na kutokuwa na usalama katika eneo hilo hata kwa vyombo vya uokoaji.

Maganga aliongeza kuwa, kulikuwa na wataalamu wa makundi mbalimbali ya uokoaji na vifaa vya kutosha kutoka kwa Jeshi na Uokoaji, mgodi wa dhahabu wa Geita (GGM), na kampuni nyingine kutoka kwenye migodi mbalimbali, lakini pamoja na juhudi zote imeshindikana kupatikana kwao.

Taarifa hiyo iliendelea kusema kuwa siku ya tukio hilo, kwenye shimo hilo kulikuwa na wachimbaji 5, ambapo 3 kati yao waliokolewa siku hiyo hiyo na wawili hawakuweza kupatikana hadi zoezi hilo la uokoaji linasitishwa.

Naibu Waziri Nyongo, alisema serikali imesikitishwa na tukio hilo na kwamba iko pamoja wafiwa na wachimbaji wote.

Alisema, serikali inathamini uhai wa mtu mmoja kuliko dhahabu au madini yote yaliko chini na ndio maana inasisitiza wachimbaji kuchimba kwa kufuata utaratibu na sheria ili wachimbe kwa kuzingatia usalama kuepukana na majanga kama hayo.

# Spika azitaka PAC, PIC, LAAC kumpa ushirikiano CAG Kichere

**INATOKA UK. 3**

na ukaguzi wa mahesabu ya serikali, akisisitizia suala la upokeaji wa taarifa kwa muda muafaka na kuongeza nguvu katika upande wa udhibiti.

"Bunge linatakiwa kujishughulisha na masuala kwa wakati huo huo yakiwa bado moto moto. Hivyo, tunatakiwa kuangalia namna ambavyo tunaweza kufikia mduara wa matumizi ya umma ili tusipitwe," alisema.

Kwa upande mwingine, Ndugai alisema kwamba ofisi ya CAG na Bunge limeweza kwa kiasi kikubwa kufanikiwa katika upande wa ukaguzi ila upande wa udhibiti unapelea.

"Katika mfumo wetu, kipengele cha udhibiti haujakaa sawa sawa, na ili tuweze kwenda huko lazima yajengeke mazingira ya kikatiba itakayo ruhusu ofisi zetu hizi kufanya hivyo," aliongeza Spika huyo.

"Hata hivyo mabadiliko ya aina haya yanaweza yakaanza polepole, ili sote tuweze kufikia malengo kwa pamoja," alisisitiza Ndugai.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, alisema mafunzo hayo yana manufaa makubwa kwa kamati za usimamizi wa Bunge kwa sababu yanawawezesha wabunge husika kufahamu wajibu wao katika kuisimamia vizuri serikali.

"Kama mnavyofahamu, mabadiliko ya wajumbe katika kamati hizi yanayotokea kila baada ya miaka miwili na nusu. Hivyo, mafunzo kama haya yanasaidia wajumbe wapya kupata uzoefu na maarifa katika eneo hili la usimamizi wa Bunge kwa serikali," alisema Kaboyoka.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa WAJIBU, Utouh, alisema baadhi ya mada zilizowasilishwa katika mafunzo hayo ni uwazi na uawajibikaji kwenye sheria ya manunuzi ya 2011, dhana ya mikataba ya manunuzi ya wazi, ripoti ya wajibikaji ya viashiria vya rushwa katika sekta ya umma na mbinu za medani katika kuendesha mahojiano katika manunuzi ya sekta ya umma.

Katika mafunzo haya, mawasilisho ya mada yalifanywa na Taasisi ya WAJIBU ikishirikiana na mashirika ya kiserikali kama PPRA na PSPTB, na shirika lisilo la kiserikali la HIVOS. Jumla ya wanakamati 72 walihudhuria.

HABARI KITAIFA



Ofisa Uvuvi na Mifugo wa Manispaa ya Morogoro, Mohamed Chamzhim (kushoto), aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Morogoro katika uzinduzi wa Klabu ya Biashara ya Benki ya NBC mkoani Morogoro, akishikana mikono na Mjumbe wa Bodi ya NBC, Dk. Kassimu Hussein, wakati akizindua rasmi klabu hiyo mkoani humo jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Biashara wa benki hiyo, Elvis Ndunguru. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watanzania wameonyesha nia ya kuwekeza Angola

**Na Felix Andrew**

BALOZI mpya wa Angola nchini, Sandro de Oliveira, amesema kuna kampuni kadhaa za kitanzania ambazo zimeonyesha nia ya kuwekeza nchi humo na kuahidi kutoa msaada unaohitajika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki,wakati akielezea maadhimisho ya uhuru wa nchi hiyo, balozi huyo hakuzitaja kampuni hizo, lakini alisema kuwa zipo tano ambazo zipo tayari kuwekeza nchini Angola.

Angola ilipata uhuru wake mwaka 1975, kutoka mikononi mwa Wareno, na baadaye umeleta amani, mwanga na matumaini mapya.

Alidokeza kuwa kuna kampuni mbili za kutoka nchini Angola zitafungua biashara hapa Tanzania muda mfupi ujao.

Alipoulizwa kuhusu takwimu za wafanyabiashara wa nchi mbili hizo, alisema kuwa kwa sasa suala hilo bado wanalifanyia marekebisho.

"Kwa sasa tunakusanya upya taarifa na kuanzisha jukwaa la ushirikiano na sekta binafsi kwani mfumo wa sasa bado haujafanya vizuri." Alisema uongozi wa sasa wa Angola umefanya jitihada kubwa sana kuboresha mazingira ya biashara kwa kutunga sera rafiki na vivutio vingi sana.

"Hiyo pia ninaweza kusema na hapa Tanzania, hatua kadhaa tunaona zinachukuliwa na serikali kuhakikisha kunakuwa na mtiririko mzuri wa kiuwekezaji." alisema.

Kwa upande wa uchumi, alisema Angola imeweza kutumia rasilimali zake kwa ajili ya kuwaendeleza wananchi wake na maisha yao.

"Ni kweli kuwa hali ya sasa ya uchumi ni nzuri ambapo watu wengi wanapenda iendelee kuwa hivyo, hata hivyo jitihada zinafanywa na serikali yetu za kulinganisha uchumi wa Angola na ule wa nchi za SADC," aliongeza.

Alibainisha kuwa uhusiano ambao umekuwapo baina ya nchi za Tanzania na Angola ni mzuri na wa kuigwa.

"Ni uhusiano uliofungamana kuanzia viongozi wetu wa awali ambao ni Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere wa hapa na Dk. António Agostinho Neto wa Angola, kwani Tanzania imejitolea kwa kiasi kikubwa sana katika ukombozi wa Angola," alisema.

Hata hivyo, kutokana na sababu mbali mbali, uhusiano huu wa kindugu haukuweza kutafsiriwa vizuri kwa kibiashara. "Moja ya kazi zangu kama Balozi mpya wa Angola hapa Tanzania ni kuanzisha upya somo hili na tayari tumeanza kukusanya mawasiliano muhimu," alisema.

Alisema ni matumaini yake kuwa tarehe kama ya leo mwaka kesho atakuwa anatangaza jinsi tulivyofanikiwa kibiashara baina ya nchi mbili hizi.

Fursa zipo tele, ninaialika sekta binafsi kutoka pande zote kuchangamkia suala hili," alisema. "Tunahitaji watu wa nchi zote kuwa wamoja katika masuala yote ikiwemo michezo na utamaduni," aliongeza.

Aidha, lisema ni muhimu kuimarisha ushirikiano wa kitaasisi.

Ni muhimu pia kusaidia jamii ya wafanyabiashara kutoka nchi mbili kutumia vizuri rasilimali zinazopatikana na kuwapa ulinzi wa kutosha na kuwapa vivutio zaidi.

"Yote haya yanaweza kupatikana kupitia makubaliano , mikutano na majukwaa mbali mbali. Tutajitahidi kuhakikisha kuwa ushirikiano huu uliokuwepo baina ya nchi mbili hizi unaendelea kuimarika," alieleza.

Balozi huyo alisema Tanzania ni maarufu sana kwa uzalishaji wa chakula na ina vivutio vingi sana vya utalii na kuahidi kuwaleta watalii wa Angola na wawekezaji na kuongeza kuwa tokea alipokuja nchini tayari amewasiliana na mamlaka husika kwa kuangalia maeneo ya ushirikiano ambayo yatanufaisha pande zote mbili.

# Kampeni ya vyoo shuleni yapata mil. 80/-

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, amekabidhi Sh. milioni 80 kwa halmashauri nne, ambapo kila moja imepata Sh. milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo shuleni.

Byakanwa aliyasema hayo mkoani hapa alipokuwa akitoa taarifa juu ya kampeni hiyo ya 'shule ni vyoo' inavyokwenda.

Alisema fedha hizo ni za michango iliyokusanywa katika kampeni yake ya 'shule ni choo' ambapo wadau mbalimbali mkoani hapa wameshangia baada ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kuhamasisha kuhusu ujenzi wa miundombinu ya vyoo. Byakanwa alisema kuwa halmashauri zilizopata mgao huo ni Nanyumbu, Masasi, Newala na Tandahimba.

Aidha, alisema mgawo wa vifaa kama saruji na vifaa vingine vinavyotumika kwenye ujenzi bado vinaendelea kuratibiwa na baada siku siku chache vitatolewa.

Alisema vifaa hivyo vitafikishwa katika halmashauri zote za mkoa wa Mtwara ili vianze kutumika.

Kadhalika, Mkuu huyo wa Mkoa aliahidi kukamilisha mgao huo wa Sh. milioni 20 kwa halmashauri zilizosalia baada ya kupata Sh. milioni 100 zilizoahidiwa na Wizara ya Elimu. "Nashukuru kampeni hii inafanikiwa kwa kiwango kikubwa na kasi mzuri, lengo letu tuone kila shule iliona changamoto ya matundu ya vyoo inakuwa na vyoo bora," alisema Byakanwa. Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Mkurugenzi Mtendaji, Changwa Mkwanzu, amezindua matundu nane ya vyoo katika Shule ya Msingi Mpitimbi.

Mkwanzu alisema wanaunga mkono kampeni hiyo na kwamba watahakikisha kila shule inakuwa matundu bora ya vyoo.

"Sisi jana kupitia kampeni hii tayari tumeanza kuzindua matundu nane ya vyoo katika Shule ya Msingi Mpitimbi na tutaendelea katika shule zingine," alisema Mkwanzu.

Pia alibainisha kuwa halmashauri ina mpango kabambe wa kuona mazingira ya shule zote yanakuwa mazuri.

# Bunge, Unicef kulinda watoto

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

BUNGE limeingia mkataba wa makubaliano (MoU) wa mwaka mmoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef) kwa ajili ya kulinda, kutetea haki za watoto.

Akizungumza baada ya kufanyika kwa makubaliano hayo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema kuwa mkataba huo utawawezesha wabunge wa kamati ya serikali za mitaa na huduma za jamii kusafiri sehemu mbalimbali nchini wakishughulikia masuala yanayowahusu watoto.

Alisema pia itasaidia wabunge kupata rasilimali zaidi zitakazowasaidia katika kutetea na kulinda haki za watoto katika kipindi cha mwaka mmoja kisha mkataba huo utasainiwa upya katika bunge la 12.

"Changamoto za watoto ni nyingi, bunge nalo lina nafasi katika kuliangalia suala hili, bunge huwa linatunga sheria za watoto, hivyo Unicef watatuongezea rasilimali zitakazosaidia kupambana na haki za watoto," alisema Ndugai na kuongeza:

"Unapozungumzia masuala ya barabara, maji, kilimo, ni lazima umguse mtoto, hivyo bunge lina nafasi kubwa sana katika kuhakikisha haki za mtoto zinalindwa, na ndiyo maana leo tumekubali kuingia nao makubaliano," alisema Spika Ndugai.

Mwakilishi wa Unicef mchini, Rene Van Dongen, alisema ushirikiano huo umekuja wakati mwafaka wakati dunia ikisherehekea kutimia kwa miaka 30 ya mkataba wa haki za watoto.

"Takwimu zinaonyesha idadi ya watoto Tanzania itaongezeka mara mbili na kufikia milioni 58 katika kipindi cha miaka 30 ijayo," alisema Van Dongen.

Alisema serikali ya Tanzania imefanikiwa kwa asilimia kubwa katika kuhakikisha haki za watoto zinapatikana, lakini kuna changamoto nyingi ambazo bado hazijatatuliwa.

Van Dongen alisema Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha watoto wanapata haki zao, kwamba idadi ya watoto walioandikishwa shule imezidi kuongezeka, vifo vya watoto waliochini ya miaka mitano vimepungua, watoto wengi wanaozaliwa wanapewa vyeti vya kuzaliwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Maendeleo ya Jamii Peter, Serukamba, alisema wazazi wanajukumu kubwa la kuhakikisha haki za watoto zinalindwa wakati wote.

Alisema wao kama wabunge watahakikisha watoto nchini wanapewa haki zao, kwa kuwatetea bungeni na kuhakikisha sheria nzuri zinatungwa kuhakikisha wanaishi katika mazingira rafiki.

## Wanafunzi h'shauri kupimwa mimba

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

BARAZA la Madiwani Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi limeagiza wanafunzi wote wa shule za sekondari na msingi waliopo darasa la tano na la sita wapimwe ujauzito baada ya wanafunzi 18 wa shule mbili za sekondari kubainika kuwa wajawazito.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki katika kikao cha Baraza la Madiwani cha kwanza katika robo ya mwaka wa fedha 2019/ 2020.

Awali kabla ya uamuzi huo mwenyekiti wa Kamati ya kudhibiti Ukimwi wa baraza hilo, Lucas Kanoni, alilieleza baraza hilo kuwa hali ya mimba za utotoni bado ni tishio katika katika manispaa hiyo.

Alisema katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita, jumla ya wanafunzi 18 wa shule mbili za sekondari walipimwa na kubainika kuwa wana ujauzito wa miezi mitatu.

Kanoni alisema wanafunzi wa shule za sekondari za Kashaulili na Kasimba walipimwa ujauzito na ilibainika kuwa katika sekondari Kasimba wanafunzi 15 walikuwa wajawazito na Kashaulili wanafunzi watatu.

Baada ya taarifa hiyo madiwani walishtushwa na taarifa hiyo ya shule mbili za sekondari kuwa na idadi kubwa kama hiyo ya wanafunzi wajawazito.

Meya wa Manispaa hiyo, Willy Mbogo, alisema kuwa tatizo la mimba za utotoni bado ni kubwa katika Manispaa ya Mpanda na hali hiyo haikubaliki kwani ni aibu kubwa na haivumiliki.

Alimwagiza Ofisa Elimu Shule za Sekondari kutoa taarifa ya hatua ambazo zimechukuliwa kwa watu waliowapa ujauzito wanafunzi hao.

Mbogo alitoa mfano kwa kusema kuwa hivi karibuni walimu wa Shule ya Msingi Majengo walimbaini mwanafunzi mmoja mwenye umri wa miaka 14 akiwa na ujauzito na walipomuoji aliwaeleza ujauzito huo alipewa na baba yake mzazi, hivyo walichukua jukumu la kumfungulia kesi polisi na mzazi wa mtoto huyo baada ya kupatikana na hatia Mahakama ilimuhukumu kifungo cha maisha.

Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Emeriana Tungulu, alisema changamoto iliyopo kwa wanafunzi wanaopata ujauzito ni kutosema ukweli wanapotakiwa wamtaje mtuhumiwa aliyempa ujauzito, kwani wamekuwa wakidai hajulikani.

Pia baadhi yao wamekuwa wakisingizia kuwa aliyempa ujauzito alikutana naye mara moja tu mnadani hivyo baada ya hapo hajui mtuhumiwa alipo.

Changamoto nyingine ni wazazi wenyewe wamekuwa hawatoi ushirikiano pindi wanapokuwa wakihitajika kutoa ushirikiano.

# Wahitimu Veta watakiwa kujiajiri

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Ufundi Stadi (VETA) Kanda ya Dar es Salaam, kimeshauriwa kuwaandaa wahitimu wake ili wawe na mtazamo wa kujiajiri wanapohitimu badala ya kutegemea kuajiriwa.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Meneja Rasilimali Watu wa Kampuni ya Kioo Limited, Jacob Msuya, aliyekuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya chuo hicho yaliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Msuya alisema serikali haibebi jukumu la kuajiri moja kwa moja bali inaweka tu mazingira mazuri na kutoa mwongozo utakaowezesha elimu inayopatikana itumike ipasavyo.

"Mkuu wa chuo umeeleza jinsi mnavyoendesha mafunzo kwa kushirikiana na taasisi zisizo za kiserikali mfano International Youth Foundation (IYF), kuwasaidia wanafunzi katika kupata mbinu bora za kuweza kupata ajira au kujiajiri wenyewe nawapongeza sana chuo pamoja na mashirika haya kwa uamuzi wenu," alisema. Alisema wahitimu hao wanaweza kufanya kazi vizuri katika katika vikundi vya ujasiriamali, taasisi za umma na makampuni au viwanda binafsi, serikali, au kuendesha shughuli zao wenyewe popote watakapokuwa. Aliwashukuru wazazi na walezi wote kwa kuwawezesha vijana hao kuhudhuria mafunzo ya ufundi stadi katika Chuo cha Veta DSM na aliwaomba wasichoke kuwapa fursa kama hizo vijana hao kwani ndio taifa la kesho.

Vilevile Msuya aliwashukuru waajiri wote kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kuwawezesha vijana hao kupata mafunzo ya vitendo kwenye maeneo yao ya kazi na pia kuwapatia ajira.

Alisema Kampuni ya KIOO Limited na Chuo cha Ufundi VETA Dar es Salaam wapo kwenye Mkataba wa Makubaliano (MOU) kuhusu utekelezaji wa mpango wa kukuza ujuzi.

Msuya alisema nchi ina uhaba mkubwa wa mafundi waliobobea katika fani mbalimbali hivyo VETA DSM ina nafasi nzuri ya kupunguza uhaba huo na kwamba serikali inatambua na kufurahishwa na mchango wa chuo hicho. "Jitihada mnazofanya hasa kwa kuzingatia mazingira magumu mnayokabiliana nayo. Kadri idadi ya wataalamu inavyoongezeka ndivyo tunavyosonga mbele kufikia lengo letu la kujitegemea kama Taifa," alisema Msuya

Msuya alisema sekta binafsi itaendelea kushirikiana na serikali wakati wote, kufanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba Chuo cha Ufundi VETA Dar es Salaam kinaendelea kuwa miongoni mwa vyuo vyenye hadhi bora katika mkoa wa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla.




Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akizungumza na Ofisa Uhusiano Msaidizi wa Wateja wa Kilimo wa Benki ya NMB, Vivian Sakoe, baada ya kufunga Mkutano Mkuu wa 13 wa Shirikisho la Wadau wa Korosho Afrika (ACA) jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Ushirikiano wafanyabiashara, taasisi fedha muhimu uchumi wa viwanda'

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

JUHUDI binafsi za wafanyabiashara kwa kushirikiana na taasisi za kifedha ni moja ya nyenzo muhimu katika kufikia malengo ya mpango mkakati wa serikali ya awamu ya tano katika kutoa kipaumbele katika uchumi wa viwanda.

Hayo yalisemwa na Mjumbe wa Bodi ya NBC, Dk. Kassim Hussein katika hafla ya uzinduzi wa Klabu ya Biashara ya NBC, maarufu kama 'NBC B-Club' ya Mkoa wa Morogoro ikiwa ni klabu ya 11 kuzinduliwa katika mikoa mbalimbali nchini .

"Kwenye biashara serikali imefanya mageuzi makubwa mfano katika kuwahamasisha wafanyabiashara kutumia mashine za kielektroniki, kurasimishwa kwa biashara, lakini kunahitaji juhudi kubwa katika kuangalia masuala ya masoko, vifungashio, mitaji na viwango vya TFDA ili kufanya biashara hizo zikue," alisema.

Ni kutokana na hayo alisema NBC B-Club itakuwa faida kubwa kwa wafanyabiashara na nguvu ya kuleta maendeleo kwa taasisi na mtu mmoja mmoja, huku benki NBC ikiongeza mafunzo ya mara kwa mara kwa kuleta wataalamu mbalimbali na kutoa punguzo la riba kwa wanachama wa klabu hizo.

Akizungumza zaidi kuhusu klabu hiyo Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara cha benki hiyo, Elvis Ndunguru, alisema lengo pia ni kuwakutanisha wafanyabiashara mbalimbali ili kuweza kubadilishana uzoefu, kupata fursa mbalimbali za masoko ndani na nje ya nchi pamoja na kuwaunganisha na wafanyabiashara wa nje.

Ndunguru alisema ni rahisi kutoa nafasi ya elimu kwa wafanyabiashara hao kupitia klabu zao, kwenye maeneo wanayobaini yanayotakiwa elimu baada ya kupata mrejesho toka kwa wateja wao.

"Klabu za Biashara tumeshazianzisha maeneo mbalimbali Tanzania, lakini lengo hasa ni kuwakutanisha wafanyabiashara mbalimbali ili kuweza kugundua fursa, kuwapa elimu, kuleta wataalamu tofauti, pia kuna fursa za kupeleka wafanyabiashara katika nchi mbalimbali," alisema Ndunguru.

Pia alisema wanatarajia kuongeza nchi nyingine ambazo zinafanya vizuri kibiashara ikiwamo Uturuki, Ujerumani na Marekani, na kwamba wana mpango wa kutengeneza dirisha maalum la wafanyabiashara wanawake wadogo na wakati ili kuwahamasisha zaidi kuingia katika biashara.

Awali akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Ofisa Uvuvi na Mifugo Manispaa ya Morogoro, Mohamed Chamzimu, alisema Klabu hiyo itawawezesha wanachama hao kuwa na uelewa wa biashara wa kisasa, na kwamba mafunzo wanayoyapata yataleta tija na kuongeza weledi katika shughuli zao.

Chamzimu aliwataka wafanyabiashara hao kujitokeza na kujiunga kwa wingi katika klabu hiyo kwa manufaa yao na Taifa kwa ujumla.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Bupe Kamugisha, wameipongeza benki hiyo kwa huduma bora na masharti nafuu ya kuchukua mikopo na kusema kwamba imekuwa haina vitendo vya kutaifisha mali za wateja wao pindi wanapopata ugumu kwenye marejesho.



## HABARI ARUSHA

# Waziri aagiza viongozi wa Saccos wakamatwe

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ameagiza kukamatwa kwa viongozi wa Kurugenzi Saccos ya Mkoa wa Arusha kutokana na kuhujumu chama hicho kwa ubadhirifu wa fedha za wanachama wake zaidi ya Sh. bilioni 2.4

Agizo hilo alitoa jana jijini hapa, baada ya kuitisha kikao cha dharura katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Arusha na kupokea malalamiko kutoka kwa wanachama na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Ushirika, juu ya uwapo wa mwenendo mbovu wa viongozi hao, kujichukulia maamuzi pasipo kushirikisha wanchama wake.

Hasunga aliliagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha linawakamata viongozi wote walioshiriki kula fedha hizo, akiwamo aliyekuwa Mwenyekiti wa Saccos, Dk. Freedom Matiago na Makamu wake, Gasper Kanyasita, meneja wa chama hicho pamoja na viongozi wa vikundi 14, hewa waliopatiwa mkopo wa Sh. milioni 40.

"Nimesikitika sana kuona watu hawa bado wapo mitaani wakiendelea kula maisha wakati wapo watu wanaumia kwa ajili ya kuhitaji mafao yao na fedha zao walizojiwekea kama akiba kwa manufaa yao ya baadaye," alisema na kuendelea:

"Naagiza kuanzia leo watu wote waliokula fedha hizo popote walipo wakamatwe ili warejeshe fedha hizo, siwezi kufumbia macho suala hili wakati watu wetu wanaumia Jeshi la Polisi hakikisheni mnawakamata na kuwafungulia kesi ya uhujumu uchumi wasipate dhamana."

Awali akitoa taarifa fupi ya Saccos hiyo, Msajili Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Arusha, Emanuel Sanka, alisema tangu mwaka 1990 chama hicho kianzishwe kinajumla ya wanachama 780, ambapo wastaafu wanaidai mafao na akiba ya Sh. milioni 831.

Alisema pia wanachama wanaoendelea na mfuko nao wanadai Sh. milioni 770, huku taasisi za CRDB, NSSF na Tumaini Saccos ya Shirika la World Vision Tanzania, wakikidai chama hicho Sh. milioni 884.

Baadhi ya wanachama hao walikiri kutoshirikishwa katika vikao na viongozi wamekuwa wakifanya maamuzi ya kutoa mikopo ovyo kwa watu wanaowafahamu wao na wanachama wakiomba mikopo kwa ajili ya matibabu wananyimwa.

Kwa upande wa Kareti Piniel alimweleza Waziri Hasunga kwa muda mrefu ameitumikia serikali akiwa muuguzi mkunga katika Hospitali ya Mount Meru mkoani Arusha, baada ya kustaafu alipokea Sh. milioni 50 kama kiinua mgongo na kuwekeza katika amana yake ndani ya Saccos hiyo.

"Nasikitika kuona fedha hizi zimetafunwa na viongozi hao, sababu kila nilipohitaji nilinyimwa hata nikiumwa, naomba Waziri unisaidie mimi na wenzangu tupate stahiki zetu," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alimweleza Waziri Hasunga Saccos hiyo imekuwa changamoto kwa wanachama wake, na kuonekana kusuasua kwa muda sasa, huku akisema kuwa ushahidi wa wazi unaonyesha watu hao wameshiriki kula fedha hizo, na kuwatupia lawama viongozi wa vyama vya ushirika ngazi za wilaya na mkoa.

"Lakini ni wazi usimamizi ulikuwa mbovu ambao wameshindwa kuwajibika ipasavyo, hivyo kuwa sehemu ya kuongeza hasara na kuwapa mzigo mzito wanachama, hivyo sisi kama viongozi wa mkoa msimamo wetu ni kuhakikisha tunalinda haki za wanachama ambao ni wananchi wangu," alisema Gambo.



Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogolo (kushoto), akionyesha magunia ya mkaa yaliyokamatwa baada ya kukiuka sheria ya misitu na nyuki katika Msitu wa Sambalu, mkoani Singida, wakati akizungumza na waandishi wa habari eneo la tukio mwishoni mwa wiki. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**

# RC Mnyeti agawa pikipiki kwa watendaji kata, vijiji

**Na Allan Isack,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, ametoa pikipiki sita kwa watendaji sita kati ya nane katika Kata za Mjini Babati, ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa usafiri kwa watumishi wa serikali.

Akizungumza wakati wa kukabidhi pikipiki hizo, Mnyeti alisema kutokana na changamoto ya usafiri kwa watumishi wa umma amegawa pikipiki hizo ili waweze kuwafikia kwa karibu wananchi katika utoaji wa huduma.

Alisema pikipiki hizo zenye thamani ya Sh. milioni 14.3, zimenunuliwa na Halmashauri ya Mji wa Babati, kupitia fedha za kujenga uwezo zitokanazo na uendelezaji wa miji (ULGSP).

Alisema kupatikana kwa vitendea kazi hivyo vitakuwa nyenzo bora ya kuwafikia wananchi zaidi tofauti na awali kwani watumishi hao walishindwa kuwafikia kutokana na kukosekana kwa usafiri wa uhakika.

Alisema watendaji waliopewa pikipiki hizo, ni wale wanaotokea kata za pembezoni mwa mji wa Babati, huku akiwasisitiza kutokaa ofisini wahakikishe wanakwenda kutoa huduma kwa wananchi.

Alimwagiza Mkurugenzi wa Mji wa Babati, Fortunatus Fwema, kuhakikisha maofisa watendaji wa kata za Babati na Bagara, wananunuliwa pikipiki kama wenzao.

Fwema alisema wapo kwenye mchakato wa kuhakikisha wananunua pikipiki za watendaji wa kata hizo.

"Baada ya kuwanunulia pikipiki watendaji wa kata zilizo pembezoni tunaahidi kutekeleza agizo lako la kuwanunulia watendaji wawili wa Babati na Bagara ili kukamilisha kata zote nane," alisema Fwema.

Ofisa Utumishi wa Halmashauri hiyo, Sadiki Mrisho, alisema pikipiki hizo zinatakiwa kutumiwa na watumishi hao wa serikaki kwa matumizi ya kiserikali.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sigino, Evelin Panga, alisema pikipiki hizo zitawasaidia kufika kiurahisi katika shughuli zao vijijini.

Panga aliishukuru serikali kwa kuwapatia nyenzo hizo za usafiri kwani awali walikuwa wanatembea kwa miguu kutoka sehemu moja hadi nyingine.

# Tanzanite sasa wapewa kibano

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

WAMILIKI wa migodi na wenye leseni za uchimbaji madini ya Tanzanite Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wametakiwa kuwasilisha taarifa ya mauzo yote waliyozalisha kuanzia Januari 2018 hadi sasa.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima, alisema juzi kuwa taarifa hiyo inatakiwa iwasilishwe kabla ya Novemba 20, mwaka huu.

Ntalima alisema mambo ya kuzingatia kwenye taarifa hiyo ni pamoja na kuambatanisha nakala ya risiti ya mauzo ikionyesha sehemu ulipouzia madini hayo.

Alisema taarifa hiyo, inatakiwa kuonyeshe madini uliyohifadhi, uliyouza bila kusahau nakala ya risiti ya mauzo.

Alisema inatakiwa ionyeshe thamani ya madini waliyonayo mrabaha waliolipa, ada ya ukaguzi na namba ya risiti ya mauzo hayo.

"Na kama madini hayo yapo nyumbani orodhesha ni kiasi gani na risiti ya malipo ya kodi ziambatanishwe," alisema Ntalima.

Alisema agizo la wanunuzi wakubwa na wachimbaji waliotakiwa kufika kwenye ofisi hiyo limeahirishwa hadi watakapotangaziwa.

Hata hivyo, mmoja kati ya madalali wa madini ya Tanzanite, William Orata alisema serikali inapaswa kuanza kuweka utaratibu wa kununua madini ili kuondokana na tatizo la kunyonywa na wanunuzi wakubwa.

"Serikali inatoa bei nzuri ya ununuzi wa madini lakini kikwazo ni wanunuzi wakubwa wanatulalia hivyo serikali iwe inanunua madini," alisema Orata.

Dalali mwingine wa madini, Ambrose Ambonya alisema baadhi ya wanunuzi wakubwa wa madini wenye asili ya bara la Asia wamekuwa kikwazo kikubwa kwao.

"Hawa ndiyo wanasababisha bei ya madini ya Tanzanite yawe yanashuka kila mara kwani wanafanya mchezo mchafu kwa kuteka soko sababu ni wenyewe wenye mitaji mikubwa," alisema Ambonya.

## Wachangamkia uzalishaji fiwi

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

KASI ya wananchi wa vijiji vya pembezoni katika Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro kuchangamkia kilimo cha uzalishaji wa fiwi kwa ajili ya malighafi ya viwandani, imeanza kutia moyo baada ya serikali kufungua milango.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusiana na maendeleo ya zao hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Zefrin Lubuva, alisema idadi ya wakulima waliojitokeza kulima zao hilo ambao linastahimili ukame kwa muda mrefu inatia moyo.

Halmashauri hiyo mpaka sasa, imetenga hekta 750 za ardhi ambayo inatoa fursa ya uwekezaji wa shughuli za kilimo.

"Tumekwenda kukagua mashamba darasa pamoja na wakulima wanaolima zao hilo na tumeridhishwa na idadi ya waliojitokeza kulima fiwi mwaka huu. Zao hili lina mafanikio makubwa kiuchumi na soko kubwa liko nchi za Kenya na India ambako wananchi wake wengi hupenda kutumia kama chakula," alieleza.

Fiwi ni aina fulani ya maharage jamii ya kunde, ambayo hulimwa katika maeneo yenye ukame, kwa sababu zao hilo hustahimili sana ukame kwa muda mrefu.

Aidha, alisema ardhi hiyo imetengwa katika Kata ya Kirya, Kileo na Kivulini. Katika Kata ya Kirya peke yake kuna jumla ya hekta 900 za umwagiliaji ambapo hadi sasa hekta 150 tu ndizo ambazo zinatumika.

"Wawekezaji wanakaribishwa kuja kuendeleza hekta zilizo baki ambazo zina rutuba nzuri na hali ya hewa nzuri inayoruhusu kilimo cha umwagiliaji kwenye eneo hili. Eneo lingine ambalo linafaa kwa kilimo cha umwagiliaji ni Kijiji cha Kileo chenye jumla ya hekta 2,400 ambazo zinafaa kulimwa kwa kipindi chote cha mwaka," amesisitiza mkurugenzi huyo.

Kijiji cha Kivulini chenyewe, kina jumla ya hekta 1,050 ambapo hekta zinazotumika kwa kilimo ni 400 tu.

Wakati katika Tarafa ya Jipe Ndea, nayo imetengwa kama maeneo yenye ardhi ya kutosha inayofaa kwa kilimo. Mazao yanayostawi ni alizeti, mtama, uwele, miwa, mahindi, maharage, ngwara, korosho, mbogamboga, matunda na mpunga.

# Jopo madaktari bingwa wa Uingereza kutoa matibabu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

JOPO la madaktari bingwa kutoka Uingereza, kwa kushirikiana na Hospitali ya Rufani ya KCMC, imetangaza kuanza kutoa matibabu ya upasuaji sanifu kwa wagonjwa wenye ulemavu unaotokana na makovu ya moto kwa watoto na watu wazima.

Mkuu wa Idara ya Upasuaji ya KCMC, Dk. David Msuya, amethibitisha jopo la madaktari hao limeshawasili nchini na matibabu ya upasuaji huo yatafanyika kuanzia Novemba 11 hadi 15 mwaka huu. "Tayari madaktari bingwa kutoka Uingereza wameshafika Moshi na leo (Novemba 11), ndio wanaanza rasmi kazi hiyo pamoja na madaktari bingwa wa KCMC. Tunawaomba wagonjwa wa aina hii wafike KCMC katika wodi ya walioungua (burn unit) kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana kwa uchunguzi zaidi," alisema Dk. Msuya.

Akizungumzia zaidi matibabu hayo ya upasuaji, Ofisa Uhusiano wa Hospitali ya KCMC, Gabriel Chisseo, alisema jopo la madaktari wa KCMC litaongozwa na daktari bingwa wa upasuaji wa hospitali hiyo, Dk. Kondo Chilonga.

Kwa mujibu wa Chisseo, gharama za matibabu ya upasuaji huo zitachangiwa kulingana na tatizo la mhitaji wa huduma hiyo.

Zaidi Chisseo alisema: "Huduma hii tunaitoa kwa wagonjwa ambao wamepata matatizo mbalimbali ya viungo kutokana na makovu mwilini yatokanayo na ajali za barabarani ama majanga ya moto, lakini pia lengo ni kuendelea kuwajengea uwezo wataalamu wetu wa ndani."

"Kuna aina mbalimbali za makovu, wapo ambao walipona kidonda lakini wakabaki na makovu mabaya yakafanya washindwe kutumia viungo vyao, mfano mikononi, miguuni au usoni, hawa tunawarekebisha ili waweze kumudu maisha yao na warejee katika hali ya kawaida.

Kwa sasa, Hospitali ya KCMC imefanikiwa kuboresha huduma katika kitengo cha huduma ya wagonjwa wa nje na wagonjwa wanaolazwa kwa sasa ni zaidi ya 36,470 kwa mwezi na asilimia 79.7 ya wagonjwa wote wanaohudumiwa katika Hospitali ya KCMC wanatoka kwenye mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tanga, na Singida.

Hospitali hiyo ya Rufani ya Kanda ya KCMC, inamilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na inasimamiwa na Shirika la Msamaria Mwema (The Good Samaritan Foundation of Tanzania).



Viongozi wa vyama vya msingi, mkaguzi wa zao la tumbaku Wilaya ya Kahama na Mkurugenzi wa Kampuni ya Petrobena, Peter Kumalilwa, wakikagua shamba la mmoja wa mkulima wa tumbaku la uoteshaji wa mbegu ya zao hilo ikiwa ni maandalizi ya msimu ujao.
**PICHA: SHABAN NJIA**

# Watumishi Same wahamia maeneo ya kazi kwa 70%

**Na Godfrey Mushi,** SAME

AGIZO la Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Rosemary Senyamule la kuwataka watumishi wa serikali wanaoishi nje ya vituo vyao vya kazi, kuhamia katika maeneo hayo limetekelezwa kwa asilimia 70.

Jana, Senyamule alithibitisha kuwa watumishi hao walikuwa wameripoti tayari katika vituo vyao vya kazi ili kuepuka adhabu ikiwamo kusimamishwa kazi.

"Nimewafuatilia kwa ukaribu sana ni kwa namna gani wanatekeleza maelekezo yangu na nimegundua wamenielewa, kwa sababu hadi kufikia wiki iliyopita walikuwa wamehamia vijijini kwa asilimia zaidi ya 70, ukiachilia mbali wale wenye udhuru ikiwamo kuwa masomoni," alisema.

Mwezi Septemba mwaka huu, Mkuu huyo wa Wilaya alitangaza kuwa watakaokaidi agizo la kuhamia kwenye vituo vyao hadi kufikia Septemba 30 mwaka huu, wangekumbana na adhabu.

Uamuzi wa Senyamule aliutoa baada ya kuzunguka vijijini na kupokea malalamiko ya wananchi kwamba watendaji wa vijiji, kata na baadhi ya watumishi wa umma, wanaishi nje ya maeneo yao ya kazi na hivyo wanapohitaji huduma za haraka hukosa msaada.

Sheria ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2014, inamtaka mtumishi aishi eneo kilipo kituo cha kazi na inawalazimisha watumishi wote wa umma wafuate sheria, kanuni na taratibu za utumishi na atakayeshindwa kuhamia atakuwa amejiondoa kwenye utumishi.

Kutokana na agizo hilo, Senyamule amemtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Anna-Claire Shija, kumpelekea orodha ya majina ya watumishi wa umma wote waliohama tayari kwenda katika maeneo yao ya kazi na wale ambao hawahami mpaka sasa.

Mwezi Juni mwaka jana, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiwa katika ziara ya kikazi Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma, aliagiza watumishi wote nchini wanaoishi mjini wahamie katika vituo vyao vya kazi ili wawe karibu na wananchi.

Alielekeza kuwa watakaokaidi, Wakuu wa Wilaya wakabidhi orodha yao kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo ili awashughulikie kwa kutotekeleza agizo lake.

# Nipashe Spotika



VIATU VYA SOLSKJAER UNITED VITAWATOSHA UK. 16&17

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich, Robert Lewandowski, anashikilia rekodi ya aina yake ya kufunga hat-trick ya haraka zaidi, nyota huyo raia wa Poland alifunga hat-trick ndani ya dakika 3 na sekunde 22. Hiyo ilikuwa ni Septemba 22 mwaka 2015 wakati klabu yake ilipocheza dhidi ya Wolfsburg.





## HUKATIZI!...

Beki wa Arsenal, Calum Chambers (kushoto0 akijiandaa kumdhibiti mshambuliaji wa Leicester City, Jamie Vardy, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi usiku. Arsenal ilichapwa mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**



# REKODI 5 ZAKUSHANGAZA MABAO YA LEWANDOWSKI

**MUNICH,** Ujerumani

TANGU kuanza kwa msimu huu wa 2019/20, mshambuliaji wa kimataifa wa Poland, Robert Lewandowski, ameonekana kuwa tishio kubwa kwa walinzi wa timu pinzani. Anaonekana kama vile yupo kwenye sayari ya kivyake kabisa.

**Ni mmoja wa washambuliaji wanaotisha zaidi barani Ulaya kwa sasa kutokana na uwezo wake mkubwa wa kuzifumania nyavu.**

Akiwa na klabu yake ya Bayern Munich, anaonekana kuwa kwenye mbio za peke yake za kuwania kiatu cha dhahabu kwa ufungaji mabao mengi kwenye ligi tano kubwa za Ulaya.

Hadi sasa amefunga mabao 13 katika mechi tisa tu alizocheza kwenye Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga.

Makala hii inakuchambulia rekodi tano za kushangaza kwa ufungaji kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31.

### 5. MABAO MENGI ZAIDI KUFUZU KOMBE LA DUNIA 2018

Baada ya Poland kukosa kushiriki michuano ya Kombe la Dunia ya mwaka 2010 na 2014, aliweka rekodi ya aina yake wakati wa kufuzu kwa michuano hiyo ya mwaka 2018.

Alifunga mabao 16 wakati wa michuano ya kufuzu na kumpiku Cristiano Ronaldo, ambaye alifunga mabao 15 kwenye harakati hizo za kufuzu akiwa na Ureno.

Lakini alishindwa kuisaidia nchini yake kwenye michuano hiyo na Poland ikatolewa hatua ya makundi.

### 4. HAT-TRICK YA HARAKA ZAIDI BUNDESLIGA

Kafunga mabao matatu 'hat-trick' katika mchezo mmoja kwa mshambuliaji ni kitu cha kuvutia zaidi.

Lewandowski alijiweka rekodi ya aina yake kwa kufunga hat-trick ya haraka zaidi ndani ya dakika 3 na sekunde 22.

Hiyo ilikuwa ni Septemba 22 mwaka 2015, akicheza dhidi ya Wolfsburg. Na hiyo ilikuwa ni hat-trick yake ya kwanza akiwa kwenye jezi za Bayern Munich.

### 3. MABAO MATANO YA HARAKA ZAIDI ULAYA

Mchezaji huyu wa zamani wa Borussia Dortmund alifunga mabao matano Septemba 22 mwaka 2015, kwa kipindi cha chini ya dakika tisa.

Na hiyo ilimfanya kuwa mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi kwa kipindi kifupi zaidi kwenye Ligi tano kubwa Ulaya.

### 2. MABAO MENGI EURO 2016

Lewandowski hadi sasa anashikilia rekodi ya kuwa mfungaji wa wakati wote wa timu ya taifa ya Poland akiwa amefunga mabao 60.

Wakati wa kufuzu kwa michuano ya mataifa ya Ulaya, Euro 2016, alifunga mabao 13. Pia hadi sasa ameisaidia Poland kukata tiketi ya kushiriki michuano ya Euro 2020 akiwa amefunga mabao matano.

Wakati wa kufuzu kwa Euro 2016, alifunga mabao hayo 13 katika mechi 10, ikiwamo hat-trick dhidi ya Georgia, ambapo alifunga ndani ya dakika nne tu.

### 1. KUFUNGA MECHI TISA MFULULIZO BUNDESLIGA

Pengine bila shaka kwa sasa ndio mshambuliaji bora zaidi kwenye Ligi Kuu Ujerumani kwa sasa.

Ameweka rekodi ya kuwa mshambuliaji wa kwanza kwenye historia ya Ligi Kuu Ujerumani, kufunga mabao katika mechi tisa mfululizo za ufunguzi wa ligi hiyo, akiipiku rekodi ya Pierre-Emerick Aubameyang, ambaye alifunga mabao nane katika msimu wa 2015/16.

Ameendelea kuwa na rekodi ya aina yake Bundesliga ikiwamo ile ya kuwa mchezaji wa kigeni aliyefunga mabao mengi zaidi nchini Ujerumani, ambapo hadi sasa amefikisha mabao 215.

Pia ni mmoja wa wachezaji wa kigeni aliyefanikiwa kufikisha mabao 100 kwenye michezo 168.

Hadi sasa amejiweka rekodi ya kuwa mfungaji wa mabao mengi zaidi kwenye ligi tano kubwa za Ulaya.

Na hivi karibuni alikwea hadi nafasi ya tano kwa kuwa mchezaji aliyefunga mabao mengi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa amefikisha mabao 37.

**JE, WAJUA?**



UONGOZI wa KMC FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara imeamua kuachana na Kocha Mkuu, Jackson Mayanja, kufuatia mwenendo mbaya wa timu hiyo ambayo inamilikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni jijini Dar es Salaam.



PLUIJM

# MAKOCHA 5 WANAOWEZA KUMRITHI ZAHERA

Na Adam Fungamwango

SIKU chache tu baada ya kuondolewa katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Yanga ilimtimua kocha wake mkuu, Mkongomani Mwinyi Zahera.

**Ni baada ya kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya Pyramids ya Misri nyumbani na kwenda kufungwa magoli 3-0 ugenini.**

Viongozi wa Yanga hawakutaja sababu yoyote ya kumtimua kocha huyo aliyekuwa kipenzi cha Wanayanga, zaidi ya kusema kuwa wameachana na kocha huyo baada ya makubaliano ya pande zote mbili.

Hata hivyo, Zahera mwenyewe amekuwa akipita kwenye vyombo vya habari, na katika maelezo na malalamiko yake, yanaonyesha kuwa hakuna makubaliano ya pande mbili bali ameondoshwa bila yeye kupenda.

Dalili za Zahera kutimuliwa zilianza mara baada ya mechi ya kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, ambapo mashabiki walianza kumrushia chupa za maji, wakiimba kwamba hawamtaki, kitu ambacho kilionekana kuwa wanamshtaki kwa uongozi, nao siku kadhaa baadaye ulitekeleza matakwa ya mashabiki wao.

Kwa sasa gurudumu linashikiliwa kwa muda na Charles Boniface Mkwasa, mchezaji, kocha na Katibu Mkuu wa zamani wa klabu hiyo.

Kwenye mechi yake ya kwanza amefanikiwa kushinda baoa 1-0 dhidi ya Ndanda FC, Uwanja wa Namgwanda Sijaona, kwa bao la faulo iliyopigwa na Patrick Sibomana.

Bado kwenye mechi hiyo, Yanga ilionekana kuwa ni ile ile ya Zahera ya kupata magoli yake kwa mikwaju ya faulo au penalti.

Wapo makocha kadhaa wanaotajwa kurithi mikoba ya Mkongomani huyo.

Mwandishi wa makala haya, anaorodhesha makocha watano wanaoweza kurithi mikoba hiyo na kulipeleka mbele gurudumu la Yanga.

**1. BEN MWALALA**

Huyu ndiye kocha anayetajwa zaidi kuliko wenzake kutaka kuchukua mikoba ya Zahera.

Alikuwa ni straika na winga machachari wa klabu hiyo mwanzoni mwa mwaka 2000, baadaye kuwa kocha wa Coastal Union ya jijini Tanga.

Kwa sasa ni Kocha Mkuu wa Bandari ambayo ameifanya kuwa tishio ndani na nje ya Kenya.

Ikumbukwe kuwa ameifanya Bandari kucheza mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika na hivi karibuni nusura itinge makundi ya michuano hiyo, kama si kukutana na kigingi cha Horoya ya Guinea, kwa kufungwa mabao 4-2 ugenini na bao 1-0 nyumbani.

Mwenyewe alikaririwa hivi karibuni katika mechi ya kirafiki dhidi ya Simba kuwa yuko tayari kuifundisha Yanga.

**2. ERNIE BRANDTS**

Ni mmoja wa makocha ambao wanaweza kuitoa Yanga ilipo na kuipeleka inapotaka kuelekea kutokana na uzoefu mkubwa wa soka la Kiafrika.

Mholanzi huyu ameshawahi kuifundisha Yanga kwa mafanikio kuanzia mwaka 2012 hadi 2013 alipositishiwa kibarua chake baada ya kufungwa na Simba mabao 3-1 kwenye mechi ya Mtani Jembe.

Huenda akarejeshwa kwenye kikosi hicho kwa sababu ukiondoa mechi hiyo dhidi ya Simba hakufanya vibaya kwenye mechi zingine na hasa Ligi Kuu.

**3. HANS VAN PLUIJM**

Mholanzi mwingine ambaye aliipa Yanga mafanikio makubwa, ikiwa ni kuibadilisha kutoka soka la kutumia mawinga na pasi ndefu ambalo ni asili ya timu hiyo, kwenda kwenye soka la pasi fupi fupi na lenye ufundi wa hali ya juu, kiasi cha kupewa majina mengi kama 'sambusa' na 'kampa kampa tena.'

Kwa miaka ya hivi karibuni ndiye kocha aliyekuwa na mafanikio makubwa zaidi kwenye klabu ya Yanga akiiwezesha timu hiyo kucheza hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika mara mbili.

Alijiunga na timu hiyo mwaka 2014 hadi 2017 kabla ya kutimuliwa kinyemela kwa kupewa nafasi ya kuwa Mkurugenzi ya Ufundi baadaye akatimka.

Huyu pia anaweza kuwa mwarobaini mkubwa kwa Yanga kama wataamua kumrejesha kwani anaweza kulibadili soka la sasa la timu hiyo ambalo ni la kujilinda zaidi kuliko kushambulia, ikifanya mashambulizi kwa kushtukiza.

**4. KIM PAULSEN**

Huyu ni kocha wa zamani wa timu ya Taifa ya Vijana ya Tanzania na aliyejipatia umaarufu mkubwa kwa kuibua wachezaji wengi vijana ambao kwa sasa wanatamba kwenye Ligi Kuu.

Ni mmoja wa makocha wanaotajwa kuchukua nafasi ya Zahera. Ni kocha mzuri kama Wanayanga wataamua kumvumilia kwa sababu falsafa yake ni ya kutumia zaidi na vijana watakaokuja kuwa bora baadaye.

Hata hivyo, wakati wanaandaa vijana anatakiwa kuwa na wachezaji wakomavu kwa ajili ya kupata matokeo kwani timu nyingi kubwa hazina tabia ya kusubiria mafanikio ya muda mrefu.

**5. MASOUD DJUMA**

Kwa sasa anasubiria simu tu kutoka kwa viongozi wa Yanga arejee Tanzania kwa mara ya pili.

Ni kocha msaidizi wa zamani wa Simba na wakati mwingine alikuwa akikaimu nafasi ya Kocha Mkuu.

Hakudumu kwa muda mrefu, aliingia mwaka 2017 na kuondoka 2018, lakini aliacha gumzo nchini kutokana na aina yake ya ufundishaji na ushangiliaji kiasi cha kupendwa si tu na wanachama na mashabiki wa Simba, bali hata wa Yanga.

Wanayanga wengi wanamkubali Masoud Juma, ndiyo maana hii inaweza kuwa fursa nzuri kwake kuwaaminisha kuwa hawajakosea kumchukua kama ikifanya hivyo.

Staili yake ya kuchezesha mabeki watatu nyuma, awali haikuzoeleka, lakini ilipozoeleka iliifanya Simba kuwa tishio na huenda akaileta kwenye klabu ya Yanga na ikiwaingia wachezaji inaweza kuleta kitu tofauti kwenye kikosi hicho.

**NJE YA UWANJA**

KIUNGO mchezeshaji wa Manchester City, Kevin De Bruyne, amesema kuwa mazingira ya mashabiki wa Liverpool wanavyokuwa kwenye Uwanja wa Anfield huwa "haimsumbui kichwa". Timu hizo zilitarajia kukutana jana katika mechi ya Ligi Kuu England.



Extra Time



MASSIMILIANO ALLEGRI

# VIATU VYA SOLSKJAER UTD VITAWATOSHA



POCHETTINO



ERIK TEN HAG

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imekuwa na mwanzo mbaya zaidi wa msimu huu. Ushindi wao dhidi ya Norwich na ushindi dhidi ya Chelsea kwenye Kombe la Carabao ulioonyesha kama vile timu hiyo imeamka, lakini kichapo kutoka kwa Bournemouth kikaonyesha kuwa bado kuna tatizo kubwa kwenye kikosi hicho.

**Hicho kilikuwa ni kichapo chao cha nne msimu huu na inaonyesha wazi kwamba, mbio zao za kutaka kumaliza kwenye nne bora kuonekana kuwa ngumu zaidi msimu huu.**

Matokeo hayo kwa kiasi kikubwa yameibua maswali mengi juu ya uwezo wa kocha, Ole Gunnar Solskjaer na wengi wanatabiri kwamba anaweza kufukuzwa wakati wowote.

Kama hilo litatokea, hapa tunawaangalia makocha wenye nafasi ya kuchukua mikoba yake pale United:

### 1. MASSIMILIANO ALLEGRI

Massimiliano Allegri amekuwa hana timu tangu aliopondoka Juventus kipindi cha majira ya joto kilichopita. Alikuwa na misimu mitano ya mafanikio makubwa pale Juventus ambapo alishinda mataji matano ya Ligi Kuu Italia, Serie A.

Pia aliiongoza Juventus kucheza fainali mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Timu anayoinoa Allegri mara zote inakuwa na nidhamu nzuri, kitu ambacho Manchester United wanaonekana kukikosa kwa sasa. Anaijenga timu yake kutoka nyuma na mara nyingi hataki iruhusu mabao. Timu yake inaweza isichezea vizuri kama United inavyocheza kihistoria, lakini ni mtu anayependa kupata matokeo.

Kumekuwa na ripoti kwamba, Allegri anajifunza lugha ya kiingereza kwa kuwa ana nia ya kufundisha timu moja nchini England. Amejithibitishia yeye mwenyewe kuwa mmoja wa makocha bora duniani wakati akiwa anazinoa Juventus na AC Milan.

Allegri atahitaji wachezaji wapya hasa kwenye safu ya ulinzi na kiungo ili kuiwezesha Manchester United kurudi kwenye ubora wake.

### 2. ERIK TEN HAG

Kocha Erik ten Hag alikuwa na msimu wa kuvutia na Ajax mwaka jana. Aliongoza timu yake kutwaa mataji mawili na kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo ilipoteza kwa Tottenham Hotspur.

Timu yake ya Ajax imeendelea kuwa na ubora ule ule wa msimu uliopita, ikiwa haijafungwa kwenye Ligi Kuu nchini Uholanzi. Kipigo pekee walichokipata msimu huu ilikuwa ni dhidi ya Chelsea kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ten Hag ameiongoza Ajax kuwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, msimu huu na wapo pointi sawa kileleni kwenye Kundi la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ten Hag ni mmoja wa makocha wenye umaarufu mkubwa Ulaya na hata mashabiki wa Manchester United wanamfahamu. Mara zote timu anayoiongoza huwa inacheza soka la kuvutia, na pia anajulikana kwa kupenda kuwaamini wachezaji vijana.

Kama akipewa nafasi ya kuinoa United, atakuwa na wakati mzuri zaidi wa kuiongoza timu hiyo kwenye mafanikio makubwa.

### 3. MAURICIO POCHETTINO

Mauricio Pochettino amekuwa akihusishwa na klabu kubwa kwa muda mrefu sasa, lakini malengo yake ya kutaka kushinda kitu fulani na Tottenham Hotspur kumefanya kuendelea kubakia pale jijini London.

Lakini sasa huku kukiwa na uvumi kwamba wachezaji nyota wa Tottenham wanataka kuondoka, kunaweza kumfanya Pochettino kuamua vinginevyo.

Pochettino pengine ndio anaweza kuonekana kuwa chaguo la haraka na rahisi zaidi kwa Manchester United. Amejithibitishia yeye mwenyewe kuwa na uwezo mkubwa katika soka la Uingereza, na msimu uliopita aliiwezesha Tottenham kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na amepata mafanikio hayo bila kuwa na kikosi chenye wachezaji wakubwa. Pale United, Pochettino anaweza kuwa na nafasi nzuri ya kusajili wachezaji anaowataka. Mara zote timu anayoinoa inakuwa imejipanga vizuri na yenye muunganiko.

Kumshawishi kuondoka pale Tottenham bado inaweza kuwa kazi ngumu na United inaweza kukabiliwa na upinzani mkubwa kutoka kwa klabu nyingine.

Kwani Pochettino amekuwa akihusishwa na mpango wa kuchukuliwa na Bayern Munich katika siku za hivi karibuni.

Hadi sasa kama United inahisi kwamba, Pochettino anaweza kuwa suluhisho kwao hawakosei, kwa sababu soka la Uingereza linamjua vizuri zaidi, hasa kwa kipindi alichokaa na miamba hao wa jiji la London.

## Nukuu

"Bayern Munich haitafanya uamuzi wa kumwajiri Mfaransa Arsene Wenger mpaka pale kocha huyo wa zamani wa Arsenal atakapopiga simu kwa mabosi wa katika klabu hiyo, ili kueleza nia yake ya kukubali nafasi hiyo ambayo iko wazi," **Karl-Heinz Rummenigge, Mwenyekiti wa vigogo hao wa Bundesliga, amesema.**



"Ni ndoto ya straika kinda wa klabu ya Paris Saint Germain na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe, kutua katika kikosi cha Real Madrid ya Hispania," **amesema Mfaransa Zinedine Zidane.**



"Mimi sio gwiji, wakati ninasajiliwa na klabu hii kamwe sikufikiria kama nitafikiri hatua hii, nina furaha kubwa, nitajaribu kuisaidia timu na vile vile kuwa kwenye ubora wangu, nataka kuendelea kuisaidia zaidi. Najisikia jasiri kama ninaweza kuwasaidia wachezaji wenzangu kwa kuzungumza, hii ni sehemu ya uzoefu wangu katika klabu," **alisema Karim Benzema baada ya kufikisha bao la 50 katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid.**





# KILIMANJARO QUEENS YASAKA REKODI CECAFA

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya kuwania ubingwa wa Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati kwa wanawake yamepangwa kufanyika kuanzia Jumamosi Novemba 16 hadi 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, jijini Dar es Salaam.

**Hii ni mara ya tatu, michuano hiyo inayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), kufanyika kwenye ukanda huu.**

Mara ya kwanza ilifanyika mwaka 2016 katika mji wa Jinja nchini Uganda na mwaka jana yalifanyika Kigali, Rwanda. Mara zote timu ya Tanzania Bara, maarufu Kilimanjaro Queens, ilifanikiwa kutwaa taji hilo.

Mashindano ya mwaka huu, yanatarajiwa kushirikisha nchi nane ambazo ni pamoja na wenyeji Kilimanjaro Queens, Zanzibar Queens, Sudan Kusini, Burundi, Uganda, Kenya, Ethiopia na Djibouti.

Katika kuonyesha kwamba, Cecafa, imejipanga kukuza kiwango cha soka kwenye ukanda wake, huu ni msimu wake mwingine wa kuwapa nafasi wachezaji wa soka wanawake kuonyesha uwezo wao.

Akizungumza na gazeti hili, Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Salum Madadi, amesema kuwa shirikisho hilo limejipanga vizuri kuhakikisha mashindano hayo yanafanyika katika kiwango cha juu kwa kutoa huduma zote muhimu zinazotakiwa kwa mujibu kwa kanuni na taratibu za michuano hiyo.

Madadi alisema kuwa TFF, inawakaribisha wageni wote na inawataka wakae Tanzania bila hofu ya aina yoyote na wanaamini kupitia michuano hiyo, bendera ya nchi itaendelea kupeperushwa vizuri.

"Maandalizi kwa ajili ya mashindano hayo yanaendelea vizuri, lengo letu ni kuhakikisha Tanzania inatetea ubingwa wa mashindano hayo, yaani tunataka kuona kombe libaki hapa nyumbani," alisema Madadi.

Alisema kuwa mbali na kukuza viwango vya wachezaji wa ukanda huu, pia michuano hiyo itatoa fursa kwa wafanyabiashara kupata kipato zaidi kutokana na kuuza bidhaa mbalimbali na vile vile kutangaza vivutio vya kitalii vilivyoko hapa nchini pamoja na tamaduni za Kitanzania.

"Mashindano ya Cecafa ni makubwa hapa nchini na katika ukanda wetu, ninaamini timu yetu ya wanawake itafanya vizuri kutokana na maandalizi ya muda mrefu tuliyowapa, kwa kuhakikisha kombe linabaki nyumbani," alisema Makamu wa Rais wa TFF, Athumani Nyamlani.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Chama cha Soka la Wanawake Tanzania (TWFA), Amina Karuma, alisema kuwa mashindano hayo yanatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa kutokana na timu zinazokutaja kushiriki kujipanga kuwavua ubingwa Kilimanjaro Queens, ambayo inashikilia rekodi ya kutwaa kombe hilo mara mbili mfululizo.

Karuma alisema kuwa, pamoja na kukiandaa vema kikosi chao, wachezaji wanahitaji kupata sapoti kutoka kwa mashabiki ili waweze kutimiza ndoto zao na kuipa heshima.

"Tunawaomba mashabiki wetu wasitutupe, waje kwa wingi uwanjani kuwashangilia wachezaji wetu katika mechi zote, kuanzia hatua ya awali hadi mwisho, tunaamini hatutawaangusha, tutafanya kile wanachokitarajia," Karuma alisema.

Kiongozi huyo amewataka wachezaji kutumia vizuri fursa hii kuonyesha viwango vyao, na kupitia kwa mawakala mbalimbali ambao watakuja kufuatilia mashindano hayo, watasajiliwa na baadaye watafaidika kiuchumi huku pia wakirejea kuisadia Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars).

"Naamini wachezaji wetu watafanya vizuri katika mashindano ya Cecafa kutokana na mazoezi pamoja na maandalizi ya muda mrefu tuliyowapa, vile vile tunaomba wadau mbalimbali wazidi kujitokeza kuiunga mkono timu yetu ili ifanye vizuri," Karuma alisema.

Alisema soka la wanawake kwa sasa limekua tofauti na ukilinganisha na miaka iliyopita vile vile anaishukuru TFF kwa uamuzi wake wa kusimama vema programu za soka la wanawake na huu ni wakati wa kuonyesha faida za kuilea timu hiyo.

Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime, aliliambia gazeti hili kuwa, kikosi chake kiko tayari kupambana katika mashindano hayo na wanaamini watawapa furaha Watanzania.

Shime alisema kuwa mashindano hayo ni magumu na kila mchezo kwao utakuwa ni sawa na fainali, kwa sababu wapinzani wote wataingia uwanjani wakifikiria kuivua ubingwa Kilimanjaro Queens.

"Ninashukuru Mungu sina majeruhi, kwa sasa maandalizi yetu yamefikia asilimia 95, tutaingia uwanjani kupambana kuanzia mchezo wa kwanza, lengo ni kuendelea kufanya vizuri katika mashindano haya," alisema kocha huyo.

Kilimanjaro Queens itafungua mashindano hayo Jumamosi kwa kuikaribisha Sudan Kusini, halafu itawavaa Zanzibar Queens na baadaye itakamilisha mechi za hatua ya makundi kwa kucheza dhidi ya Burundi.

## NAJUA WAJUA



KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, amesema kuwa klabu yake haina mpango wa kusajili mchezaji mpya katika kipindi cha dirisha dogo la Januari hata kama adhabu yao ya kufungiwa usajili itakuwa imemalizika.

SOKA




# MBEYA CITY, PRISONS HALI MBAYA SOKOINE

Na Nebart Msokwa, MBEYA

HUKU Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20 ikisimama kwa muda kupisha maandalizi ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), inayojiandaa na mechi mbili dhidi ya Equatorila Guinea na Libya, huu ni msimu wa pili na wa mwisho kwa ligi hiyo kushirikisha klabu 20.

**Hii ni baada ya kanuni zinazotumika kusimamia ligi hiyo ya juu nchini, kubadilishwa.**

Majiji ya Mbeya na Mwanza, ndiyo pekee yenye timu mbili zinazoshiriki ligi hiyo ukiacha Dar es Salaam ambao una timu zaidi ya mbili zikiwamo vigogo Simba, Yanga na Azam.

Mbeya ina timu za Mbeya City inayomilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Tanzania Prisons ambayo inamilikiwa na Jeshi la Magereza nchini. Kwa upande wa Mwanza, kuna timu za Mbao FC inayomilikiwa na wafanyabiashara wa Mbao katika Mji wa Ilemela na Alliance FC ambayo inamilikiwa na Shule ya Vipaji ya Alliance chini ya Mkurugenzi wake James Bwire.

Wakati wapenzi na mashabiki wa mpira mkoani Mbeya wakifurahia jiji lao kuwa na timu mbili zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, timu hizo zimeshindwa kuwapa raha mashabiki hao hasa katika mechi za nyumbani.

Ikiwa Ligi ikiwa imeingia katika mzunguko wa 11, timu hizo ambazo zote zinautumia Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine, zimeshindwa kuwa na mwendelezo mzuri wa matokeo ya ushindi hasa zikiwa katika uwanja wao wa nyumbani.

Timu hizo zimecheza jumla ya michezo saba katika Uwanja wa nyumbani ambapo Mbeya City wamecheza mechi nne na Tanzania Prisons Mechi tatu.

Kati ya mechi hizo ushindi ni mechi moja pekee ambao ulipatikana katika mzunguko wa pili kwa Tanzania Prisons kuichapa Ruvu Shooting mabao 2-1 Septemba 15. Vilevile katika michezo hiyo hiyo saba, timu hizo zilipata matokeo ya sare katika michezo michezo minne ukiwamo "dabi" yao, iliyochezwa Agosti 24, mwaka huu.

Aidha, timu hizo zimepoteza jumla ya michezo miwili ambayo yote ilipotezwa na timu ya Kizazi Kipya, Mbeya City ambayo ilifungwa goli 2-0 na Biashara United kutoka mkoani Mara na ikapoteza kwa goli 4-1 dhidi ya "Wanankulukumbi" Kagera Sugar kutoka mkoani Kagera.

Hivyo katika michezo saba ambayo timu hizo zimecheza zikiwa katika uwanja wao wa nyumbani, zimekusanya jumla ya alama saba ambazo ni wastani wa kupata alama moja katika kila mchezo.

Mbali na kukusanya alama hizo kiduchu, pia timu hizo zimeruhusu nyavu zao kutikiswa mara tisa ikiwa ni mabao manne zaidi ya ambayo timu hizo mbili zimepachika ambayo ni mabao matano.

Kati ya mabao tisa ambayo timu hizo zimeruhusu, Mbeya City ambayo ndiyo yenye mashabiki wengi, ndiyo iliyoruhusu mabao mengi ambapo imedunguliwa magoli saba sawa na michezo ambayo timu zote mbili zimecheza kwenye Uwanja wa Sokoine.

Tanzania Prisons imeruhusu nyavu zao kutikiswa mara mbili pekee ambapo mchezo mmoja ilitoka sare ya 1-1 na Kagera na bao lingine ilikuwa katika mechi ya ushindi wa 2-1 dhidi ya Ruvu Shooting.

Mechi zilizoonyesha kuwakera zaidi mashabiki wa timu hizo mbili ambazo Mbeya City ilizipoteza kwa mabao 4-1 dhidi ya Kagera Sugar ambacho kilikuwa ni kipigo cha kwanza kwa ukubwa tangu msimu huu ulipoanza.

Siku ambayo timu hiyo iliambulia kipigo hicho, mashabiki wake walionekana kujawa na gadhabu pale walipoanza kutoka uwanjani mapema, huku wakimshambulia kwa maneno makali Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mwambusi.

Kipigo hicho kilikuwa cha pili mfululizo kwa timu hiyo katika uwanja wa nyumbani baada ya kile cha 2-0 dhidi ya timu iliyokuwa kibonde kwa wakati huo, Biashara United ambayo ilikuwa imecheza michezo minne na kuambulia vichapo vitatu, sare moja na ilikuwa inaburuza mkia kwenye msimamo.

Pamoja na timu hizo kuwa vibonde zikiwa nyumbani lakini zimeonyesha angalau kuwa miamba zinapokuwa kwenye viwanja vya ugenini ambapo zimecheza michezo 12 na kukusanya alama 19 ambazo Tanzania Prisons imekusanya 13 na City alama sita.

Kwenye michezo hiyo Tanzania Prisons ambayo ni timu pekee katika Ligi iliyofika mzunguko wa 10 bila kupoteza imepata ushindi katika michezo mitatu ya ugenini na sare nne hivyo kukusanya alama 13 ugenini tofauti na City ambayo imeshinda mchezo mmoja na kuambulia sare michezo mitatu hivyo kukusanya alama sita.

Katika michezo hiyo 12 timu hizo zimefumania nyavu za wapinzani wake mara 15, ambapo Mbeya City imefumania mara tano huku kaka zao Tanzania Prison wakizifumania mara 10.

Vile vile timu hizo zimefungwa mabao 14 zikiwa ugenini katika michezo hiyo 12 ikiwa ni tofauti ya goli moja na magoli ambayo zimefunga zikiwa ugenini.

Kati ya mabao 14 ambayo timu hizo zimefungwa zikiwa ugenini Mbeya City imefungwa mabao nane na Tanzania Prisons mabao sita.

Mpaka kufikia mzunguko wa 10 Tanzania Prisons ilikuwa imeshika nafasi ya pili kwenye msimamo ikiwa na alama 18 nyuma ya vinara Simba ambao wana alama 21 huku City ikichechemea katika nafasi ya 17 ikiwa na alama nane.

FRANK Lampard amefanikiwa kutwaa tuzo ya Kocha Bora wa Mwezi wa Ligi Kuu England baada ya kikosi chake cha Chelsea kuonyesha kiwango kizuri katika kipindi chote cha Oktoba. Katika mwezi huo Chelsea walipata ushindi dhidi ya Burnley, Southampton na Newcastle.




NDANI YA 18

KLABU ya Manchester United imekuwa na mwanzo mbaya zaidi wa msimu huu. Ushindi wao dhidi ya Norwich na ushindi dhidi ya Chelsea kwenye Kombe la Carabao ulioonyesha kama vile timu hiyo imeamka, lakini kichapo kutoka kwa Bournemouth kikaonyesha kuwa bado kuna tatizo kubwa kwenye kikosi hicho.

Uk. 16&17

# WAAFRIKA WANAOTISHA UWANJANI KWA SASA




AUBAMEYANG

**LONDON,** England

WAKATI ukifikiria wachezaji wakubwa wa Afrika katika soka la dunia, majina ya magwiji kadhaa yanakujia kichwani. Didier Drogba, Samuel Eto'o na George Weah, ni miongoni mwa wachache.

**Katika soka la kisasa, wachezaji kutoka Bara la Afrika wanaofanya vizuri kama sio bora kuliko wale wa Ulaya na Amerika Kusini.**

Katika wachezaji hao, wapo Mohamed Salah na Pierre-Emerick Aubameyang, ni miongoni mwa wachezaji wanaofanya vizuri zaidi kwa sasa duniani.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano kutoka Afrika ambao wanatisha kwa sasa duniani.

Ijulikane kuwa, hapa hatuwaangalia wachezaji ambao wana asili ya Afrika na wanazichezea nchi nyingine kwenye timu ya taifa kama N'Golo Kante.

**5. THOMAS PARTEY - ATLETICO MADRID, GHANA**

Alizaliwa Krobo Odumase mashariki mwa Ghana, na kwa sasa Thomas Partey anasimama kama kiungo muhimu zaidi kwa kikosi cha Atletico Madrid. Alisaini mkataba wake na miamba hao wa Hispania mwaka 2011.

Kwa sasa Partey ana umri wa miaka 26 na ni mmoja wachezaji viungo wakabaji.

**4. KALIDOU KOULIBALY - NAPOLI, SENEGAL**

Akiwa amepata tuzo ya beki bora kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, msimu wa 2018-19, Kalidou Koulibaly ni mmoja wa walinzi bora zaidi duniani na kwa urahisi tu bora kwa Bara la Afrika kwa sasa. Akiwa anaichezea klabu ya Napoli, Koulibaly amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa mabeki bora kabisa duniani.

Msimu uliopita, mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal alicheza zaidi ya dakika 4,300 kwenye ngazi ya klabu.

Koulibaly kwa sasa ana umri wa miaka 28, lakini anaonekana kuwa ni mmoja wa walinzi bora zaidi kuwahi kutokea Bara la Afrika.

**3. PIERRE-EMERICK AUBAMEYANG - ARSENAL FC, GABON**

Ingawa anashika nafasi ya tatu kwenye orodha hii, lakini hakuna shaka kwamba, Pierre-Emerick Aubameyang ni mmoja wa wachezaji wenye kiwango mwendelezo kwa kipindi kirefu.

Nahodha huyu wa timu ya taifa ya Gabon, Aubameyang alianza kijithibitishia ubora wake kule kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, akiwa na klabu ya Borussia Dortmund kabla ya kuhamia kwenye Ligi Kuu England, ambako amekuwa mchezaji bora zaidi pale Arsenal.

Mchezaji huyu bora wa zamani wa Afrika, ni mmoja washambuliaji bora zaidi duniani kwa sasa, akiwa ameshinda kiatu cha dhahabu kule Bundesliga na Ligi England msimu uliopita.

Kwa sasa Aubameyang ana umri wa miaka 30, lakini bado anaonekana kuwa kwenye ubora wake.

2 Sadio Mane - Liverpool FC, Senegal

Kwa namna anavyocheza kwa sasa Sadio Mane amejipambanua mwenyewe kama mmoja wa wachezaji bora kabisa duniani. Mane sio tu amekuwa bora kwenye Ligi Kuu England, lakini pia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwani alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa Liverpool walioiwezesha kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa msimu uliopita. Pia alikuwa mshindi wa tuzo ya kiatu cha dhahabu kwa kufunga mabo mengi msimu uliopita.

**1 MOHAMED SALAH - LIVERPOOL FC, MISRI**

Nani anaweza kuwa kama yeye? Pengine Sadio Mane, lakini Mohamed Salah raia wa Misri amekuwa kwenye ubora wa juu zaidi.

Msimu uliopita alishinda kiatu cha dahabu kwa ufungaji wa mabao mengi kwenye Ligi Kuu England.

Na pia alikuwa nguzo muhimu zaidi kwa kikosi cha Liverpool kilichotwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Hawa ni heshima kuwataja:
Riyad Mahrez - Manchester City
Wilfred Ndidi - Leicester City

**USILOLIJUA**



KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema kuwa anaweza kusajili nyota "wawili wapya" katika kipindi cha dirisha la Januari, lakini mchakato mkubwa wa usajili ataufanyanya kwenye kipindi cha majira ya joto mwakani.





# Zimamoto waonywa kuhusu rushwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMISHNA Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini, Thobias Andengenye, amewatahadharisha askari wa jeshi hilo kuepuka kushiriki vitendo vya rushwa, huku akisema atakayepatikana atashughulikiwa bila kujali kiwango cha rushwa atakayopokea.

Kamishna Andegenye alitoa tahadhari hiyo mwishoni mwa wiki jijini Mbeya alipokuwa anazungumza na askari wa jeshi hilo, Kituo cha Mbeya alipofanya ziara ya kukagua utendaji kazi pamoja na vitendea kazi ambapo alisema rushwa haivumiliki ndani ya jeshi.

Aliwataka askari hao kuwa waadilifu na waaminifu katika kuwatumikia wananchi hasa wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao ya kila siku ikiwemo ya kuzima moto na kufanya uokoaji pale yanapotokea majanga.

"Tutamwadhibu kwa kile kitendo alichofanya cha kupokea rushwa na sio kiwango cha rushwa, hivyo askari asije akajidanganya kuwa akipokea Sh. 1000 hatutamshughulikia, tutamkamata, tutamfukuza kazi na tutamfunga," alisema Kamishna Andengenye.

Alisema jueshi hilo linakabiliwa na changamoto ya uhaba wa askari, lakini ni bora likabaki nao wachache ambao ni waadilifu kuliko likawa nao wengi ambao ni wala rushwa.

Alisisitiza kuwa kwa sasa wanaendelea kuchukua hatua dhidi ya wote wanaobainika kushiriki vitendo vya rushwa kwa sababu rushwa inasababishwa mwenye haki akikose haki yake na wengine kupata haki wasiyoistahili.

Katika hatua nyingine alisema jeshi hilo limeanza kujenga vituo katika wilaya ambazo bado hazina vituo hivyo pamoja na kununua vitendea kazi ili kurahisha utendaji kazi hasa kwenye kukabiliana na majanga.

Alisema katika Mkoa wa Mbeya zimebaki wilaya mbili pekee ambazo ni Chunya na Kyela hazina vituo hivyo na ni miongoni mwa maeneo ambayo yanalengwa kwenye mpango wa kujenga vituo vipya. "Kutokana na uhaba wa watumishi na vitendea kazi, tutavitumia vituo hivyo kwa ajili ya kutoa elimu ya kukabiliana na majanga kwa wananchi na kadri tutakavyokuwa tunapata fedha tutapeleka vifaa ili zifanye kazi ya kuzima moto na kuokoa," alisema Andengenye.

Alisema serikali imetenga bajeti kwa ajili ya kununua magari ya zimamoto pamoja na kufufua yaliyoharibika ili kuongeza ufanisi wa jeshi hilo.

Pia aliwaonya baadhi ya wananchi ambao wanatumia vibaya simu ya dharura ya jeshi hilo kwa kupiga simu wakieleza kuwa kuna matukio ya moto kumbe sio kweli. Alisema vitendo hivyo vinalisababishia jeshi hilo hasara kwa kutumia raslimali nyingi kwenda kukabili matukio ambayo hayapo na kwamba vinaweza pia kusababisha kushindwa kuyakabili matukio ya kweli kutokana na rasilimali.

Kamishna Andengenye alisema jeshi hilo litaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi ya simu ya dharura pamoja na namna ya kukabiliana na majanga.



Mafundi wakiendelea kuweka alama za pundamilia kuashiria vivuko vya watembea kwa miguu katika moja ya barabara za Jiji la Mbeya eneo la Sokoine ili kupunguza matukio ya watu kugongwa na magari. **PICHA NA NEBART MSOKWA.**

# Mil. 45/- kuondoa tope Mto Mbarali

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI inakusudia kutumia zaidi ya Sh. milioni 45 kuondoa tope na mchanga kwenye Mto Mbarali ili kuuwezesha mto huo kutiririsha maji katika mkondo wake badala ya kusambaa kwenye makazi ya watu.

Mto huo ambao unatiririsha maji yake katika Mto Ruaha Mkuu umejaa mchanga na tope kwa umbali wa zaidi ya kilomita saba katika Kijiji cha Ibohola kutokana na baadhi ya wananchi kufanya shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo kwenye kingo za mto huo.

Inadaiwa kuwa uharibifu huo wa mkondo wa mto unaweza ukasababisha maji kujaa na kusambaa kwenye makazi na hivyo kuhatarisha maisha ya wananchi na mali zao hasa kipindi cha mvua. Ofisa Maji wa Bonde la Mto Rufiji, Idrisa Msuya, alisema fedha hizo zimetolewa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na kwamba kazi hiyo ya kuanza kusafisha mkondo wa mto huo inatarajiwa kuanza mara moja ili kuuwahi msimu wa mvua.

Alisema wananchi hao walikuwa wanalalamika kwa muda mrefu wakiomba serikali iwasaidie kuepukana na hatari hiyo lakini bajeti ilikuwa hairuhusu lakini sasa fedha zimeshapatikana.

"Mto huu ni miongoni mwa mito inayotiririsha maji mwaka mzima, lakini kutokana na kujaa kwa mchanga na tope, kipindi cha kiangazi maji huwa yakifika katika eneo hilo hayawezi kuendelea tena na hivyo kusababisha vijiji vya upande wa chini kukosa maji," alisema Msuya.

Aliwataka wananchi wa vijiji vyote vilivyopo pembezoni mwa mito kuacha kufanya shughuli za kilimo ndani ya mita 60 kutoka kwenye kingo za mito kwa madai kuwa madhara yake ni makubwa.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watumiaji Maji wa Mto Mbarali, Ally Makwetta, alisema baada ya mto huo kujaa mchanga maji yamepoteza mwelekeo na kusambaa hivyo katika maeneo tofauti hasa katika Kijiji hicho cha Ibohola.

Alisema mbali na kijiji hicho cha Ibohola pia kijiji cha Warumba ambacho kipo upande wa chini kina hatari zaidi endapo mto huo hautarekebishwa kwa madai kuwa yanaweza yakatokea maafa wakati wa mvua za masika.

Aliipongeza serikali kwa hatua ambazo imeanza kuzichukua kwa maelezo kuwa ni moja ya hatua ambazo zinaonyesha kujali wananchi wanaoishi maeneo ya vijijini.

"Dalili za mvua ya mwaka huu sio nzuri, imenyesha kidogo tu lakini kila kona ya nchi kulikuwa na maafa, sasa endapo huu mto hautasafishwa mapema, serikali inaweza ikaingia hasara kubwa endapo maafa yatatokea, watu wanaweza wakapoteza maisha na mali," alisema Makwetta.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Asheri Mwakimonga, aliwataka watendaji wa vijiji na kata kushirikiana na watendaji wa jumuiya za watumiaji maji kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwenye kingo za mto ili kudhibiti uharibifu wa mazingira.

Alisema ili kukomesha vitendo vya uharibifu huo wa mazingira hatua za kisheria zinatakiwa kuchukuliwa dhidi ya wote watakaobainika kufanya shughuli za kibinadamu kwenye kingo za mto.

## Vijana watakiwa mafunzo Mgambo

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Mhandisi Maryprisca Mahundi, amewataka vijana wilayani humo kushiriki mafunzo ya Mgambo bila kujali viwango vya elimu zao ili kujiongezea maarifa na uzalendo kwa taifa lao.

Alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki alipokuwa anafunga mafunzo ya jeshi hilo yaliyofanyika katika Kata ya Chalangwa wilayani humo na kushirikisha vijana 153 wakiwemo wanawake nane ambapo alisema baadhi ya vijana wamekuwa wakibeza mafunzo hayo.

Alisema baadhi huwa wanayabeza wakidai kuwa ni mafunzo yanayowafaa watu ambao hawajasoma na baadhi wakidai kushiriki ni kupoteza muda, hivyo akawataka wote wenye afya za kuweza kushiriki washiriki.

Alisema mafunzo hayo yanafanyika kila mwaka wilayani humo na katika Kata tofauti ili kuhakikisha vijana wote wanashiriki kikamilifu na kwamba kwenye mafunzo hayo vijana wanajifunza mambo mengi ikiwamo ukakamavu, uzalishaji na uzalendo.

"Kuna watu huwa wanadharau sana mafunzo haya na baadhi wanayaita mafunzo ya mgambo, nawataka wajuwe kabisa kuwa hili ni jeshi maana vitu wanavyofundishwa hapa sio tofauti na majeshi mengine, ndio maana linaitwa Jeshi la Akiba," alisema Mahundi.

Aidha, aliwapongeza wanawake waliojitokeza kwenye mafunzo hayo na kushiriki mpaka mwisho ambapo alisema wameonyesha uwezo mkubwa ambao unastahili kuigwa na wengine ambao hawakujitokeza na kwamba hamasa itolewe pia katika kata zitakazofuata.

Mshauri wa Mgambo wa Wilaya ya Chunya, Stafu Sajent Uswege Mwasasumbe, alisema mafunzo hayo yamefanyika kwa muda wa miezi minne na wiki moja ambapo vijana hao wamefundishwa mambo tofauti tofauti.

Alisema wakati mafunzo hayo yanaanza washiriki walikuwa 156, lakini waliovumilia mpaka mwisho ni 153 na kwamba ni washiriki watatu pekee ambao walitoroka kutokana na sababu ambazo hazijulikani.

Mwasasumbe alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa taifa kwa madai kuwa yanawafanya vijana kuwa walinzi wa jamii inayowazunguka pamoja na kuwafanya washiriki vema kwenye shughuli za uzalishaji hasa katika kipindi hiki ambacho taifa linaingia kwenye uchumi wa viwanda.

"Tunashukuru mafunzo haya yamefanyika vizuri na hatujapata tatizo lolote la kiafya kwa vijana wetu ukiacha yale madogo madogo ambayo huwa ni lazima yatokee, tunawashauri wahitimu kwenda kuwa mabalozi wazuri kwenye maeneo yao," alisema Staff Sajenti Mwasasumbe.





# Serikali yaagiza kutolewa vibali vya usajili wa Azaki

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameiagiza mikoa na halmashauri zote nchini kuhakikisha zinatoa vibali vya usajili kwa asasi za kiraia (AZAKI) ili ziende kufanya kazi za kuleta maendeleo.

Aidha, amemwagiza Katibu Mkuu wa Tamisemi kuhakikisha anasimamia utoaji wa vibali vya usajili wa Asasi za kiraia kwa ukaribu ili ziweze kufanikiwa.

Pia, Jafo amezitaka asasi za kiraia kwenda kulisemea mambo mazuri taifa lao hususani maendeleo yanayotekelezwa ili wananchi wajue jitihada za maendeleo zinazofanywa na serikali.

Akizungumza wakati wa kufungua kongamano la azaki, Jafo alisema hataki kuona malalamiko yoyote kuhusiana na kukwama kwa vibali vya usajili.

"Ninachotaka kusikia ni Asasi zimepewa vibali ili mradi tu vina sera na mwongozo inayohitajika ndani ya serikali.

Alisema azaki ni moja ya chachu ya kufichua matatizo ambayo hivi sasa yote yamefanyiwa kazi na serikali.

"Nakuagiza Katibu Mkuu katika ofisi yangu hakikisha vibali vinatolewa bila vikwazo kwa Asasi hizo, ili mradi ina manufaa kwa taifa na jamii kwa ujumla, na pia iwe na sera zinazoeleweka katika kuchagiza maendeleo," alisema Jafo.

Alisema maendeleo mengi yanayofanywa na serikali , yametokana na mchango wa azaki wa kuibua changamoto zilizopo katika sekta mbalimbali nchini, hivyo zinastahili kupongezwa na kusikilizwa.

"Naomba niwapongeze sana azaki, mmekuwa mkiibua matatizo yaliyopo sehemu tofauti, kwa mfano Hakielimu na tangazo lao la shule mbovu...yamesaidia serikali imeona na kuwekeza fedha nyingi katika sekta ya elimu kwa ajili ya kuziboresha na kufanya ujenzi," alisema.

"Katika sekta ya afya pia, barabara kote mmekuwa mkipasemea na hivi sasa serikali inayafanyia kazi yote, na matokeo yanaonekana katika sekta hizo zilivyoimarika."

Kutokana na hilo, alisema hakuna maendeleo ya mtu mmoja, maendeleo hufanywa na watu wote bila kuangalia itikadi ya mtu.

Kadhalika, aliziagiza asasi za kiraia kuhakikisha zinasaidiana katika kuwezeshana na kurekebishana badala ya kusemeana vibaya ili asasi nyingine zife, jambo ambalo alisema halikubaliki.

Naye Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi, Humphrey Polepole, alisema azaki na serikali ni kitu kimoja, hivyo haina haja ya kuogopana kama kuna suala lolote la wanapaswa kukutana ili kulipatia ufumbuzi.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa, Dk. Charles Msonde, akizungumza na waandishi wa habari jijini Mbeya jana, juu ya maandalizi ya mtihani wa taifa wa kidato cha pili unaonza leo kote nchini, kushoto ni Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Mariamu Mtunguja, kulia ni Katibu Tawala Elimu Mkoa, Paulina Ndigeza. **PICHA: KENETH NGELESI**

# Kasi ya ndoa za utotoni Afrika yatisha

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JUMLA ya watoto wa kike milioni 15, wenye umri chini ya miaka 18 huolewa kila mwaka katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, imeelezwa.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la HakiElimu, John Kalaghe, katika mdahalo uliohusu haki za mtoto wa kike uliofanyika jijini hapa.

Kalaghe alisema idadi hiyo ni kubwa sana, hivyo inapaswa kupigiwa kelele kwa sauti moja kutoka kwa jamii ili kutokomeza kabisa hali hiyo.

"Watoto wa kike wanahitaji kupata haki zao za msingi kutoka katika jamii inayotuzunguka, mkiwaozesha mapema wanashindwa kutimiza ndogo zao," alisema Kalaghe. Alisema kinachotakiwa sasa kila mmoja kuwa askari wa mtoto wa kike kwa ajili ya kuwalinda ili kuhakikisha wanapata haki ya msingi ikiwamo elimu kama ilivyo kwa watoto wengine wa kiume.

Aliwataka wazazi kuacha tabia ya kukubali kuwaoza watoto katika umri usio stahili badala yake wawaache wasome ili waweze kutimiza ndoto zao waliojiwekea.

Kwa upande wa mimba za utotoni, alisema milioni moja kila mwaka hutokea kwa watoto ambao hawajafikia umri wa miaka 15, kitu ambacho hakikubaliki kwa sababu mtoto anakwenda kupata mtoto mwenzie, hivyo kisababisha ugumu katika malezi.

Katika hatua nyingine, alisema asilimia 11 ya watoto duniani kote sawa milioni 168, wanatumikishwa kazi majumbani badala ya kwenda shule ni kusoma.

Kalaghe alisema wazazi wanapaswa kuacha tabia ya kuwatumikisha watoto, badala yake wawapeleke shule kutokana na elimu hivi sasa kutolewa bila malipo. Naye Mwanaharakati wa masuala ya haki ya mwanamke na mtoto, Marry Ndalo, amesema kinamama ndio walezi wakubwa wa mabinti, hivyo kama mama katika familia akisimama imara mtoto wakike hawezi kuyumba.

Alisema ni vema wazazi kuwa mstari wa mbele kuwaangalia watoto wa kike kwa ajili ya maisha yao ya baadaye katika suala zima la elimu.

# Mazao ya kijani kuundiwa kitengo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchini (TPA), wamekubaliana kuanzisha kitengo cha ukanda wa mazao ya kijani kwa ajili ya kusafirisha mazao ili kuepuka kukaa muda mrefu bandarini na kusababisha baadhi kuharibika kabla ya kusafirishwa.

Aidha, serikali imekubaliana na TPA kuanzisha kitengo maalum ambacho kitawajumuisha TRA, TPA ili kusimamia na kutatua changamoto kwa haraka inayokwamisha ucheleweshaji wa kusafirisha mazao.

Hayo yalibainishwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, wakati wa mkutano ulioihusisha Wizara za Kilimo, Viwanda, Fedha na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, bajeti na TPA uliofanyika jijini hapa kwa lengo la kuangalia namna ya kutatua matatizo yanayowakabili wakulima wa mboga, matunda na maua.

Bashe alisema lengo la kuanzisha kiwanda cha mazao ya kijani ni kutaka kuepusha mazao ya mboga kukaa bandari ni kwa muda mrefu kabla ya kusafirishwa kwenda nje kuuzwa.

"Tumeamua kuanzisha vitengo hivyo ili kuondoa matatizo yanaokabili sekta hiyo ndogo ya kilimo na hii itasaidia kuepusha kuchanganya kontena za parachichi ambazo haziwezi kukaa muda mrefu kama ilivyo za kopa ambazo zikikaa muda mrefu haziwezi kuharibika," alisema Bashe.

Alisema kontena za mazao ya mbogamboga zikikaa kwa muda zinaharibika na kumsababishia hasara mkulima na mfanyabiashara.

Naye Ofisa Mkuu wa Utafiti wa Masoko wa TPA, Lydya Malya, alisema katika kikao cha awali na watu wenye meli, walikubaliana wawekeze vifaa vya kuhifadhia shehena ya mboga, maua na matunda.

Malya alisema katika kikao hiko pia watu wa meli waliombwa kuwekeza vifaa vya kuhudumia shehena za matunda, mboga na maua ambavyo vitaepusha kuharibika kwa bidhaa hizo wakati zikiwa bandarini.



## HABARI ZANZIBAR

# Serikali kusimamia soko kilimo hai

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Dk. Makame Ali Ussi, amesema serikali itahakikisha inalisimamia soko la kilimo hai na kuwajengea uwezo wakulima.

Aliyasema hayo katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Omar Ali Ameir, katika ufunguzi wa soko la wazi la kilimo hai katika bustani ya Forodhani mjini Unguja.

Alisema, Zanzibar ina fursa kubwa ya kuingia katika soko la kilimo hai duniani kwa bidhaa za matunda, mboga na viungo kwa ajili ya kukuza uchumi.

Alisema sekta ya kilimo hai inakua kwa kasi duniani kutokana na utafiti uliofanywa mwaka 2015 kuonyesha soko la kilimo hicho lina thamani ya Dola za Marekani 81.6 bilioni na mboga na matunda ndilo linalobeba sehemu kubwa.

Pia alisema nchi zaidi ya 179 zinashiriki katika shughuli za kilimo hai, huku watu zaidi ya milioni mbili wanajishughulisha na kilimo hicho.

Alisema mbali na fursa za soko duniani, kilimo hai kina faida kubwa kwa afya za binadamu pamoja na kutunza na kurekebisha mazingira yaliyoharibika kutokana na matumizi mabaya ya ardhi.

"Serikali inafahamu kuwa bidhaa za kilimo hiki ndio bora kwa afya ya mtumiaji, lakini sekta hii bado inakabiliwa na changamoto ikiwamo ya utekelezaji wa sera ya kilimo hai, inayotokana na usimamizi wa kilimo hasa kwa wakulima kukosa elimu na msimamo wa kutumia njia madhubuti za udhibiti wa mazao," alisema.

Alieleza changamoto nyingine ni ukosefu wa dawa asilia kwa wakulima, hali ambayo inachangia kuongeza changamoto kwa wakulima.

Aliwaomba wakulima kujikita katika kilimo hicho kwa faida za wananchi na uchumi wa nchi.

Aliwapongeza wadau wa kilimo na Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation kwa uamuzi wa kuhamasisha wakulima, kulima kilimo hai.

Naye Mkuu wa miradi kutoka Milele Zanzibar Foundation, Khadija Sharif, alisema lengo ni kuwawezesha wanawake na vijana kukuza kipato chao na kumudu maisha yao kupitia kilimo hicho.

Alisema, wanaangalia kilimo cha mwani na mboga kwa ajili ya kukuza soko la ndani na nje ya nchi, lakini zaidi wanajikita katika kilimo hai ili kusaidia maendeleo endelevu.

Kwa upande wake, ofisa kilimo hai kutoka Jumuiya ya Wakulima wa Matunda na Mboga (UWAMWITA), Khamis Issa Mohammed, alisema kilimo hai ndio pekee kinachoweza kuongeza kipato kwa kuwa wakulima wengi wanaolima kwa kutumia mbolea za kemikali bidhaa zao zinakosa viwango.



Meneja Rasilimali Watu wa Kampuni ya Kioo Limited, Jacob Msuya, akimkabidhi cheti mmoja wa wahitimu katika Chuo cha Ufundi Stadi Veta, Kanda ya Dar es Salaam, kwenye mahafali yaliyofanyika mwishoni mwa wiki chuoni hapo jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi watakiwa kujenga utamaduni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amewataka wananchi wa kisiwa cha Uzi Ng'ambwa, kujenga utamaduni wa kujitolea na kushirikiana kwa pamoja katika shughuli za ujenzi wa taifa wa barabara iliyoanza Kijiji cha Unguja hadi katika kisiwa hicho huku serikali ikiendelea na azma yake ya kujenga daraja la kisasa.

Ayoub alieleza hayo baada ya kushiriki kazi ya ujenzi wa taifa wa upangaji mawe katika barabara hiyo na kukabidhi mifuko ya saruji 20, magari mawili ya mawe na nyundo ili kuunga mkono juhudi za wananchi katika kufanikisha ujenzi huo.

Alisema suala la kujitolea katika ujenzi wa taifa ni hatua ya msingi kujiletea maendeleo na kukuza uchumi na kuahidi kuwa serikali ya mkoa huo itaendelea kuunga mkono nguvu za wananchi kuondoa changamoto zinazowakabili.

"Naomba tuwe na utaratibu huu wa kujitolea katika shughuli hizi za kijamii na mimi kwa upande wa serikali ya mkoa tutaendelea kuunga mkono juhudi hizi mnazozichukua endeleeni kuwa wamoja katika kujiletea maendeleo," alisema Ayoub.

Alieleza kuwa utaratibu uliofanywa na wananchi hao wa kujitolea katika ujenzi wa taifa, ndio ulikuwa ukitumika kwa viongozi wa serikali ya awamu ya kwanza chini ya usimamizi wa marehemu mzee Abedi Amani Karume kwa kujenga majengo mbalimbali ya maendeleo.

Hata hivyo, aliwataka wananchi wa kisiwa hicho kuondoa tafauti zao za kisiasa na kuhakikisha wanakuwa na ushirikiano ili kuona ujenzi huo unafanikiwa kama ulivyokusudiwa.

Kwa upande wao wananchi wa kisiwa hicho waliiomba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kusaidia ujenzi wa barabara hiyo ili kuondokana na usumbufu wanaoupata hivi sasa wa kutopitika vizuri kutokana na kiwango cha ujenzi wake.

Walisema, awali barabara hiyo ilipata msaada wa ujenzi kwa kiwango cha zege kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ikiwa kama utafiti kwa kipande cha zaidi ya mita 300 na kudumu zaidi ya miaka mitatu.

Kisiwa cha Uzi Ng'ambwa kimezungukwa na bahari na kufanya wananchi wake wanapohitaji huduma mbalimbali za kijamii kuvuka ng'ambo nyingine.

# Rais Shein asifu ushirikiano mihimili mitatu

**Na Rahma Suleiman**,
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema Zanzibar imefanikiwa kupiga hatua kubwa ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kutokana na ushirikiano wa mihimili yake mikuu mitatu ambayo ni Serikali, Mahakama na Baraza la Wawakilishi.

Dk. Shein alisema hayo wakati alipokutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu, Jaji Sylvain Ore, aliyefika Ikulu akiwa na ujumbe wa majaji wa mahakama hiyo.

Alisema mafanikio hayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuimarika kwa amani na utulivu kutokana na mihimili hiyo mitatu kushirikiana katika kuendesha nchi na ustawi wake.

Alisema mihimili hiyo inafanya kazi zake bila kuingiliana kunakoweza kuathiri utendaji wa kazi katika kuwatumikia wananchi kupata maendeleo.

"Tunajivunia amani na utulivu wa nchi ambayo ni matokeo ya ushirikiano ya mihimili mitatu kufanya kazi zao pamoja," alisema.

Alisema katika suala la haki za binadamu na utawala bora, Zanzibar imepiga hatua kubwa na suala hilo limetajwa katika katiba yake.

"Mafanikio yote tunayopata ya kiuchumi na kisiasa ni matokeo ya kuzingatia haki za binadamu na utawala bora katika kuendesha nchi," alisema.

Naye Rais wa Mahakama hiyo, Jaji Ore, alimpongeza Dk. Shein kwa juhudi zake za kuimarisha amani na utulivu kwa wananchi wa Zanzibar na kuwapo mafanikio makubwa.

Alisema Zanzibar imekuwa eneo moja lenye utulivu wa kisiasa na kutoa fursa kubwa kwa taasisi na mashirika mbalimbali ya kimataifa kufanya mikutano yake. Jaji Ore lisema mafanikio yote hayo ni matokeo ya kuimarika kwa utawala wa katiba na sheria unaozingatia haki za binadamu.

"Mahakama ya Afrika ya haki za binadamu imeamua kufanya mkutano wake Zanzibar kutokana na kuvutiwa na mazingira yaliopo ya amani na utulivu wa kisiasa," alisema.

Vile vile, mahakama hiyo yenye makao makuu yake Arusha, miongoni mwa majukumu yake ni kuhakikisha inatekeleza matakwa ya Umoja wa Afrika (AU).

# Waganga wafawidhi kusakwa tuhuma za wizi mali ya umma

**Na Gurian Adolf,** KAKAMBO

BARAZA la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Kakambo mkoani Rukwa, limemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo na Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwakamata waganga wafawidhi wa Zahanati ya Kijiji cha Kantalemwa na ya Kijiji cha Ilango kwa tuhuma za wizi wa mali ya umma.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na baraza hilo, baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa Diwani wa Kilesha, Benard Maskini na Diwani wa Mnamba, Jimson Chilulumo.

Diwani Maskini alilalamikia kitendo cha Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Kijiji cha Ilango, Denis Mapori, kuwalaghai wajumbe wa kamati ya ujenzi wa nyumba ya kuishi mganga wa zahanati hiyo, hivyo kukubali kusaini muhtasari, kisha yeye kwenda benki na kutoa Sh. milioni 24 na kukimbia nazo kusikojulikana.

Alisema nyumba hiyo iliyojengwa kufikia kwenye lenta, imesimama ujenzi wake tangu mwaka 2010, na baada ya mganga aliyekuwapo alikimbia na fedha za ujenzi ambazo alizitoa benki kwa madai kuwa anakwenda kumlipa mkandarasi ili amalizie ujenzi wa nyumba hiyo.

Diwani huyo alisema kutokana na zahanati hiyo kukosa mganga kwa kuwa aliyekuwapo alikimbia na fedha, wananchi wamekosa huduma kwa muda mrefu, hali inayowalazimu kutembea umbali mrefu kufuata huduma katika vijiji vingine.

Naye Diwani Chilulumo alilalamikia kitendo cha Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Kantalemwa, Faraja Sanga, kung'oa sola iliyokuwa inatumika katika zahanati hiyo na kwenda kuifunga katika kilabu chake cha pombe ili wateja wapate mwanga.

Alisema sola hiyo ilipatikana baada ya wananchi wa kijiji hicho kuchangishana fedha na kuinunua ili isaidie kupata mwanga katika zahanati yao wakati wahudumu wa afya wanapotoa huduma nyakati za usiku, lakini mganga wa zahanati hiyo aliamua kuchukua na kuipeleka kwenye kilabu chake cha pombe.

Kutokana na hali hiyo, alisema wananchi hasa wakina wajawazito wamekuwa wakikabiliwa na wakati mgumu wanapokwenda kujifungua nyakati za usiku, ambapo hulazimika kubeba koroboi kutokana na kukosekana mwanga katika zahanati hiyo.

Alifafanua kuwa taarifa za vitendo hivyo zimekwishafikia ofisi ya mkurugenzi, lakini hakuna hatua zilizochukuliwa.

Baada ya malalamiko hayo, ndipo baraza hilo la madiwani kupitia Mwenyekiti wake, Daud Sichone, lilipomwagiza mkurugenzi wa halmashauri hiyo na Jeshi la Polisi kuwasaka watumishi hao na wafikishwe katika vyombo vya sheria ili wakajibu tuhuma zinazo wakabili.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Magreth Kakoyo, alikiri kuwapo kwa tuhuma hizo na kuahidi kutekeleza maagizo ya baraza hilo haraka iwezekanavyo ili wananchi waweze kupata haki yao ya huduma bora zinazotolewa na serikali.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack (kulia), akiwa na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (kushoto), wakiangalia pombe kali aina ya shujaa ambayo ilikuwa ikitoroshwa ili kukwepa kulipa kodi ya serikali, ikiwa ndani ya gari aina ya lori. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wakulima tumbaku waiangukia serikali

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa tumbaku wa Halmshauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kutoyaruhusu makampuni ya ununuzi wa zao hilo kusitisha mikataba ya ununuzi mpaka yakamilishe kununua tumbaku yote iliyozalishwa katika msimu uliopita.

Waliyabainisha hayo jana katika kikao cha kuitambulisha kampuni ya ununuzi ya zao la tumbaku katika msimu ujayo ya Petrobena katika Chama cha Msingi Ngokolo Halmashauri ya Ushetu, na kueleza kuwa mpaka sasa bado kuna tumbaku nyingi kwenye maghala haijapata wanunuzi.

Mariam Paul, mkulima alisema,mpaka sasa tumbaku iliyozalishwa katika msimu uliyopita haijapata mnunuzi, huku baadhi ya kampuni zilizoingia mikataba na wakulima zikisitisha kununua na kuondoka ikiwamo kampuni ya TLTC.

Naye Paschal Ndimbo, alisema wakulima wamepata hasara kwa msimu uliyopita na wengine kukosa fedha kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao, na kuiomba serikali kabla ya kutoa vibali kwa makampuni kuingia makubaliano ya kununua na tumbaku yote.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Emmanuel Charahani, alisema zaidi ya wakulima 14,800 nchini nzima hawataweza kulima tumbaku msimu ujao kutokana na baadhi ya kampuni zilizokuwa zikinunua zao hilo kusitisha ununuzi kutokana na madeni wanayodaiwa na serikali.

Alisema Wilaya ya Kahama ina vyama vya msingi 13, vyama vinane vilipata wanunuzi wa tumbaku, huku vyama vitano vya Mliza, Isolamageba, Mshikamano, Mweli, Twende wakati pamoja na Ibambala vimekosa wanunuzi wa kununua tumbaku yao.

Aliongeza: "Tunakosa wanunuzi wa tumbaku nchini, serikali inangalie namna bora ya kulipatia ufumbuzi kwa kukaa na wanunuzi na wazungumze kibiashara ili wanunuzi warudi kwa wakulima kuwahudumia, kununua na wakulima kuongeza uzalishaji.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, Michael Matomora, alisema baadhi ya makampuni kusitisha kununua tumbaku iliyozalishwa nje ya mikataba kumepunguza mapato kwenye halmashauri yake kwa zaidi ya asilimia 50.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Petrobena, Peter Kumalilwa, alisema wanatarajia kununua kilo 250,000 za tumbaku katika chama cha msingi Ngokolo na kama wakulima watazalisha vizuri kwa kuzingatia misingi ya kilimo cha kisasa, wataongeza kiwango cha ununuzi.

## Wagonjwa wa sukari, shinikizo washauriwa

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANAOUGUA maradhi ya kisukari na shinikizo la damu, wametakiwa kuacha kutumia dawa za miti shamba na badala yake watumie dawa wanazopewa na daktari.

Daktari wa Hospitali ya Chake-chake, Pemba, Ali Omar Khalifa, alisema kuna baadhi ya wagonjwa wa kisukari na shindikizo la damu wana tabia ya kutumia dawa za miti shamba, jambo ambalo sio sahihi.

Alisema ni vyema kwa wagonjwa hao kufuata ushauri wa daktari kuendelea kutumia dawa kwa usahihi na waache kutumia dawa za miti shamba, kwani sio salama na hazina viwango, jambo ambalo linaweza kuwasababishia maradhi mengine kama ya tumbo, figo na ini.

"Kuna baadhi ya wagonjwa hutumia dawa za miti shamba licha ya kupewa na dawa za hospitali, maradhi haya huwezi kupona moja kwa moja, lakini iwapo utafuata ushauri wa daktari na kutumia dawa kama ulivyoelekezwa yanaweza kukupa unafuu," alisema.

Alieleza licha ya elimu inayotolewa kwa wagonjwa hao, hawatumii dawa ipasavyo, jambo ambalo lisababisha kuongezeka kasi ya ugonjwa huo na hatimaye kusababisha vifo.

"Mgonjwa unampa dawa hizi katumie, lakini anapofika nyumbani anaziacha na anatafuta miti shamba, hili ni tatizo kubwa kwetu, hivyo tunawaomba wawe wasikivu na wafuate utaratibu, ili kuweza kufanikiwa," alieleza daktari huyo.

Dk. Khalifa alieleza kuwa kwa mwezi hupokea wagonjwa wapya kuanzia watatu hadi wanne wanaougua kisukari na hupokea wagonjwa wapya kuanzia watatu mpaka sita wanaougua shinikizo la damu.

"Kwa mwezi tuna jumla ya wagonjwa 1,200 wa kisukari na shinikizo la damu wanaokuja kliniki na wanaoendelea kupatiwa matibabu hospitalini hapa," alisema.

Alitaja athari za magonjwa hayo kuwa ni pamoja na kupata upofu, ulemavu, kukatwa viungo, maradhi ya figo, moyo, kiharusi na kuwa tegemezi katika familia.

Aliishauri jamii waache kutumia vilevi pamoja na kula vyakula hatarishi hasa vyenye mafuta, ili kujikinga na magonjwa ya kisukari pamoja na shinikizo la damu.

Mwananchi mmoja ambaye hakutaka kutajwa jina lake ambaye anasumbuliwa na ugonjwa wa kisukari, alisema ugonjwa huo ni hatari sana kuliko magonjwa mengine na kuiomba jamii kula vyakula vya asili, mboga na matunda.

"Maradhi ya kisukari sio mchezo jamani, huna raha ya maisha kwa sababu unapangiwa chakula (miiko) tofauti na maradhi men-

## HABARI KIMATAIFA

# Iran yaishinda Saudia kimikakati

**TEHRAN,** Iran

IRAN inashinda mapambano ya kimikakati ya ushawishi katika Mashariki ya Kati dhidi ya mpinzani wake, Saudi Arabia, kwa mujibu wa ripoti mpya ya taasisi ya kimataifa ya mafunzo ya kimikakati iliyo na makao yake mjini London.

Mahasimu wa kikanda wa Iran wametumia mabilioni ya dola kununua silaha katika mataifa ya Magharibi hususan kutoka Uingereza.

Japo Iran inakabiliwa na vikwazo, imetumia sehemu ndogo ya fedha hizo kujiimarishia ushawishi wake katika eneo la mashariki ya kati.

Iran ina ushawishi mkubwa kwa kudhibiti mzozo unaoendelea katika mataifa ya Syria, Lebanon, Iraq na Yemen.

**Ilikuwa mara ya kwanza Marekani kutaja sehemu ya serikali nyingine kama shirika la kigaidi la kigeni.**

Hatua ya Iran kubuni mtandao wa ushirikiano usiokuwa wa serikali kote Mashariki ya Kati, ambayo mara nyingi huitwa "wanamgambo wakala", sio jambo geni na limesaidia kuipa nguvu kubwa ya ushawishi.

Kupitia mtandao wa Hezbollah nchini Lebanon, taifa hilo la Kiislamu limekuwa likieneza falsafa ya mageuzi na kutanua wigo wake nje ya mipaka yake tangu kiongozi wa kidini Ayatollah Ruhullah Khomeini aliporejea mjini Tehran mwaka 1979.

Lakini ripoti hiyo ya IISS ya kurasa 217 inayofahamika kama "Mitandao ya Ushawishi ya Iran Mashariki ya Kati", inaangazia kwa kina ushawishi wa Iran katika eneo la Mashariki ya Kati.

Jamuhuri ya Kiislamu ya Iran, inasema ripoti hiyo imedhihirisha utendaji kazi wa kikosi chake Mashariki ya Kati kufikia hatua hiyo. Kiungo muhimu katika mapambano ya kimkakati ya ushawishi huo ni vikosi vya Kikurdi, ambavyo vinaendesha operesheni yake kwa ushirikiano na Jeshi la Ulinzi la Iran.

Vikosi vya Kikurdi na kiongozi wake, Meja Jenerali Qasem Soleimani, vinafanya kazi chini ya kiongozi mkuu wa kidini, Ayatollah Ali Khamanei, badala ya kufuata muundo wa kawaida wa kijeshi wa Iran.

Tangu Marekani ilipoivamia kijeshi Iraq na kuung'oa madarakani utawala wa Saddam Hussein mwaka 2003, vikosi vya Kikurdi vimeimarisha operesheni yake katika eneo karibu lote la mashariki ya kati, kwa kutoa mafunzo, kufadhili ununuzi wa silaha kwa mataifa yaliyo na ufungamano na Tehran.

April, Rais wa Marekani Donald Trump, aliorodhesha Jeshi la IRGC, ikiwamo vikosi vya Kikurdi kuwa "shirika la kigaidi la kigeni" (FTO).

Ilikuwa mara ya kwanza Marekani kutaja sehemu ya serikali nyingine kama shirika la kigaidi la kigeni.

Iran ilijibu madai hayo ya Trump kwa kutaja vikosi vya Marekani katika eneo la Ghuba kuwa kundi la kigaidi kama hatua ya kulipiza kisasi.

Jack Straw, ambaye alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza kutoka 2001 hadi 2006 na ambaye alizuru Iran mara kadhaa, anaamini kuwa jukumu la Jenerali Soleimani ni zaidi ya kamanda wa jeshi. **BBC**

# Aanzisha chama kipya Rwanda

**KIGALI,** Rwanda

MWANASIASA wa upinzani nchini Rwanda, Victoire Ingabire, amejiuzulu kuwa mkuu wa chama cha FDU na kuanzisha chama kipya cha kisiasa, Chama cha Maendeleo na Uhuru kwa Wote - "DALFA-UMURINZI".

Ingabire ameeleza sababu zilizompelekea kuchukua hatua hiyo ni kutokana na chama cha FDU kuwa nje ya Rwanda hivyo kinakuwa hakihusiani na hali halisi nchini Rwanda.

Katika mazungumzo na waandishi wa habari mjini Kigali, Victoire Ingabire ameeleza pia kuwa amechoka kuendelea kuongoza chama kwenye mtandao kwa sababu wafuasi wake wengi na wakuu wengine wa chama hicho wako nje ya nchi na kwamba wakati umewadia kuwa na chama kinachobainisha matatizo kikiwa ndani ya nchi.

Ingabire ameondoa wasiwasi wa kwamba amekisaliti FDU kwa manufaa ya chama tawala RPF.

"Kuna waliosema kwamba ninakwenda kuwa mpambe wa chama tawala RPF, sio kweli. Ni vizuri watu wafahamu kwamba siasa lazima ipige hatua." Alisema na kuongeza hisingewezekana kuendelea kuongoza chama kupitia mtandao. Nilizungumza na wafuasi wakuu wa FDU tukakubaliana kwamba heri kuwapo chama cha watu walioko ndani ya nchi kuliko kuwa na chama kilicho na uongozi nje ya nchi," Ingabire ameeleza.

Chama cha FDU Inkingi katika taarifa rasmi, kimetoa shukran kwa kujitolea kwa mwenyekiti huyo wa zamani Ingabire na kumtakia kila la kheri katika uzinduzi wa chama chake kipya Dalfa.

Kadhalika kimeeleza kwamba Justin Bahunga ndiye aliyeteuliwa kwa sasa kuwa kaimu mwenyekiti wa chama hicho, wakati kukisubiriwa kikao cha chama kuchukua hatua za kulijaza pengo hilo. **BBC**



Mwanasiasa wa upinzani nchini Rwanda, Victoire Ingabire, ameachana na chama chake cha zamani na kuunda chama kipya cha Dalfa. **PICHA: BBC**

# Wasaidia wenza kufanya sherehe ndoa

**CAPE TOWN,** Afrika Kusini

RAIA wa Afrika Kusini wametoa ofa kuwasaidia wenza kufanya sherehe ya ndoa waliokuwa wakitamani siku zote baada ya picha ya video za mwanaume aliyekuwa akimwomba mpenzi wake kwenye mgahawa wa chakula KFC wafunge ndoa kusambaa kwenye mitandao ya kijamii.

Video hiyo ilimwonesha mwanaume akiwa amepiga goti na kutoa pete kwa mpenziwe wakati walipokuwa wakila kuku. Mgahawa wa KFC ulisambaza video hiyo ikiomba msaada wa kuwatafuta wenza hao.

Baadaye wenza hao walifahamika kwa majina Bhut' Hector na Nonhlanhla, lakini haikuishia hapo tu. Baada ya muda mfupi watu waliokuwa hawafahamiani na wapenzi hao walianza kutoa ahadi ya kuwasaidia kupanga siku yao ya harusi, ikiwamo malazi wakati wa fungate na kutumbuiza siku ya sherehe.

"Ningependa kutoa ofa ya kutumbuiza kwenye harusi bure...Ninapenda mapenzi" aliandika katika ukurasa wake wa Twitter, msanii maarufu na mtunzi Zakes Bantwini.

Athari za mitandao ya kijamii zilikoleza katika maandalizi ya harusi hiyo kisha makampuni binafsi yakaanza kutoa zawadi mbalimbali.

"Maeneo ya fungate yanaonekana kuwa mbali. Mtu atahitaji kuwapeleka huko. Tutashughulikia," akaunti ya twitter ya kampuni ya magari ya

Audi ya Afrika Kusini ilieleza "Tungependa muungano wao uwe wa kipekee kwa kuwapa kurasa mbili za kwenye jarida letu ili waeleze hadithi yao nzuri ya mapenzi! Jarida la DRUM liliandika kwenye ukurasa wa Twitter.

Ofa za kila kitu kuanzia vilevi mpaka masufuria ya kupikia, nguo za michezo zilijitokeza siku ya Ijumaa, sambamba na michango ya maelfu ya pauni.

Kateka Malobola, mpita njia ambaye alirekodi picha ya video na kuiweka kwenye mtandao wa kijamii, alizungumzia furaha yake isiyo kifani kutokana na mchango wa raia wa nchi hiyo.

"Nilirekodi video hiyo na kuipeleka kwenye kikundi cha WhatsApp nikisema 'tazameni'! Kisha nikaiweka kwenye mtandao wa Facebook na Instagram, na kisha Boom! " Alieleza.

Wapenzi hao wamewashukuru wote wanaowatakia heri walipozungumza na kipindi cha Sowetan Live. Wapenzi hao pia wameiambia tovuti kuwa awali walioana mwaka 2012, lakini bwana harusi hakuridhika na pete alizonunua wakati huo na kutaka kumnunulia mke wake kitu kizuri zaidi.

"Sifanyi kazi hivyo sikuwa na fedha za kutosha kumpa Nonhlanhla harusi nzuri, mapambo ya vito lakini nilitaka kufanya kitu kidogo," Hector alisema.

"Asante Afrika kusini. Ukarimu wenu umetugusa kwa kweli.

Hatukufikiria kuwa hadithi yetu ya mapenzi ingewagusa wengi," waliongeza wapenzi hao.**BBC**

# Dk. Shoo awataka wahitimu kutumikia taifa kizalendo

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kirutheli Tanzania (KKKT), Dk. Frederick Shoo, amewataka wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu nchini kutumia vyema taaluma zao kuisaidia jamii na taifa kwa ujumla husan kwa kutanguliza mbele uzalendo.

Pia aliwataka kuwa na maadili wanapokwenda kazini kwa kuhakikisha kuwa wanafanyakazi kwa bidii na ufanisi ili kuwa mfano wa kuigwa.

Dk. Shoo alitoa wito huo juzi, jijini Dar es Salaam, wakati wa mahafali ya 13 ya Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es Salaam (TUDARCo). Katika mahafali hayo wahitimu 743 walitunukiwa vyeti katika ngazi mbalimbali za cheti, stashahada na shahada.

"Tunafurahi kuona TURDACo inatimiza yale malengo ambayo ndiyo ilikuwa kiu yetu, kutoa elimu kwa Watanzania kwa ubora zaidi, kutoa mchango kwa nchi yetu," alisema Dk. Shoo na kuongeza:

"Tutaendelea kukiboresha chuo chetu ikiwamo kuhakikisha kwamba tunaongeza wahadhiri wa kutosha wenye sifa."

Naye Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, alisema kanisa linaendelea kujivunia kutoa elimu bora na wataendelea kuhakikisha ada ya masomo katika vyuo vyake inaendana na maisha halisi ya wazazi na walezi wa wanafunzi.

"Hatutaki kuona ada inakuwa kikwazo wanafunzi kushindwa kusoma, Bodi ya Chuo itaendelea kujipanga na kuona inapanga ada za kumsaidia kila mwenye uhitaji wa elimu anaipata," alisema Askofu Malasusa.

Mkuu wa chuo hicho, Askofu Uswege Minga, aliwataka wahitimu wa chuo hicho kuendeleza maadili mema waliofundishwa ikiwamo matumizi mazuri ya lugha, kumcha Mungu na kuvaa nguo zinazoendana na maadili ya Kiafrika.

Baadhi ya wahitimu akiwamo Diana Akama wa Shahada ya Elimu, aliwataka wanafunzi wanaobaki chuoni na wanaotarajia kujiunga na vyuo kuhalikisha wanajiwekea malengo na kusoma kwa bidii.

Naye Mwandishi Mwandamizi wa gazeti hili, Salome Kitomari, aliyehitimu Shahada ya Mawasiliano ya Umma, aliwashauri wananahabari kukubali kurudi shuleni kuongeze maarifa.

"Unajua elimu haina mwisho, hata uko kazini, unapoona kwamba kuna umuhimu wa kujiongeza kielimu ni bora kufanya hivyo kwa kuwa unaongoza kitu kikubwa sana kichwani kwako, na utafanyakazi kwa kujiamini zaidi," alisema Kitomari na kuongeza:



Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tumaini, Dar es Salaam (TUDARCo), wakiwa wamenyanyua herufi za kifupisho cha chuo hicho, wakati wa mahafali ya 13 ya wahitimu 743 juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Vijana walengwa kujifunza mbinu za kibiashara

**Na Mwandishi Wetu**

KUTOKANA na uhitaji wa viongozi shupavu wenye uelewa kuhusu teknolojia nchini, wito umetolewa kwa wamiliki wa makampuni na mashirika mbalimbali kuwekeza kwa vijana na wajasiriamali wabunifu ili kuisaidia serikali kupunguza tatizo la uhaba wa ajira nchini.

Wito huo ulitolewa jijini Dar es Salaam na kampuni ya masuala ya kiteknolojia Smart Lab kupitia kwa Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Smart Codes, Edwin Bruno, wakati akizungumza katika warsha iliyopewa jina la 'Corporate Unwind'.

Warsha hiyo ambayo imefanyika kwa mara ya pili, hufanyika kila baada ya miezi mitatu kwa kuwakutanisha vijana wajasiriamali wabunifu wa masuala ya kiteknolojia na wawekezaji au wamiliki wa makampuni waliofanikiwa ili kuwajenga kibiashara na kuwapatia mbinu za kukua zaidi kulingana na mawazo waliyobuni.

Bruno alisema Corporate Unwind pia hulenga kujenga daraja kati ya wavumbuzi wakubwa na wachanga kwa kuwakutanisha pamoja na kujifunza mbinu mbalimbali za kukua kibiashara. Alisema Corporate Unwind msimu huu imekuja na kauli mbiu inayosema "Uongozi bora unaochochea ukuaji kwenye sekta ya kibenki" inalenga kuwaandaa vijana kuwa viongozi bora katika sekta ya benki nchini.

Aidha, akizungumza katika jukwaa hilo, mzungumzaji mkuu wa msimu wa pili wa Corporate Unwind ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Standard Chartered Tanzania, Sanjay Rughani, alisema, benki yake imelenga kutoa kipaumbele kwa vijana kujifunza maarifa mbalimbali katika sekta hiyo ili kukua kiuchumi.

# Waliotenguliwa sasa kushiriki uchaguzi mitaa

INATOKA UK. 8

"Hatufanyi kazi kwa mihemko, tunafanya kazi kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi, kila mtu ana uhuru wake kujitoa au kubaki," alisema Jafo.

Kadhalika, alisema wagombea wa uchaguzi huo wataanza kupokea ratiba kutoka vyama vya siasa kwa ajili ya kufanya kampeni kuanzia jana hadi leo, na kwamba wasimamizi waanze kuandaa karatasi za kupigia kura.

### VYAMA VYATOA MASHARTI

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, viongozi wa vyama vya upinzani, walisema kuwa hawakubaliana na uamuzi huo kwa kuwa mchakato ulishaharibiwa toka mwanzo na wagombea wengi kunyimwa haki zao.

Akizungumza na gazeti hili, Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema hawawezi kuhalalisha uharamu kwa kuwa mchakato wote umeshanajisiwa katika hatua zote za kuchukua na kurejesha fomu kwa kuwa kuna watu ofisi zilifungwa wiki nzima.

Alitolea mfano wa maeneo ya Maswa mkoani Simiyu na Liwale mkoani Lindi, ambako wiki nzima walikuwa wanahangaika kurejesha fomu baada ya watendaji kuzikimbia ofisi na hakuna waziri aliyechukua hatua.

"Hatuwezi kuingia kwenye mtego aliotuwekea, mchakato uanze upya, iundwe kamati huru yenye uwakilishi wa vyama vyote, mchakato wa kuchukua kurejesha uanze upya ili uchaguzi ufanyike katika mazingira ya kuaminiana, amani na uhakika," alisema na kuongeza:

"Hatutahalalisha haramu hata siku moja. Mchakato wa uchaguzi uanze upya kwa kuundwa kwa kamati huru ya kusimamia uchaguzi chini ya Tamisemi yenye wajumbe kutoka vyama vyote vya siasa. Uchaguzi wa Novemba 24, ufutwe, itangazwe tarehe mpya na mchakato uanze upya," alisema.

Kwa mujibu wa Zitto, uhalisia ni kuwa wagombea watashiriki uchaguzi, lakini wasimamizi watawatangaza watu waliowaacha kwenye mchakato wa awali.

"Kama waliweza kufuta watu bila sababu ya msingi basi hawashindwi kuwatangaza waliowaacha awali kama washindi. Walisema wagombea wa upinzani wameshindwa kujaza fomu, sasa fomu walizonazo zimerekebishwa saa ngapi?" Alihoji Zitto.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Bara, John Mnyika, alisema wasimamizi wa uchaguzi huo wameshapoteza uhalali wa kusimamia uchaguzi huo kwa kuwaengua wagombea bila sababu za msingi.

"Uchaguzi usimamiwe na watu huru ili mchakato uwe huru, takwimu za CCM kupita bila kupingwa siyo halali. Waziri kama angekuwa na nia njema asingetangaza kuwa CCM imepita bila kupingwa wakati anajua kuna waliozuiliwa bila sababu," alisema Mnyika.

### CHADEMA YAPIGA MARUFUKU

Chadema imepiga marufuku jina na nembo za chama hicho kutumika kwenye uchaguzi huo kwa kuwa chama hicho tayari kimekwishajitoa.

Aidha, Mnyika amewataka wanachama wa chama hicho kuendelea kutekeleza maamuzi ya Kamati Kuu ya chama hicho ya kuandika barua ya kujitoa katika uchaguzi huo kwa kile alichodai kuwa umekosa uhalali baada ya wasimamizi na wasimamizi wasaidizi kuuvuruga.

"Waziri Jafo hawezi kutengenisha mgombea na chama kauli zake zinaonyesha ama hajui kanuni au anapotosha kwa makusudi kanuni za 14, 15, 16 zinaweka bayana sifa za mgombea," alisema Mnyika.

Mbali na kupiga marufuku kutumika kwa nembo na jina la chama hicho katika uchaguzi, chama hicho pia kimeitaka serikali kufuta uchaguzi huo na kutaka kuanza upya kwa mchakato wa uchaguzi baada ya kupata Tume huru ya kusimamia chaguzi nchini.

### NCCR-MAGEUZI YAJITOA

Wakati huo huo, Chama cha NCCR-Mageuzi kimejitoa kwenye uchaguzi huo mwaka huu kwa sababu ya majina ya wagombea wake kukatwa.

Pia kimeviomba vyama vya upinzani nchini kutafuta njia ya maridhiano na serikali ili kuendelee kuilinda amani ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Mwenyekiti wa chama hicho, James Mbatia, alisema wameamua 'kuweka mpira kwapani' kutokana na majina ya wagombea wa chama hicho kukatwa. Alisema katika majina 35,567 waliyopitishwa na NCCR-Mageuzi kugombea nafasi mbalimbali nchini majina yaliyorejeshwa ni 149.

Mbatia alisema jambo hilo halikubaliki, hivyo wameamua kujitoa katika kinyang'anyiro hicho.

"Baada ya kufanya kikao cha Kamati Kuu tumeagiza wagombea wetu wajitoe na wadhamini, waliowadhamini ambayo ni matawi, tumeagiza waondoe udhamini au wagombea wajiondoe wenyewe.

"Sisi hatushiriki uchaguzi huu wanatakiwa kufuata kanuni, hatuwezi tukaliacha Taifa linapelekwa ovyo, hii ni hatari sana," alisema.

***Imeandikwa na Gwamaka Alipipi, Paul Mabeja, DODOMA, na Enock Charles, DAR***

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA 2 ENEO MOJA ZINAUZWA** Zipo Ukonga Mombasa. Ya mbele mjengo wa kisasa vyumba 4 nyingine chumba na sebule 4 kiwanja robo eka. Za kupaua. Bei maelewano. Piga simu: 0719 619444 / 0782 574669.

**VIWANJA VITATU VINAUZWA,** NO.1-1341-1890 SQM NO. 2-1342- 1391 SQM NO.3 1343- 1556 SQM BLOCK A KISUKURU-TABATA. SIMU. 0754 857523/0786 857523

### NAFASI ZA KAZI

**Wanahitajika wanaume wenye umri kuanzia miaka 30 hadi 45** kwa nafasi za udereva (Ikiwemo Class C, C1, C2 na C3). Wanahitajika wanawake wenye umri kuanzia miaka 25 hadi 35 kwa nafasi za mauzo (sales za bidhaa). Mshahara wa kuvutia utatolewa. Mawasiliano piga 0714 634 046. Piga simu kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni tu.

### 2 ACRE YARD FOR RENT

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**

## NIPASHE NI JIBU LAKO

### KUPOTEA KWA CHETI



**BARAKA WILLIAM** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2652-0076** kilichotolewa na KOM SEKONDARI mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MOR/MOR/RB/442490/2019.**

115511302

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DEOGRATIAS PATRICK MKWAMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 806 ATE SUZUKI ESCUDO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KJN/MAG/RB/44955/2019.**

115511402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**TANGA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi No; 160/2019**

**Kwa: Yeyote anayehusika**

Ombi la MFAUME JAMBIA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **RUKIA MBWANA YUSUFU**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 27/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 08/10/2019

215511502

**JAHMURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**HATI YA KIAPO**

**Mimi AHMAD ABDALLAH JANGA** wa TANGA kwa niaba ya Taasisi ya **AL-MUSTAFAA ISLAMIC CHARITABLE FOUNDATION** nikiwa mtu mzima na akili zangu timamu bila ya kushawishiwa na mtu yoyote naapa na kuthibitisha mbele ya HAkimu Mahakamani kama ifuatavyo:

1. Kwamba Taasisi ya **AL-MUSTAFAA ISLAMIC CHARITABLLE FOUNDATION** ni wamiliki wa kiwanja Na.9 kitalu 120 kilichopo Ngamiani Tanga Mjini.
2. Kwamba kiwanja hicho tuliuziwa na Mdugu **MOHAMED RASHID GOMBE.**
3. Kwamba kwa bahati mbaya hati ya kumiliki kiwanja hicho imepotea ikiwa bado ina jina la **MOHAMED RASHID GOMBE** na jitihada za kuitafuta zimefanyika bila mafanikio .
4. Kwamba Kwa hiki tunaomba Idara ya Ardhi na Mipango Miji Tanga itupatie hati ya kumiliki kiwanja hicho kwa jina la **MOHAMED RASHID GOMBE.**

**UTHIBITISHO**
Nathibitisha kuwa yote niliyotamka hapo juu ni kweli tupu na kwa kadri ya sharia viapo

215511602

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa**

**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0767 223311**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# CHELSEA KUWAPIGA BEI PEDRO, GIROUD




**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea imeripotiwa kwamba, itakuwa tayari kusikiliza ofa za kuwauza wachezaji wake watatu katika dirisha dogo la Januari.

Kwa mujibu wa ESPN, Chelsea inataka nyota wake hao wakiongozwa na Olivier Giroud mwenye umri wa miaka, 32 ambaye hana nafasi katika kikosi cha kwanza.

Giroud anahusishwa kurudi nyumbani kwao Ufaransa lakini Chelsea pia inaweza kuachana na Pedro mwenye umri wa miaka, 32 ambaye amekuwa akisakwa na klabu za Ligi Kuu China baada ya Kocha, Frank Lampard kutumia makinda zaidi katika nafasi yake.

Inafahamika kuwa Giroud na Pedro mikataba yao wote inamalizika Juni mwakani na wataruhusiwa kuanza mazungumzo na klabu nyingine kuanzia Januari.

Giroud akiwa chini ya Lampard ameanza kwenye mechi moja tu, huku pia beki wa kushoto, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 28 ambaye amepoteza nafasi yake kwa Emerson ataruhusiwa kuondoka, huku pia ikidaiwa kwamba Lampard anamsaka beki wa kushoto wa Leicester City, Ben Chilwell.

# Enrique atajwa kumrithi Unai Arsenal

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal wanaripotiwa wanafikiria kumchukua, Luis Enrique kwa sababu wanaamini ni mtu mwafaka wa kwenda kuchukua mikoba ya Unai Emery.

Arsenal mambo yao si mambo huko kwenye Ligi Kuu England, juzi Jumamosi walikubali kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Leicester City na kocha wao Emery amezidi kuwa kwenye presha kubwa ya kupata matokeo baada ya hali kuwa ngumu kwa siku za karibuni.

Kabla ya mechi hiyo iliyopigwa kwenye Uwanja wa King Power, Arsenal walikuwa nyuma kwa pointi sita kuifikia nne bora, huku mpango wao mkubwa kwa msimu huu ni kumaliza ndani ya timu nne za juu ili kukamatia tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Kwa sasa mabosi wakubwa wa Arsenal bado wana imani na Emery, lakini kuendelea kuboronga uvumilivu unaweza kuwashinda na kumfungulia mlango wa kutokea Mhispania huyo.

Kwa mujibu wa taarifa ya kutoka Hispania, maofisa wa Arsenal wanamtazama kocha wa zamani wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Hispania, Enrique kwenye orodha ya makocha ambao wanahitaji wakatoe huduma zao pale Emirates wakati Emery atakapofunguliwa mlango wa kutokea.

Enrique mwenye umri wa miaka 49, hivi karibuni aliachana na kikosi cha Hispania kutokana na sababu zake binafsi na haieleweki kama atakuwa tayari kurudi haraka kwenye soka kupiga kazi.





# Scholes: Solskjaer sasa ameanza kupata kikosi

**MANCHESTER,** England

MCHEZAJI wa zamani wa Manchester United, Paul Scholes, amesema kuwa Kocha, Ole Gunnar Solskjaer, sasa ameanza kupata kikosi bora na cha ushindi.

Na pia kikosi hicho ndicho kinachofaa kuanza kwenye kila mechi kama wanahitaji matokeo matamu baada ya ushindi wa 3-0 dhidi ya Partizan Belgrade kwenye Ligi ya Europa.

United imetinga hatua ya mtoano kwenye michuano hiyo ikiwa bado ina mechi mbili za kucheza kwenye kundi lake, ambapo mechi hiyo ya Alhamisi usiku, washambuliaji wake wote aliowaanzisha, Mason Greenwood, Anthony Martial na Marcus Rashford walitikisa nyavu.

Scholes sasa anaamini kikosi bora cha Solskjaer kinaanza kupatikana, wakati timu hiyo ikiwa na shughuli pevu ya kupanda mlima huko kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya huku ikitambua imeshatinga kwenye hatua ya 32 bora ya Ligi ya Europa.

Gwiji huyo wa Old Trafford alisema bado kuna swali zito la nani anayefaa kuwa patna wa Harry Maguire kwenye beki ya kati, lakini yeye anamwona Axel Tuanzebe anastahili kuanza ndipo atakapopona majeraha yake na hapo anampiga benchi Victor Lindelof.

Kikosi hicho cha Scholes, anasema Paul Pogba atacheza na Scott McTominay kwenye kiungo, wakati Danie James, Rashford na Greenwood watacheza nyuma ya Martial kwenye safu ya ushambuliaji.

HABARI MICHEZO

# Kiwango Madrid chamkuna Zidane

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amekisifia kikosi chake cha Real Madrid baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Eibar kwa kusema "walicheza kwa kiwango bora" na kuwataka wachezaji wake kuendelea kuwa kwenye ubora huo.

Sergio Ramos na Karim Benzema kila mmoja alifunga penalti katika kipindi cha kwanza kwenye mchezo huo uliopigwa uwanja wa Ipurua.

Federico Valverde aliongeza bao la nne na la kwanza kwake kuifungia klabu hiyo na hivyo kuifanya Madrid kuwa pointi sawa na Barcelona kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Hispania, La Liga.

"Najisikia vizuri kushinda hapa," alisema Zidane akiiambia Movistar. "Huu sio uwanja rahisi kuja kucheza. Mara nyingi kila timu inayokuja hapa inafungwa, lakini tulianza vizuri.

"Kipindi cha kwanza kilikuwa bora. Tulitawala maeneo yote na tuliwakabili vizuri wapinzani wetu.

"Tulicheza vizuri zaidi kwa kutawala mchezo na kuwa kwenye nafasi nzuri ya kufunga na tulitumia vizuri kila nafasi tuliyopata.

"Timu ilicheza katika kiwango bora kabisa na kwa uhakika tulikuwa kwenye wakati mzuri zaidi."

Madrid sasa imeshinda mechi nne kati ya tano katika mashindano yote tangu ilipofungwa bao 1-0 na Real Mallorca Oktoba 19, mwaka huu.

"Tulifanya kazi ya ziada na tuliamini kila tulichokuwa tukifanya," aliongeza kusema. "Mchezo dhidi ya Mallorca ulikuwa mgumu kwa upande wetu.

"Lakini kuanzia pale tumekuwa tukicheza kwa umakini mkubwa na kuhakikisha tunakuwa bora katika kila dakika uwanjani. Tunatakiwa kuendelea kucheza kwa kiwango hiki."

Kikosi hicho cha Zidane sasa kimecheza mechi tano bila kuruhusu nyavu zake kutikiswa katika mashindano yote, ikiwa ni kwa mara ya kwanza tangu Septemba 2015, ambapo walifungwa kwa jumla mabao 16.






# MESSI AIFIKIA REKODI YA RONALDO KWA 'HAT-TRICK'

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi alifunga penalti na kwa adhabu ndogo mara mbili wakati Barcelona wakiibuka na ushindi wa 4-1 dhidi ya Celta Vigo na kufikia rekodi ya Cristiano Ronaldo ya kufunga 'hat-trick' nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu Hispania, La Liga.

Mabao hayo matatu ya Messi kwenye mchezo uliopigwa pale katika dimba la Camp Nou kuliwafanya Barca kukaa kileleni mwa msimamo baada ya kufungwa na Levante na kutoka sare na Sparta Prague.

Wote sasa, Messi na Ronaldo wamefunga 'hat-trick' 34 kwenye Ligi Kuu Hispania, ingawa mshambuliaji huyo wa zamani wa Real Madrid awali alicheza kule Sporting CP na Manchester United kabla ya kujiunga na Juventus mwaka jana, alikaa muda mfupi kwenye ligi hiyo.

Mreno huyo alikaa pale Madrid kwa misimu tisa na aliweka rekodi ya kufunga hat-trick nyingi zaidi mbele ya Alfredo Di Stefano (22) na Ferenc Puskas (12).

Messi ambaye huu ni msimu wake wa 16 pale Barcelona, huku akiwa na mabao nane kwenye mechi saba za La Liga ana nafasi ya kuipita rekodi hiyo.

# *Tuchel amtaka Cavani apambane*

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel, amesema kwamba Edinson Cavani atahitaji kujifunza kushindana na Mauro Icardi kuanza kwenye kikosi cha kwanza.

Cavani alianza kikosi cha kwanza kwa PSG kwa mara ya kwanza tangu Agosti 25 wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Brest, lakini hakuwa na mchango mkubwa kwa kikosi chake hicho.

Alitolewa dakika ya 80 na nafasi yake kuchukuliwa na Icardi, ambaye alifunga bao la ushindi dakika tano baada ya Samuel Grandsir kusawazisha lile la Angel Di Maria alilofunga kipindi cha kwanza.

Tuchel alizungumzia ushindani uliopo kwa wawili hao na kumpa changamoto raia huyo wa Uruguay kwamba, anatakiwa kupigania namba.

"Sio rahisi kuwachezesha wote wawili kwenye safu ya ushambuliaji, ni lazima apambane kupata namba," alisema akiiambia Canal+.

"Yeye anatakiwa kuhakikisha kwamba, anapata nafasi ya kucheza kwa kuonyesha kiwango chake uwanjani."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# WENGER: SIJAOMBA KUFUNDISHA BAYERN

Lakini Mfaransa huyo asema yuko tayari kwa mazungumzo endapo atafuatwa na vigogo hao...

**LONDON,** England

ALIYEKUWA kocha wa Arsenal ya England, Arsene Wenger, amekanusha taarifa za kuzungumza na mwenyekiti wa FC Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge, kwa ajili ya kumwomba kazi.

**Wenger amekanusha taarifa hizo, baada ya jarida la Bild la Ujerumani kuthibitisha kulikuwapo na mazungumzo baina ya pande hizo mbili.**

Kocha huyo kutoka nchini Ufaransa amesema hakuwahi na wala hatowahi kufanya mazungumzo ya kuomba kazi kwenye klabu yoyote, zaidi ya kusubiri ofa, kama ilivyo taratibu za mchezo wa soka.

Bayern Munich wapo kwenye mchakato wa kumsaka kocha mpya, baada kumtimua, Niko Kovac, baada ya kikosi chao kufungwa mabao 5-1 dhidi ya Eintracht Frankfurt.

Wenger ana rekodi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England mara tatu, Kombe la FA mara saba, katika kipindi cha ukufunzi wake wa miaka 22 akiwa na kikosi cha Arsenal, kabla ya kuondoka mwishoni mwa msimu wa 2017-18. Mzee huyo mwenye umri wa miaka 70, kwa sasa anafanya shughuli za uchambuzi wa soka kwenye televisheni ya beIN Sports, na aliitumia nafasi hiyo kukanusha taarifa za kuomba kazi FC Bayern Munich.

"Niliwahi kukaribia kujiunga na Bayern miaka kadhaa iliyopita, lakini sikufanya hivyo kwa sababu nilikua na majukumu mazito nikiwa na Arsenal, sijawahi na wala sitowahi kuomba nafasi ya kazi kama ilivyoripotiwa katika jariba la Bild," alisema Wenger.

"Hakukua na mazungumzo yoyote kati yangu na mwenyekiti wa Bayern Munich, na nimeshangazwa kwa taarifa hizi, sijui zimetokea wapi."

Bayern Munich kwa sasa inashika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi ya Bundesliga, ikiwa nyuma kwa alama nne dhidi ya Borussia Mönchengladbach wanaoongoza msimamo huo.

## ZISIKUPITE

### ENRIQUE ANUKIA ARSENAL

ARSENAL iko katika mazungumzo na Kocha wa zamani wa Timu ya Taifa ya Hispania na Barcelona, Luis Enrique, ili kuchukua mikoba ya Unai Emery, ambaye anaelekea kutimuliwa. ***(El Confidencial, via Metro)***

### UNITED YAREJEA KWA ZAHA

KWA mara nyingine, mabosi wa Manchester United wamemtaja straika wa Crystal Palace, Wilfried Zaha (27), kuwa ni miongoni mwa wachezaji wanaowahitaji katika kikosi chao. ***(The Sun on Sunday)***

### LENO ANUKIA BAYERN

GOLIKIPA wa Arsenal Mjerumani Bernd Leno, ambaye ana umri wa miaka 27, ametajwa kuwindwa na Bayern Munich. Wajerumani hao wanataka Leno awe kipa chaguo la kwanza la timu yao. ***(The Sun on Sunday)***

### SPURS YAMFUATA DEPAY

TOTTENHAM imesema iko tayari kuweka ofa ya pauni milioni 50 ili kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay (25), ambaye alihamia Lyon ya Ufaransa akitokea Manchester United Januari 2017. ***(Sunday Mirror)***

### SERGEJ ATAJWA CHELSEA

CHELSEA itafanya mchakato wa kumsajili awali kiungo wa Lazio na Timu ya Taifa ya Serbia, Sergej Milinkovic-Savic (24), katika dirisha dogo la Januari kama adhabu yao ya kusajili itaondolewa. ***(Sunday Mirror)***

### GIROUD AUZWA BEI CHEE

KLABU ya Chelsea imesema inahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 5 kwa klabu yoyote inayotaka kumsajili straika wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud (33), katika kipindi cha dirisha dogo la Januari. ***(Sunday Express)***

### PSG YAJIPANGA KWA MBAPPE

PARIS St-Germain imeanza kufanya mazungumzo ya kumpa mkataba mpya straika wake Mfaransa Kylian Mbappé, ambaye ana umri wa miaka 20, lakini bado haijaweka mezani kiasi cha fedha atakayolipwa nyota huyo. ***(L'Equipe, via Marca)***

### KLOPP: LOVREN HAONDOKI

KOCHA wa Liverpool, Jürgen Klopp, amesema hatakubali kuona beki wa kati wa Timu ya Taifa ya Croatia, Dejan Lovren (30), anaondoka katika klabu hiyo kwenye kipindi cha dirisha la usajili la Januari. ***(Football Insider)***

### POGBA KUTOA WATATU JUVE

JUVENTUS inatarajia kuwatoa Mario Mandzukic (33), Emre Can (25), Daniele Rugani (25) na Blaise Matuidi (32), kwa Manchester United ili kuhakikisha wanampata kiungo Mfaransa Paul Pogba (26). ***(Tuttosport, via Sunday Express)***

### EVERTON YAINGIA SOKONI

EVERTON inajiandaa kumuuza golikipa wake, Maarten Stekelenburg katika dirisha la usajili Januari. Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 37 anatarajia kumaliza mkataba wake na klabu hiyo ifikapo mwisho wa msimu. ***(Football Insider)***

# HABARI MICHEZO

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 9 | 7 | 0 | 1 | 4 | 16 | 22 |
| 2. Kagera Sugar | 10 | 6 | 2 | 2 | 14 | 8 | 22 |
| 3. Lipuli | 10 | 5 | 3 | 2 | 18 | 10 | 18 |
| 4. Tanzania Prisons | 10 | 4 | 6 | 0 | 13 | 8 | 16 |
| 5. Namungo | 10 | 5 | 1 | 4 | 7 | 7 | 16 |
| 6. JKT Tanzania | 10 | 4 | 3 | 3 | 7 | 7 | 15 |
| 7. Mtibwa Sugar | 11 | 3 | 3 | 4 | 10 | 11 | 15 |
| 8. Ruvu Shooting | 10 | 4 | 3 | 3 | 8 | 8 | 15 |
| 9. Alliance | 10 | 3 | 5 | 2 | 8 | 7 | 14 |
| 10. Mbao | 11 | 2 | 5 | 3 | 10 | 10 | 14 |
| 11. Azam | 7 | 4 | 1 | 2 | 7 | 4 | 13 |
| 12. Polisi Tanzania | 9 | 4 | 1 | 3 | 9 | 10 | 13 |
| 13. Coastal Union | 10 | 3 | 2 | 5 | 8 | 9 | 11 |
| 14. Mwadui | 11 | 2 | 5 | 3 | 7 | 9 | 11 |
| 15. Young Africans | 5 | 3 | 1 | 1 | 6 | 4 | 10 |
| 16. Kinondoni MC | 7 | 2 | 2 | 3 | 4 | 6 | 8 |
| 17. Biashara United | 9 | 2 | 2 | 5 | 5 | 9 | 8 |
| 18. Mbeya City | 9 | 1 | 5 | 3 | 7 | 15 | 8 |
| 19. Ndanda | 8 | 1 | 4 | 3 | 6 | 8 | 7 |
| 20. Singida United | 10 | 0 | 4 | 6 | 4 | 15 | 4 |



Kaimu Balozi wa Marekani nchini, Dk. Inmi Patterson (wa pili kutoka kulia), akimvalisha medali mchezaji wa kikapu baada ya kumalizika kwa mafunzo ya wachezaji vijana wa umri chini ya miaka 14, 16, 17 na 18 yaliyofanyika juzi kwenye viwanja vya JMK Park jijini Dar es Salaam. Mafunzo ya yosso hao yalifadhiliwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Marekani kwa kushirikiana na NBA na ubalozi wa nchi hiyo. **PICHA: UBALOZI WA MAREKANI**

## Mikoa sita kusaka 'Mr Tanzania'

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya kusaka bingwa wa kutunisha misuli nchini (Mr Tanzania 2019) yamepangwa kufanyika Novemba 29, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Katibu Mkuu wa Chama cha Mchezo wa Kutunisha Misuli Tanzania (TBBF), Francis Mapugilo, alisema jana kuwa maandalizi kwa ajili ya mashindano hayo yanaendelea vizuri na washiriki wanatarajia kuingia kambini ifikapo Novemba 26, mwaka huu.

Mapugilo alisema kuwa wanatarajia michuano ya mwaka huu itakuwa na ushindani na katika kuboresha, wameipanga kwenye madaraja mawili.

Aliongeza kuwa wanatarajia kutoa zawadi nzuri za kuhamasisha wachezaji na tayari mikoa sita imethibitisha kushiriki mashindano hayo ambayo ni pamoja na Mwanza, Tabora, Dodoma, Mbeya, Zanzibar na wenyeji Dar es Salaam.

# STRAIKA STARS ATARAJIA MAMBO MAZURI IJUMAA

**Na Shufaa Lyimo**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Kelvin John, amesema licha ya kuwa na umri mdogo, anaamini anaweza kuipa matokeo makubwa timu hiyo endapo atapata nafasi ya kucheza katika mechi ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Afrika (Afcon 2021), dhidi ya Equtorial Guinea, itakayochezwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Kelvin, ambaye alianza kutamba akiwa na kikosi cha Serengeti Boys, amesema kuwa anajiandaa kuonyesha soka la kiwango cha juu ili kuhakikisha Stars inapata matokeo mazuri katika mchezo huo wa kwanza.

**Kelvin alisema kuwa kikosi chao kimejiandaa vema na wanatarajia watafuata maelekezo kutoka kwa walimu wao na hatimaye kupata ushindi katika mechi hiyo na nyingine zinazofuata.**

"Nimejiandaa kujituma, nitaendelea kumsikiliza mwalimu kwa makini ili niweze kuisaidia timu, ninataka kutimiza ndoto za kufika mbali, lengo langu ni kufika mbali zaidi, kikubwa ni kumsikiliza mwalimu pamoja na kushirikiana na wachezaji wenzangu ili tuipe heshima nchi yetu," alisema Kelvin.

Mshambuliaji huyo pia aliwataka wachezaji wenye umri kama wake wajitume zaidi ili wapate nafasi kama aliyoipata yeye na kuwakumbusha hakuna jambo lisilowezekana.

"Naomba wachezaji wenzangu wajitume kucheza ili waweze kupata nafasi kama niliyoipata mimi ya kuichezea timu ya Taifa," alisema kinda huyo.

Aliongeza kuwa, anawaomba Watanzania wajitokeze kwa wingi kuishuhudia timu hiyo ili wafanye vizuri katika mchezo huo wa kwanza na baadaye ugenini dhidi ya Libya. Kikosi cha Stars kinachofundishwa na Mrundi Etienne Ndayiragije na wasaidizi wake, Juma Mgunda na Suleiman Matola, kimeshaingia kambini kujiandaa na mechi hizo mbili huku kikiwa hakina mabadiliko makubwa.




Msanii wa filamu nchini, Ahmed Salim 'Gabo' (wa pili kushoto), akimkabidhi zawadi ya seti ya DStv kutoka MultiChoice Tanzania, Ashura Selemani wa jijini Dar es Salaam (katikati), wakati wa uzinduzi wa kampeni maalum ijulikanayo kama "Shangwe za Sikukuu na DStv", ambayo itadumu hadi Desemba 31, mwaka huu na itawawezesha wateja wapya wa kampuni hiyo kuunganishwa kwa Sh. 99,000. **PICHA: DSTV**

# *Gofu yatumika kusaidia macho*

**Na Margaret Malisa**

WANAMICHEZO 90 kutoka sehemu mbalimbali walishiriki mashindano maalumu ya gofu yaliyoandaliwa na klabu ya Lions ya jijini Dar es Salaam (Mzizima) kwa lengo la kukusanya fedha za kusaidia watu wenye matatizo ya macho, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Lion Shabir Khanbhai, alisema kuwa kwa muda mrefu wamekuwa wakitoa huduma za matibabu ya macho bure kwa wagonjwa katika mikoa yote ya Tanzania.

Alisema kuwa huduma hiyo imekuwa ikitolewa mara nne kwa mwaka na wanaamini husaidia kupunguza tatizo hilo kwa Watanzania wenzao.

"Huduma za macho tunazozitoa ni kuanzia vipimo, kutoa miwani, dawa na pia upasuaji endapo utahitajika," alisema kiongozi huyo.

Aliitaka jamii kujitokeza kucheki afya ya jicho pindi wanapoasikia matangazo ya klabu yao wakati wanaweka kambi katika eneo lolote hapa nchini kwa lengo la kuendesha huduma wanazozifanya kuhusu magonjwa ya macho.

"Jicho ndio kila kitu kwenye mwili wa binadamu, ushauri wangu ni kila mtu anapaswa kujua afya ya jicho lake, ndio maana sisi pamoja na huduma nyingine kwa jamii, pia tukajikita zaidi kusaidia suala zima la afya ya macho," alisema mwenyekiti huyo.

Abdallah Gunda, mmoja wa washiriki wa mashindano hayo, alisema kuwa mchezo huo ni mzuri lakini bado idadi ya wanawake wanaoshiriki imekuwa ndogo kutokana na kukosa mwamko wa kuucheza, hivyo amewashauri kujitokeza kwa wingi ili kujifunza.

# Michezo

Jumatatu Novemba 11, 2019
Nipashe



Chelsea kuwapiga bei Giroud, Pedro UKURASA 28



Straika wa Leicester, Jamie Vardy akipiga shuti lililotinga wavuni moja kwa moja na kumwacha kipa wa Arsenal, Bernd Leno, akiruka bila mafanikio katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa King Power juzi. Arsenal ilichapwa mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## Wachezaji Stars wasaka ufundi

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), jana kilianza mazoezi rasmi kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea mchezo wao wa kuwania tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2021), dhidi ya Equatorial Guinea, utakaochezwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Juma Mgunda, aliliambia gazeti hili kuwa, wachezaji wote wanaocheza Ligi Kuu Tanzania Bara waliripoti kambini na kuanza programu maalumu kuelekea mchezo huo ambao wanatarajia wataanza vema kampeni ya michuano hiyo.

Mgunda alisema kuwa kila mmoja katika kikosi hicho anafahamu umuhimu wa kupata matokeo mazuri, hivyo watajipanga imara zaidi kuhakikisha malengo ya pamoja ya timu na nchi yanatimia.

"Tuliingia kambini tangu jana (juzi), na leo (jana) asubuhi tumeanza mazoezi, hali ni nzuri, kila mmoja hapa anafurahia mazoezi, tutakuwa na programu maalumu kuelekea mechi ya Ijumaa na ile ya Libya, zinapishana siku chake, hivyo ni lazima tuweke mikakati itakayofanana na nguvu inayohitajika," alisema kocha huyo.

# Vita ubingwa Bara mapema

## Mchuano wake wazidi kuwa mkali msimu huu, huku vigogo Simba, Yanga vikibanwa...

**Na Adam Fungamwangwo**

HUKU mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu zikiwa zimesimama kwa muda kupisha kalenda ya kimataifa, hali imekuwa ni vuta nikuvute, timu nyingi zikionekana kuimarika zaidi tofauti na msimu kadhaa iliyopita.

**Tumeshuhudia misimu iliyopita tukiona hadi kufikia wakati huu timu za Simba, Yanga, Azam, Mtibwa Sugar zikifuatana juu, lakini hali imekuwa tofauti kabisa kwa msimu huu, timu zisizotarajiwa ndizo zinamfukuza bingwa mtetezi kileleni, tena kwa tofauti ya pointi ndogo.**

Mpaka kufikia raundi ya 11, misimu kadhaa iliyopita ilishuhudia timu zikigawana makundi matatu, zinazopigania kutwaa ubingwa, kutafuta pointi za kufanya zisishuke daraja na pia zinazopigana kufa na kupona ili zisiteremke.

Msimu huu timu zote kuanzia juu na kushuka chini hazijapishana sana pointi, hivyo kufanya kinyang'anyiro cha kuwania ubingwa wa msimu 2019/20 kuonekana kuwa kigumu.

Inawezekana kabisa msimu huu ligi imekuwa ngumu kwa sababu timu nne za juu huenda zote au tatu zikashiriki michuano ya kimataifa mwakani, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, huku timu sita zikiteremka daraja.

Ufafanuzi ni kwamba timu itakayoshika nafasi ya nne, inaweza kucheza Kombe la Shirikisho kama timu tatu za juu moja wapo itakuwa bingwa wa Kombe la FA.

Huko chini ni kwamba timu nne zitashuka daraja moja kwa moja na nyingine mbili zitacheza 'play off', na timu za Daraja la Kwanza Tanzania Bara, hivyo zinaweza nazo zisirudi hata moja.

Msimu huu hakuna timu yenye uhakika wa kushinda hata ikicheza nyumbani kwake. Timu inayojiandaa vema imekuwa ikipata ushindi hata ugenini.

Simba ambayo mpaka sasa inaongoza ligi ikiwa na pointi 22, ikicheza mechi tisa, iko kwenye wakati mgumu kwani chini yake kuna Kagera Sugar ambayo imefikisha pointi 20, mbili tu nyuma ya vinara hao, ikiwa imecheza mechi 10.

Ni Kagera Sugar ambao ilikuwa "almanusura" msimu huu icheze Daraja la Kwanza, kwani ilirejea Ligi Kuu kwa kucheza 'play off' na kuifunga Pamba ya Mwanza na kupata tiketi ya kurejea Ligi Kuu tena, lakini sasa iko katika nafasi ya pili na tena ikifanya vema zaidi kwenye viwanja vya ugenini.

Prisons ambayo msimu uliopita haikuwa vizuri, msimu huu imejizatiti kwani pamoja na kukamata nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu kwa kujikusanyia pointi 19 katika michezo 11 iliyocheza, lakini hadi sasa ndio timu pekee haijapoteza mechi yoyote ile.

Lipuli ya Iringa, iliyotetemesha msimu uliopita, inaonekana labda msimu huu haitokuwa vizuri kutokana na kuondoka kwa kocha wake Selemani Matola na baadhi ya wachezaji akiwano, William Lucian 'Gallas' aliyekwenda Polisi Tanzania na Miraji Athumani aliyetua kwa mabingwa watetezi, lakini makali yake yameongezeka na inakamata nafasi ya nne kwa pointi 18, ikiwa tayari imeshacheza mechi 10.

Ingizo jipya kwenye Ligi Kuu msimu huu, Namungo FC inakamata nafasi ya tano ikiwa na pointi 16 kwa michezo 10 iliyocheza, huku Mtibwa Sugar, timu ambayo miaka kadhaa nyuma kwenye mechi za mwanzo ilikuwa ikitetemesha iko kwenye nafasi ya sita kwa pointi 15, Ruvu Shooting ikiwa kwenye nafasi ya saba kwa pointi hizo hizo 15.

Alliance, timu iliyopanda msimu uliopita na kuanza kwa kusuasua kabla ya kuzinduka mwishoni, msimu huu imeanza na moto, kwani mpaka sasa inakamata nafasi ya nane, ikiwa na pointi 14.

Katika hali inayoonyesha kuwa msimu huu hakuna lelemama, timu zilizozoea kukaa juu kama Azam FC inakamata nafasi ya 10 kwa kuwa na pointi 13, ikicheza michezo saba, Yanga ikiwa kwenye nafasi ya 15 kwa pointi 10, yenyewe ikicheza mechi tano.

Baadhi ya timu ambazo msimu uliopita zilikuwa moto wa kuotea mbali, lakini bado zinaonekana hazijaamka vizuri ni Mbao FC iliyo kwenye nafasi ya tisa kwa pointi 14, JKT Tanzania nafasi ya 12, ikiwa na pointi 12, KMC nafasi ya 16 kwa pointi nane, Mbeya City nafasi ya 18, ikiwa na pointi nane, Ndanda FC nafasi ya 19 ikiwa na pointi zake saba, na Singida United ambayo inaburuza mkia ikiwa na pointi nne.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042